**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma naUtawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |

| | |
|---|---|
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31. Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 32.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasiza Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 43.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 44.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 47.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 50.Mhe. Marina Joel Thomas | Kateuliwa na Rais |
| 51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |

| | |
|---|---|
| 52.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 54.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 56.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Jimbo la Mpendae |
| 57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Nafasi za Wanawake |
| 58.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 62.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 63.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 64.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 65.Mhe. Rashid Seif Suleiman | Jimbo la Ziwani |
| 66.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 69.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 70.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 71.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |

| | |
|---|---|
| 75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Jimbo la Dole |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 25 Julai, 2012**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Na. 192**

**Kupatikana kwa Huduma ya Krini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma –** Aliuliza

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya yote naomba uniruhusu niseme japo neno moja kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kupata bosi mpya, nimpongeze kwa hilo.

Naishukuru serikali kwa kuamua kuanzisha kutoa huduma ya krini tangu 1984 ingawa baadae krini hizo zilisita kutoa huduma na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Hata hivyo, serikali ilijitahidi kuona huduma hiyo inaendelea kupatikana na ndio maana imewapatia wananchi krini nyengine hivi karibuni.

a) Jee, Mhe. Waziri unaweza kutuambia krini hiyo ni ya aina gani, imetengenezwa nchi gani, kila moja imenunuliwa kiasi gani na nani aliyenunua.
b) Jee, Mhe. Waziri kila krini ina uwezo wa kubeba tani ngapi.
c) Jee, krini hizo 2 sasa zimeweza kutatua matatizo ya bandari.
d) Ni sababu gani zilizopelekea karibu miaka 30 serikali kushindwa kuagiza krini, kwa kuwa zinaleta tija kwa serikali pamoja na wananchi kupata mizigo kwa wakati muafaka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 192 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, krini mbili mpya ziliopo bandarini hivi sasa ni aina ya *mobile crane.* Krini hizi zimetengenezwa na Kampuni ya Manitowoc/Grove ya Marekani. Bei ya krini hizo ni CIF Zanzibar zenye thamani ya Dola za Kimarekani 898,639 kwa krini kubwa na krini ndogo ina thamani ya Dola za Kimarekani 352,783. Krini hizo zimenunuliwa na Shirika la Bandari.
b) Krini kubwa ina uwezo wa kubeba hadi tani 75 na krini ndogo ina uwezo wa kubeba hadi tani 18.

c) Krini hizo mbili zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la krini bandarini. Hata hivyo, bado bandari inahitaji angalau krini nyengine mbili za ziada kwa bandari ya Malindi na krini kama hizo kwa ajili ya bandari za Pemba, yaani Mkoani na Wete.
d) Sababu zilizopelekea shirika kutoagiza krini kwa miaka kadhaa iliyopita zinatokana na ufinyu wa bajeti ya shirika pamoja na kuwezo kwa vipaumbele vyengine kama vile gati yenyewe, boti za kusukumia meli, boti za rubani na kadhalika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya kutoridhisha kabisa ya Mhe. Naibu Waziri.

Jee, utakuwa tayari Mhe. Naibu Waziri kwa Kamati ya Mawasiliano na Miundombinu kwenda kuchunguza jambo hili kupata ukweli wa jambo hili; kwa vile ukizingatia hizi pesa ni mkopo kutoka PBZ kama milioni moja na laki tatu.

Pili, ulijibu katika jawabu lako kwa krini kubwa ina uwezo wa kubeba tani 75 ambapo jambo hili si la kweli kabisa Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya kikao hiki kwenda kuhakikisha kuwa inaweza kubeba tani hizo 75 au itakuwa kama kawaida yako, maana Mwanamapinduzi alipokuuliza swali moja ukamwambia kuwa upo tayari kwenda Pemba na mpaka leo hupo tayari kwenda Pemba.

Huu ni mwezi wa Ramadhani hivi sasa kuna tatizo kubwa kule, na wananchi wanakuwa wanaumia wamefunga kubeba magunia ya mbatata. Una mpango gani wa dharura kuwasaidia wananchi wetu kwenye mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, ninashukuru kuwa kunipatia nafasi ya kujibu maswali ya Mhe. Mwakilishi ya nyongeza yenye vifungu moja, mbili na tatu kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nijibu hilo la mwisho ya kwamba ahadi yangu ya kutaka kwenda Pemba sijaipinga, nilichosema kama nitatolewa nauli mimi nipo tayari kwenda Pemba. Sasa kama Mhe. Jaku kama atanitolea nauli hata kesho mimi nitakwenda nirudi nije nitimize kazi zangu ambazo nilizopangiwa.

a) Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa kauli thabiti kabisa namthibitishia na ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yetu ipo tayari kushirikiana na kuendeleza ushirikiano wetu uliopo kati ya wizara na Kamati husika, na tunawakaribisha kwa mikono miwili waje wakague krini hizo ili kuona ufanisi wa utendaji kazi.

b) Mhe. Naibu Spika, krini hii kubwa ina uwezo wa kunyanyua tani 75. Tatizo liliopo inawezekana ikawa tafsiri inatuzonga. Maana *specification* tulizowapelekea, tani 75 zinazonyanyuliwa inategemea na uwezo wa ile *radius* yenyewe ilivyo. Kila kitu kinapokuwa mbali ule mkonga wa ile krini kunyanyua kitu kizito hakiwezi. Kwa hivyo *radius* inapokuwa karibu hiyo krini ina uwezo wa kunyanyua mpaka tani 75. Sasa hilo tumeliona na tumewaambia wenzetu wa Shirika la Bandari waangalie vizuri *specification* kama itakuwa wamekosana kwenye *specification* zao na uwezo wa krini kunyanyua kulingana kwamba *distance* kutoka katika *radius* basi tunawaambia waweze kuwasiliana

na kampuni husika, ili waweze njia mbadala nyengine ikiwa na suala la kuwarejeshea na kutafuta krini nyengine.

c) Mhe. Naibu Spika, swali la tatu sikumfahamu maudhui yake Mhe. Mwakilishi, anaposema kwamba kuna wananchi wanabeba mizigo kwa magunia tuwaonee huruma katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Naomba tu anielekeze ni kitu gani anachokihitaji nimwambie ili niweze kumjibu vizuri Mhe. Mwakilishi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku maelezo zaidi ili afahamu Mhe. Naibu Waziri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ninachomwambia huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na kwamba serikali yetu imeshindwa kutokana na hali ya fedha na bajeti yake inavyokwenda hivi sasa hasa ukiangalia hii Wizara ya Miundombinu, mwezi huu wakasaidiwa angalau kwa dharura hiyo krini mpya, maana yake tokea kuletwa haijafanya kazi hiyo hata siku moja, *at least* kwa mwezi huu wa Ramadhani na jawabu lake Mheshimiwa ananiambia mimi nimuulize atakuwa tayari kwenda kuhakikisha hizo tani 75 baada ya kumaliza hiki kikao. Maana siwezi kumwambia mtu mzima muongo na yeye ni bosi wangu huyu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, naona Mhe. Mwakilishi anauliza swali jengine jipya.

Suala la uwezo wa krini kunyanyua tani 75, mimi nimeeleza kwamba ile krini yenyewe ilivyo inategemea na *radius* ni kama wewe unaposimama hapa ndoo unaweza kuinyanyua lakini ndoo ikiwa kwa mbali huwezi kuinyanyua. Na nilichokisema kama hawa watendaji wetu wa Shirika la Bandari wamekosea katika *specification* zao kinyume na hiyo krini ilivyo, wakae na liwepo suala la kuwarejeshea kwa kampuni iliyohusika.

Lakini swali lake la kwanza aliuliza suala la wafanyakazi kwamba wanabeba magunia kwenye mwezi wa Ramadhani ndicho ambacho sijakisikia. Sasa naomba Mhe. Mwakilishi unielekeze unachokihitaji ni kitu gani, hao watu wanaopata katika mwezi wa Ramadhani kubeba mizigo kwa mabega.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, amesema kanunua krini mbili kubwa, moja ina thamani karibu Dola laki nane na upuuzi na ya pili ni laki tatu. Sasa kwa muda huu moja angeweka angalau kwa dharura kuwasaidia wale wananchi wa nchi hii waliokuwa wanyonge wakwezi, wakulima na wachukuzi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa swali umelifahamu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, tumeeleza kwamba krini mbili hizi zimesaidia Shirika la Bandari katika kufanya kazi na ndio malengo ya kununua hizi krini.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza maswali mawili Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi juu ya safari yake ya kwenda Pemba ambayo amezungumza na Mhe. Mwakilishi, amesema kwamba atakapopewa nauli atakwenda Pemba. Mimi ninataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, jee safari hii ya Pemba ni safari ya kibinafsi au ni safari ya kiserikali.

Pili kama ni safari ya kiserikali atakubali na Baraza hili kwamba itakapofika bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, fungu la safari za kikazi tusimuidhinishie safari hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa heshima na taadhima kubwa sana itakapokuja na bajeti yetu mafungu yetu yote mutupitishie likiwemo hili fungu la safari za kikazi. Lakini suala la msingi kwamba safari ile ambayo niidhinishiwe nauli ilikuwa ni safari maalum ya Mhe. Mwakilishi.

Kwa hivyo kama ilivyokuwa ni safari ya Mhe. Mwakilishi ndio mwenye safari yake, na mimi sina pesa sijajipangia hiyo safari na yeye Mhe. Mwakilishi ana safari yake basi namuomba tu aendelee kunifadhili hiyo safari kwa kunipatia nauli ili tuweze kwenda.

**UTARATIBU**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Umeulizwa safari watakayokwenda huko Pemba ni safari ya kikazi au safari ya binafsi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Ni safari ya Mhe. Mwakilishi.

**Mhe. Naibu Spika**: Ya binafsi au ya kikazi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Ni safari ya Mhe. Mwakilishi.

**Na. 196**

**Kuwepo kwa Sehemu za Watembea kwa**
**Miguu katika Ujenzi wa Barabara**

**Mhe. Hassan Hamad Omar –** Aliuliza:

Ili kupunguza ajali na usumbufu kwa watumiaji wa barabara zetu, ni muhimu kuwa na sehemu maalum za watembea kwa miguu (*side walks*)

a) Ni kwa nini barabara zinazojengwa hapa Zanzibar hazizingatii kuwepo kwa sehemu hizo.
b) Wizara ina mpango gani wa kutengeneza sehemu maalum kwa watembea kwa miguu kwa barabara ambazo zimeshajengwa na hazikuwa na sehemu hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 196 kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, barabara zote zinazojengwa hapa Zanzibar zinazingatia uwezo wa sehemu maalum za wapitao kwa miguu. Jambo la kuzingatia ni kwamba upana wa jamii yetu kuhusiana na sehemu hizo juu ya matumizi ya uwepo wake, sio barabara zote ambazo sehemu hizo zimejengwa kwa alama maalum za kuwajuulisha wale wote waendao kwa miguu.

   Mhe. Naibu Spika, kwa mfano barabara ya Kinazini hadi Bububu iliyojengwa miaka ya 1980 ina sehemu maalum ya waendao kwa miguu na baiskeli, kwa bahati mbaya sana sehemu hiyo haitumiki kama ilivyokusudiwa na badala yake kuna baadhi kama maeneo, kama vile eneo la Mahurubi, Sharifumsa yamegeuzwa kuwa ni sehemu ya soko kwa kupanga mafungu ya mihogo, viazi na kadhalika.

   Kwa upande mwengine barabara zinazojengwa hivi karibuni zimezingatia suala la sehemu maalum za waendao kwa miguu na waendesha baiskeli. Maeneo hayo ni mule pembezoni mwa barabara, yaani michoro ya barabara tunatekeleza. Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, ukiangalia barabara yetu ya Amani/Dunga, barabara inayotoka Dunga kuelekea Upenja, Mfenesini hadi Bumbwini, Mazizini hadi Fumba, Makunduchi hadi Paje. Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imekuwa ikizingatia suala la ujenzi wa sehemu maalum ya waendao kwa miguu wakati wa matengenezo makubwa ya barabara. Kwa mfano barabara ya Kinazini hadi Malindi nayo pia imezingitiwa.

b) Kwa maeneo ambayo hayana sehemu hizo maalum, wizara imezingatia kuweka hasa wakati wa matengenezo makubwa ya barabara hizo. Kwa mfano kwenye mradi wa barabara zinazoingia mjini suala hili limezingatiwa na litapewa kipaumbele maalum kuhakikisha kwamba huduma hiyo inapatikana.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu yako Mhe. Naibu Waziri nilikuwa ninataka kukuuliza swali moja la nyongeza.

Barabara nyingi mpya zinazojengwa hivi sasa zinakosa maegesho ambayo yanatakiwa kuwepo kwa ajili ya kusimamia daladala. Jee ni lini serikali au wizara yako itaanza kufikiria suala hilo la kuweka maegesho kwa ajili ya kusimamia daladala.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara zetu nyingi zinazojengwa tunakosa hiyo sehemu kwa ajili ya kuegesha magari yanapokuwa safarini. Lakini katika huu mradi wetu mkubwa wa barabara zinazoingia mjini suala hilo nalo limezingatiwa kwa maeneo maalum baada ya kukaa na wahusika wakiwemo wenzetu wa Usafiri na Leseni na wadau wengine wanaohusiana na

masuala ya usalama barabarani yatakayoelekezwa maeneo maalum kwa ajili ya *parking* za magari yanazofanya safari barabarani.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali langu la nyongeza, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa ahadi yake ya wiki mbili kunitengenezea barabara ya jimbo langu kunitilia lami kwamba jana zote zimekamilika zote, ninamshukuru sana kwa hilo.

Lakini baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Ukiachilia masuala ya kutembea pembezoni mwa barabara, lakini barabara zetu zinazojengwa hivi sasa zinaonekana kuwa zina kasoro mbili kuu, nazo ni ukosefu wa *drainage* na kingo za pembeni ambazo zinaleta uchafuzi wa barabara kwa nyakati za mvua. Jee, ni sababu gani za msingi zinazopelekea barabara nyingi zinazojengwa hivi sasa kukosa mambo hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, sijamfahamu.

**Mhe. Naibu Spika:** Anasema hajakufahamu, hebu sema kidogo kidogo**.**

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namuuliza Mhe. Naibu Waziri barabara zetu nyingi ambazo zinajengwa hivi sasa zinakosa baadhi ya sifa ikiwemo mambo ya *drainage* na kingo za barabara; ambazo zinapelelekea uchafuzi wa barabara kwa nyakati za mvua. Ni sababu gani za msingi zinazopelekea barabara zetu zinazotengenezwa zikiwa hazina mambo hayo, yaani hazitiliwi *drainage* pembeni pamoja na kingo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:**Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara zetu nyingi ziliopo mjini zimekosa hiyo *drainage*. Tatizo la *drainage* ni tatizo pana, maana linahusisha wenzetu wa Baraza la Manispaa lakini pia wajenzi na wapangaji wa mji nao pia linawahusu.

Tunapotaka kufanya *drainage* kwa barabara hizi tunalazimika tuingie gharama kubwa sana, kwa sababu maeneo mengi yanayopita barabara hizi tayari yamevamiwa na majengo. Lakini ni imani yetu kwamba barabara ziliopo nje ya mji tutaanza na utaratibu huo wa kuhakikisha kwamba hizo *drainage* zinawekwa. Lakini kwa hivi sasa barabara ziliopo katika maeneo ya Magomeni tayari kuna mradi ule unaofadhiliwa na World Bank, kuna utaratibu mzuri ambao tutaweza kuchukua mtaro wa kupeleka mpaka baharini maeneo ya Kilimani.

Matarajio yetu kwamba barabara zile zitanusurika na kutuama kwa maji na huduma ya *drainage* itakuwa imepatikana. Lakini jambo la msingi ambalo serikali kulichukulia suala hili nalo ni kweli lina umuhimu, kwani tutakapojenga *drainage* tutakuwa tunaiongezea barabara muda wake wa kuishi na kuweza kutumika, lakini pia kuondoa usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

Suala la kingo za barabara Mhe. Naibu Spika, bado barabara zetu tunazojenga zina maeneo ya kutosha ya kingo, na ukiangalia barabara zetu tunazozijenga baada ya mwishoni mwa barabara kunakuwa na alama ya mchoro wa manjano wa barabara, wataalamu wanaita ni *shoulder, shoulder* ile ndio matumizi hayo ya kingo kwa ajili ya wapitao kwa miguu, walemavu na watu wengine ili kuweza kutoa huduma kama maeneo ya Kianga.

Lakini jambo la msingi ni kuomba tu wananchi wetu waendelee kutii sheria ziliopo za nchi kwa kupisha barabara katika maeneo yake na wasivamie; na kama kuna taasisi ya serikali basi tunapotoa vibali tuzingatie kwamba kibali hakitoendana kinyume na sheria za hifadhi ya barabara.

## KAULI ZA MAWAZIRI

(Kauli ya Serikali Kuhusu Tukio la Kuzama kwa Meli ya MV SKAGIT Iliyotokea Tarehe 18/07/2012 Katika Eneo la Bahari ya Chumbe

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tena kuwepo hapa na kuendelea na shughuli zetu za kawaida.

Aidha nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuja kujibu maswali mbali mbali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana Wajumbe kwa maswali yao ya msingi yenye nia ya kujenga ili tupate ufumbuzi muafaka wa kushughulikia matatizo yetu yanayotukabili.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kukushukuru kwa kunipa dakika 45 na mimi nitajitahidi nijibu kwa utaratibu ambao nisizidi muda ambao umenipa. Ninaamini nitajitahidi utosheleze haja.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba uniruhusu nitoe taarifa ya ajali kutokana na kazi inayofanywa na vijana wa uokozi kwa ajili ya kuokoa au kuibua miili iliyokuwa haijapatikana. Mpaka jana jioni tumeweza kuona miili 21 hapa Zanzibar na miili 5 ilionekana kule Bagamoyo. Lakini kutokana na hali ilivyokuwa ilibidi izikwe huko Bagamoyo.

Kwa hivyo mpaka sasa kwa siku ya jana tumeweza kuona miili 26. Hivyo sasa jumla ya waliofariki wote itakuwa ni 104 na walioonekana wakiwa hai ni 146. Kwa hivyo watu 250 tayari wameshajulikana.

Hivyo kwa mujibu wa manisfesto ile bado watu 40. Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kwanza uniruhusu niwataje Waheshimiwa Wawakilishi waliochangia hoja hii ili nisiendelee kurudia rudia kila mara kuwataja tena, kwa sababu ya muda uliojitokeza.

Mhe Naibu Spika, Mheshimiwa wa kwanza hoja maswali yaliyoulizwa ambapo na yeye pia alitoa taarifa kama kwa mujibu wa taratibu zetu za Kibaraza – Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma

2. Mhe. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Mohammed Haji Khalid
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
10. Mhe. Saleh Nassor Juma
11. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
12. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
13. Mhe. Rufai Said Rufai
14. Mhe. Hassan Hamad Omar
15. Mhe. Asha Bakari Makame
16. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
17. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
18. Mhe. Fatma Mbarouk Said
19. Mhe. Salmin Awadh Salmin
20. Mhe. Asaa Othman Hamad
21. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
22. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk
23. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
24. Mhe. Nassor Salim Ali
25. Mhe. Hamad Masoud Hamad

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali maswali yao yalikuwa ni ya msingi na nia yake yalikuwa ni ya kujenga; ili tuweze kurekebisha kasoro za hapa na pale zinazojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli nchi yetu imekumbwa na janga kubwa la uzamaji wa meli ambapo serikali, wananchi wote jambo hili limetusikitisha sana, limetuhuzunisha na sote kwa pamoja linatuuma, kwa sababu waliopoteza maisha na walioumia ni ndugu zetu, marafiki zetu, wapenzi wetu na ni wananchi wenzetu. Kwa vyovyote vile ni jambo gumu, kubwa, na kwa sote linatusikitisha.

Kwa niaba ya serikali naomba nitoe pole kwa wale wote walioguswa na msiba huu. Lakini vile vile niwatakie malazi mema wale ambao wametangulia mbele ya haki na wale walioumia tunawaombea dua wapoe haraka.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili limejitokeza sana baada ya serikali kuchukua hatua ya kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika shughuli za kibiashara, hasa katika sekta hii ya usafiri wa baharini na angani.

Tuliporuhusu sekta hii iweze kuchukua nafasi ya kutoa huduma za usafiri, nia yetu ilikuwa ni kuwapunguzia wananchi wetu mzigo wa matatizo katika sekta ya usafiri. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, baadhi ambao wamejitokeza kuingia kutoa huduma hii ya usafiri

uwezo wao ni mdogo, na vile vile kitaaluma uwezo wao ni mdogo na hii inatokana na sekta binafsi iliopo Zanzibar, ni wachache sana ambao wana uwezo mkubwa.

Sasa matokeo hayo Mhe. Naibu Spika ndio maana wengi wamekimbilia kununua meli chakavu na matokeo yake yamekuwa yanaleta athari kubwa sana kwa nchi yetu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo; na kwa sababu kwa njia moja ama nyengine, sasa uchakavu wa meli hiyo unaathiri maisha ya watu wetu, inabidi serikali ifanye uamuzi mwengine kwa nia ya kuvipunguza ama kuviondoa kabisa vyombo vichakavu visiweze kufanya shughuli zake katika maeneo ya bahari yetu au maji yetu ya sehemu ya Zanzibar, hasa kwa huduma za Zanzibar/Dar es Salaam, Zanzibar/Pemba na kadhalika.

Kwa msingi huo, serikali imekusudia kufanya mapitio makubwa ya sheria ili kuweka utaratibu mpya wa viwango vya meli ambavyo vitaruhusiwa kufanya shughuli za usafiri kati ya visiwa vyetu. Na nia kwamba meli zote ambazo sasa zitakuja kutoa huduma katika usafiri wa Zanzibar inabidi zitimize viwango vinavyotakiwa na meli hizo zisizidi umri wa miaka 15.

Kwa msingi huo meli yoyote ambayo itazidi miaka 15 toka kuundwa kwake haitoruhusiwa kufanya kazi za usafirishaji katika maeneo yetu ya Zanzibar. Sasa hivi serikali imekusudia kuzifanyia uchunguzi meli zote zilizopo ili zile zote ambazo hazitimizi viwango itabidi zifungiwe na zisiendelee na shughuli za kutoa huduma za usafiri nchini kwetu.

Hapa lazima niwaombe sana wananchi watuvumilie, kwa sababu nina hakika kutokana na utaratibu huo itapunguza sana huduma za usafiri kati ya visiwa vyetu. Lakini kutokana na hali ilivyovifikia sasa hatuna budi tuchukue hatua nzito japo ni ngumu lakini kuhakikisha usalama wa watu wetu unakuwepo.

Vile vile leo nilisikia redio ikizungumzia wamiliki wa kampuni hii ya Seagull Sea Transport ikisema kwamba hawajapata taarifa rasmi ya kusimamishwa kwa meli ya MV Kalama. Hapa ninaposema ninasema katika chombo kikubwa cha serikali, uamuzi wa serikali tumeifungia MV. Kalama isiendelee kufanya shughuli zake katika visiwa vyetu.

Kwa hivyo, huo ni uamuzi wa serikali na hayo ndio maamuzi rasmi na wahusika tunawataka leo hii wawaandikie barua wamiliki hawa ili usafiri wa MV Kalama hauruhusiwi kufanyakazi katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Mara moja taasisi ya *ZMA* ikishirikiana na *SUMATRA* na vyombo vyengine husika vichukue hatua ya kufanya ukaguzi wa meli zote chakavu ili zile meli ambazo hazifai kufanya usafiri katika visiwa vyetu ziweze kusimamishwa haraka sana na zisiendelee kutoa usafiri. Ili wananchi wetu wasipate hasara zaidi ya kununua vyombo ambavyo hatokubalika hapa Zanzibar, itabidi mwenye nia yoyote yule ya kutaka kuleta chombo chake Zanzibar basi awasiliane na wahusika *ZMA* ili kama ya kununua wataalamu kwanza wakakifanyie uchunguzi ili ionekane ubora, uwezo na umri wake na ndio baadae kiweze kuruhusiwa kuingia Zanzibar. Hatutaki Zanzibar iwe dampo ya kuleta meli mbovu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana wafanyabiashara washirikiane na taasii yetu hii ili kuhakikisha vyombo vinavyokuja hapa ni vizima na madhubuti. Ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wale wanaonunua vyombo vipya vyenye kutimiza viwango na inaonesha wazi kwamba wenye vyombo vipya wanaweza kufanya kazi nzuri na zinaweza kusaidia usalama

wa wananchi wetu. Kwa hivyo, serikali itatoa vivutio maalum kwa wale ambao wataagiza meli mpya zitakazoweza kutoa huduma bora na zitakazoweza kuwahakikishia maisha na usalama wa watu wetu unafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imekusudia kuimarisha huduma za ukaguzi na vile vile imekusudia kuimarisha vikosi vyake vya uokozi ili viwezi kwenda na wakati. Ni kweli vikosi vyetu vya uokozi vina matatizo makubwa sana ya vyombo na zana za kisasa. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali kuhakikisha hilo linafanyika. Lakini kutokana na hali yetu ya uchumi, jambo hili hatuwezi kulifanya kwa mara moja, nia yetu ni kulifanya, lakini nyote ni mashahidi uwezo wetu wa kiuchumi hauturuhusu sasa hivi kuwa na *helicopter* tunazozihitaji kwa ajili ya uokoaji, kuwa na *rescue boat* tunazozihitaji, kuwa na vyombo vya kuinulia meli wakati inapozama na kuwa na vyombo mbali mbali vinavyohitajika katika shughuli nzima za uokoaji, ni *challenge* yetu pamoja Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wote.

Mhe. Naibu Spika, sasa ni wakati wetu Wanzanzibari kushirikiana ili kuhakikisha kwamba tunauimarisha uchumi wetu. Siri kubwa ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu ni hali ya usalama na utulivu wa nchi yetu, ndio itakayotusaidia katika kuimarisha uchumi wetu na wakati uchumi unaimarika ndio utaotuwezesha kutoa mapato mazuri ya kutoa huduma za msingi katika nchi yetu. Kwa hivyo, jambo la msingi sana ni Wazanzibari tushirikiane kulinda amani, utulivu, umoja na upendo ili kuhakikisha kwamba sasa tunatazama namna bora ya kuimarisha uchumi ili Serikali ipate uwezo wa kutosha wa kuweza kutoa huduma zinazotakiwa kwa watu wake. Kwa hivyo, *challenge* kubwa iliyokuwa mbele yetu ni upungufu wa fedha au uwezo mdogowa fedha za kununulia vifaa. Tungependa leo hii Serikali iwe imenunua meli mpya na vyombo vipya ili tuweze kutoa huduma nzuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada zake za kutafuta meli mpya na naamini Mwenyezi Mungu akitujaalia muda sio mrefu nchi yetu itakuwa na meli mpya ili tuweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu. Vile vile serikali itachukua jitihada maalum ya kuwakaribisha wawekezaji ambao watakuwa na nia ya kuleta meli mpya ili ziweze kutoa huduma bora katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, lilizungumziwa suala la Kamati ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kukabiliana na Maafa ipo kisheria na inaongozwa na Mwenyekiti Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wajumbe wake wengine ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Waziri wa Afya, Wakuu wa Mikoa yote wa Unguja na Pemba na Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Mhe. Mwanasheria Mkuu, pamoja na Makatibu wao Wakuu. Hiyo ndio Kamati ya Kukabiliana na Maafa, pamoja na Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Naibu Spika, kamati hii kazi yake kubwa ni kuratibu ili kuwaunganisha pamoja wale wenye sekta muhimu au wenye sekta zinazohusiana na mambo ya majanga pale yanapotokea, ili kuwe na *commanding post* moja ya kuweza kuwa na mawasiliano yanayoowana ili tuweze kutoa huduma hii vizuri. Kwa hivyo, kamagi hii ina wajumbe hao niliowataja na kazi yake kubwa ni kuratibu masuala haya yanapotokea ili kuunganisha timu hii iwe moja na iweze kufanyakazi kwa

pamoja, ili kuepuka kufanya makosa na iwe na mawasiliano vizuri na iweze kutenda kazi zake vizuri.

Kwa yaliyotokea Mhe. Naibu Spika, kamati hii nataka niipongeze sana, ilifanya kazi nzuri sana. Vile vile tuna wajibu wa kuwapongeza vijana wetu wanaoendelea na shughuli za uokozi wamefanyakazi kubwa na nzuri na wanaendelea kuifanya. Waheshimiwa Wajumbe kazi ile ni ngumu sana na hali yake ni ngumu na yaliyotokea siku ile yalikuwa katika hali ngumu sana, maana upepo ulikuwa mkali na mawimbi makubwa. Kwa hivyo na hawa waliojitolea vile vile walijitolea na maisha yao, kwa sababu lolote lingeweza kutokea. Kwa hivyo, lazima tuwapongeze watu hawa kutokana na hali ambayo imetokea. Mpaka hivi leo juhudi wanazozifanya za kuokoa maiti mheshimiwa ukienda ndio utapata kuona hali yenyewe ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, sote tunajua maiti za baharini, lakini vijana wetu hawa wamejitolea. Vijana hawa ni wa vikosi vya SMZ pamoja na watu binafsi. Mhe. Hassan jana hapa alisema, na huko mbele nitavitaja vile vikundi ambavyo vimeshiriki kikamilifu katika kutoa huduma hiyo. Kwa kweli wanafanyakazi kubwa, nzuri na ni kazi ya kupigiwa mfano. Ni vizuri pale ambapo pamefanyika vizuri basi tuwape pongezi zao, tusiendelee kuwalaumu vijana hawa, tunapowalaumu tunawavunja moyo. Wametusikitikia sana jana tulikuwa na baadhi ya wajumbe namna ambavyo wametoa malalamiko yao. kwa hivyo, ni vizuri tuwape moyo, wanafanyakazi katika mazingira magumu sana.

Mhe. Naibu Spika, hali yetu ya kiuchumi nasema tena ni ndogo, haiwezi kumudu mahitajio yote tunayotaka kufanya kwa hivi sasa, japokuwa tuna nia njema ya kutaka tuwe na vifaa bora, lakini bado hali ni ngumu. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa tuwape pongezi sana kutokana na kazi kubwa na nzito ambayo wameweza kuifanya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la meli, serikali ina nia ya kununua meli mpya ili iweze kutoa huduma za kisasa. Vile vile Serikali ina nia ya kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya uokoaji. Hivi sasa kuna baadhi jitihada zimeanza kufanywa ili kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa wa uokoaji wanapata zana za kisasa zaidi na suala hilo tutakwenda hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ubani wa *MV Spice Islander*. Waheshimiwa Wajumbe ni kweli kwamba tumeweza kutoa ubani kwa wale tu ambao majina yao yaliorozeshwa na tume, na huo ndio ulikuwa muongozo wa serikali. Lakini wako watu ambao kwa uhakika kabisa walikutwa na mkasa ule wa kuzama kwa meli ya *MV Spice Islander*, lakini kwa bahati mbaya majina yao hayakuwemo katika orodha ya tume iliyoorozesha yale majina. Kwa msingi huo basi serikali imechukua hatua nyengine kwa kupitia Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Idara ya Maafa kuhakiki majina yale ambayo yalilalamikiwa kwamba wamo katika kadhia ile na hawakutiwa katika orodha ya tume. Kazi hiyo sasa imemalizika na hivi karibuni wale ambao walikuwa hawajapata fedha zao, tunawahakikishi kwamba watapata fedha zao na kila mmoja atapata haki yake kama mpango wa serikali ulivyofanya, ili kuepusha matatizo hayo. Hili jambo limemalizika na huo ubani utagaiwa kutokana na taratibu kama walivyopata wenzao, basi na wao watapata katika mwezi huu huu mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kulikuwa na hoja inayohusu idadi ya watu katika meli ile ya MV Skagit. Je, ni ile 320 iliyosomwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam au ni 290 iliyotolewa

taarifa Zanzibar. Sisi kwa upande wetu tunafuata karatasi ya orodha ya abiria iliyowasilishwa na mmiliki wa meli. Karatasi hiyo ya orodha wa abiria inasema 290, kwa hiyo sisi tunasimamia hoja ya 290. Lakini Tume iliyoundwa ya uchunguzi ndio itatuthibitishia jambo hili kutupa uhakika kwamba walikuwa 290 ama 320. Kwa sasa hatuwezi kulisemea sana isipokuwa sisi kwa mujibu wa taratibu zetu za kisheria tunafuata karatasi hiyo ya orodha wa abiria ambayo wenye meli wameikabidhi kwa taasisi zetu husika za *ZMA* na *SUMATRA*. Kwa msingi huo sisi tunaendelea kusimama kwamba idadi ya watu waliokuwemo mule ni watu 290. Lakini tume ndio itatupa mwanga zaidi kuwa ni idadi gani walikuwemo ndani ya meli ile.

Kuhusu kutekelezwa kwa ripoti ya *MV Spice Islander*. Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, mapendekezo ya tume yalikuwa ni ya aina tatu. Yalikuwa ni ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Mapendekezo yale kama nilivyosema mwanzo, kuna mengine yanayohusu rasilimali fedha na rasilimali watu kwa maana ya utaalamu. Kwa hivyo, kuna suala hapa la kuwa na uwezo wa kutosha katika kuyatimiza yale mapendekezo. Lakini vile vile kuna suala la kusomesha wataalamu wetu ili waweze kufikia viwango vinavyohitajika ili waweze kutoa huduma. Lakini kwa yale ambayo yalikuwa ni ya muda mfupi Serikali imeyachukulia hatua. La mwanzo ni lile la kuachishwa kazi, wale wote ambao wamehusika na kadhia ile na vile vile kupelekwa katika vyombo vya kisheria, na hivi sasa kesi iko mahakamani kwa hivyo mahakama itaamua.

Mhe. Naibu Spika, hatua nyengine ni kuchukua hatua za kufanya mapitio ya sheria za usafiri wa baharini, ili tuwe na sheria bora zaidi itakayodhibiti hali yanapotokea matatizo. Vile vile tuliwataka *ZMA* kwa maana *Zanzibar Marine Authority* na *SUMATRA* wakae pamoja wafanye shughuli zao kwa pamoja ili kuepuka matatizo yanayojitokeza.

Pia Mhe. Naibu Spika, tulipiga marufuku uuzwaji holela wa tiketi na tiketi zinatakiwa ziuzwe kwenye ofisi husika tu. Kwa hivyo, napenda nitowe wito kwa Jeshi la Polisi kwa wale wote wanaouza tiketi za mikononi basi wakamatwe mara moja na wafikishwe kwenye vyombo vya sheria. Suala hili tutalisimamia zaidi kwa sababu imekuwa ni mtindo wa sasa kwa baadhi ya watu kuuza tiketi nje ya vituo halali. Kwa hivyo, Jeshi la Polisi muchukuwe hatua mara moja ili utekelezaji uendelee.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ukaguzi. Kwa kweli harakati za ukaguzi wa mara kwa mara zimeanza na vyombo vyengine vilishawahi kusimamishwa hapa nanyote ni mashahidi kutokana na ukaguzi huo. Kwa hivyo, utaendelea ukaguzi na tutahakikisha kwamba vile vyombo vyote ambavyo havifai itabidi visimamishwe na visiendelee na shughuli za kutoa huduma za usafiri.

Mhe. Naibu Spika, tutaendelea kuhakikisha kwamba vifaa na vyombo vya uokoaji vinapatikana hatua kwa hatua kama ambavyo ripoti ya tume ilivyotutaka. Hatua za ununuzi wa meli mpya zinaendelea. Nataka niwahakikishie kwamba zinaendelea vizuri. Kamati za shehia na wilaya zimepewa mafunzo kuhusu namna ya kukabiliana na maafa na hatua hizo zinaendelea. Lakini ni lazima niseme kwamba tatizo letu kubwa ni uwezo wa fedha katika kumudu kununua vifaa vinavyohitajika kama vile *rescue boat, helicopter*, *baj* na vyombo vya kuokolea meli, *sound scanes* na vifaa mbali mbali uokozi ambavyo ni muhimu yakiwemo magari na wataalamu wa kutosha. Lakini kadiri siku zinavyokwenda Mwenyezi Mungu atatusaidia tuweze kupata suluhu ya matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mfuko wa maafa. Hivi sasa tumeshafikia ukingoni mwa *draft* ya sheria ya mfuko wa maafa na *Inshaallah* katika Baraza lijalo tutaileta sheria ile ili mfuko wa maafa uweze kuanza kazi rasmi. Waheshimiwa Wajumbe, nataka niseme kwamba mfuko wa maafa utategemea sana hali ya uwezo wa nchi yetu, ukubwa wa uwezo wa kiuchumi ndio utakaotuwezesha kuwa na mfuko wa maafa mzuri utakaoweza kutoa huduma zinazotakiwa. Kwa sasa hakuna mfuko wa maafa, mfuko wa maafa ule mnaouona, fedha zile ndio zile zinazochangiwa na wananchi kwa kutoa misaada ya waliopatwa na maafa hayo.

Kwa hivyo, hizo sio fedha za operesheni, ni fedha za kusaidiwa wale wahusika ndio uliokuwa uwamuzi wa serikali. Sasa fedha zile zote ni kwa ajili ya wale wahusika na zilizobaki ni zile ambazo watalipwa wale ambao walikuwa hawakuonekana katika orodha ile ya tume. Kwa hivyo, ninachotaka kusema Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa sasa hakuna mfuko wa maafa, mpaka hapo sheria itakapopitishwa ndio tutakuwa na mfuko wa maafa. Zile tumeziweka ni *account* maalum za maafa kwa wahusika wale wa ajali peke yao, hiyo ndio hali yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Zanzibar kudai fedha zake zilizokuwepo SMT. Suala hili Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleeo analishughulikia na atalifuatilia na Inshaallah kila haki ya Zanzibar itapatikana.

Kuhusu suala la *modification* ya kuongezwa meli. Suala hili litahitaji uchunguzi wa Tume iliyoundwa ili tupate uhakika ni namna gani wameiongeza meli hiyo na ikijulikana hivyo, kwa hiyo makosa hayo yatakuwa ni makubwa zaidi, kwa sababu wamefanya mambo kinyume na taratibu na hilo pengine litapelekea hata kuwa ni *criminal case.* Kwa hivyo, jambo hili litachunguzwa na tume na Tume itatoa mapendekezo yake ili tujuwe ukweli hasa ni vipi waliweza kuongeza meli hiyo.

Vile vile lilizuka suala la kwamba meli hii ni ya masafa mafupi katika kusafirisha abiria na sio kwa masafa marefu. Kwa msingi huo kuna kila dalili ya kuonesha kuwa meli ile ni ya masafa mafupi, lakini tume ndio watatoa jibu sahihi katika jambo hili, pindi watakapofanya uchunguzi na kujua ukweli wa hali halisi na hapo tutapata ukweli wa hali yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la deni la Mkoa wa Kaskazini Zanzibar. Ni kweli suala hili lililetwa hata kwenye kamati ya kukabiliana na maafa na suala hili lilitakiwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuleta vielelezo vinavyohitajika na bahati nzuri Mkuu wa Mkoa alileta vielelezo na hivi sasa uwamuziwa Wizara ya Fedha, kwa sababu sisi hatuna mfuko wa maafa, tunatumia fedha za serikali yaani kasma ya serikali. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeitaka mkoa itowe katika kasma yake ili iweze kujilipia hizo fedha zilizotumika katika shughuli hiyo. Lakini ni vizuri wakati mwengine fedha zinapotumika kwenye haya mambo ya dharura zifuate zile taratibu zinazotakiwa. Kwa sababu japokuwa ni jambo la dharura, lakini zile kumbukumbu ziwekwe vizuri. Ni kweli penye dharura panatakiwa pafanywe mambo kidharura dharura, lakini kumbukumbu zote ziwekwe vizuri ili zipatikane mapema. Unapocheleweshe kumbukumbu kufika kwa wakati ndio matatizo mengine yanacheleweshwa na hivyo kuleta tatizo.

Kwa hivyo, naomba Mkoa wa Kaskazini sasa katika kasma yao wajithibitishie kwamba vielelezo walivyonavyo ni vya halali na vinatukidhi haja na kwa msingi huo basi waweze kulipa deni linalotakiwa.

Vile vile kuna suala limejitokeza kwamba meli nyingi hizi zinazozama zinaanzia Dar es Salaam. Je, SMZ imefanya utafiti ni kwa nini meli zinazotokea Dar es Salaam ndio hizo ambazo zinasababisha ajali. Ukweli serikali haijafanya utafiti, lakini ushauri huu ni mzuri na kwa msingi huu basi tume hii itabidi tuipelekee taarifa hii ili jambo hili nalo waweze kulichunguza ili tuweze kupata uhakika ni kwa nini hizo meli zinazoanzia Dar es Salaam ndio zinazotokea ajali. Kwa hivyo, suala hilo tutaiwachia tume husika ifanye uchunguzi huo na baadae tupate taarifa ambazo zitatusaidia kuwa ni nini chanzo chake. Lakini kwa mara hii jambo lililotokea ni kubwa, wataalamu wanatuambia ulikuwepo pale upepo mkali na mawimbi makubwa, ndio kilichokuwa chanzo cha kusababisha meli ile kuanguka, lakini yako mambo mengine ambayo ni muhimu kuyajua. Kwa hivyo, tume wao watatuletea taarifa hizo ili tujiridhishe, na hatua zichukuliwe kwa wale watakaoonekana kuwa wamefanya makosa ama taasisi iliyofanya kosa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *Sea* w*orthiness* ya meli ile, ukweli tume hii ya kuchunguza ndio itatupa uhakika wa mambo hayo, ili tuweze kujua ni kweli meli hizi zilikuwa zina uwezo na zimetimiza vigezo vya kuchukua abiria na kweli kwa muundo wake na asili yake vimeruhusiwa kufanya shughuli za kupakia abiria na mizigo. Kwa hivyo, jambo hili sasa litachunguzwa na tume kwa kiasi kikubwa halafu itatuletea taarifa.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwahakikshie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba taarifa za tume zitaletwa katika Baraza lenu tukufu, ili mujuwe kila kilichotokea na kila muhusika wa jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuweka uzio katika eneo la makaburi ya Kama. Waheshimiwa Wajumbe, ilikuwa ndio nia ya serikali kuweka uzio katika maeneo ya makaburi ya Kama na huo ndio uwamuzi wetu, kwa sababu makaburi yale kwa sasa kwa njia moja ama nyengine yanahistoria kubwa na itabidi yatunzwe pale na yaonekane kwa sababu ni jambo la kuwakumbuka ndugu zetu waliopata maafa makubwa, wakatangulia mbele ya haki. Kwa hivyo, hilo ni jambo zuri na ushauri wa kuweka alama maalum katika eneo lile tunaupokea na tutaufanyia kazi.

Kuhusu *diver's* binafsi kuwa hawatambuliwi. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana hawa *divers* binafsi, wamefanyakazi kubwa, nzuri na wameshirikiana vizuri sana na serikali na wamesaidia sana. Ni vijana wazuri, wastahamilivu na wenye moyo wa uzalendo wa kupenda nchi yao na watu wake, wamefanyakazi nzuri sana. Sasa tutaweka utaratibu rasmi wa kuwatambua hawa waokoaji binafsi, kwa sababu waokoaji binafsi hawa wametusaidia sana. Wao na wavuvi wa jirani na wananchi wengine wameshiriki vizuri katika kuhakikisha kwamba wanafanyakazi hii vizuri na wamejitolea vizuri sana.

Vile vile kulikuwa kuna ushauri kwamba fedha zilizouziwa meli ya MV Mapinduzi, ziongezee katika ununuzi wa meli. Fedha zile zipo japokuwa ni kidogo, basi katika harakati zetu za ununuzi wa meli zitasaidia, kwa sababu nia yetu ni kununua meli mpya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuwepo kwa chombo cha *DNA*. Hivi sasa madaktari wetu wanatumia chombo cha *DNA* kwa kila maiti inayookolewa inachukuliwa *DNA* na kila maiti inapewa nambari yake na kaburi lake lina nambari yake, ili kuhakikisha kwamba itakapotokea mtu kuhitaji maiti yake yeyote yule inaweza kufukuliwa na akamchukua mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, pia serikali ina mpango wa kupanua *mortuary* yake. Suala hili lilishazungumzwa sana na Mhe. Waziri wa Afya. Lakini napenda na mimi nilirudie kwamba serikali mpango huo tunao wa kupanua *mortuary* yake ili tuweze kuhifadhi maiti pale ambapo panatokea ajali za namna hiyo. Lakini yote hayo niseme kwamba ukweli ni ule ule unabaki pale pale wa tatizo la uwezo wa fedha ndio tatizo gumu zaidi.

Kuhusu mpangowa kuweka alama katika eneo lililotokezea ajali. Huo ndio utaratibu unaotumika na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama hasa vikosi vya uokoaji, vikiwemo KMKM na Watu wa Zimamoto, kuweka alama maalum kwa ajili ya kujua lile eneo ambalo limetokea ajali ili kila mara waweze kufika katika maeneo yale. Lakini kwa sababu ya *current* ya maji chombo hakiwezi kukaa pale pale, kinaburuzwa na kupelekwa sehemu nyengine, ndio maana mpaka hivi leo chombo hakijapatikana na ndio maana hata miili mingine inakwenda kuokotewa Bagamoyo, kwa sababu ya *current* ya maji inavyosukuma. Kwa hivyo, hata ukiweka alama, bado huna ushahidi kwamba kile chombo kipo pale. Wazamiaji wetu walikwenda pale na walijitahidi kwenda zaidi ya mita 30 na bado hawakuweza kukiona kile chombo. Kwa hivyo, ukweli ni kwamba utaratibu huu unatumika, lakini *current* ile inapokuwa kubwa kunakuwa na tatizo sana la kuweza kuelewa kwamba chombo hiki kiko wapi, maana kinaburuzwa na maji.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ripoti ya Tume kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Kama nilivyosema Mhe. Naibu Spika, nitahakikisha kwamba ripoti ya Tume itawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Kuhusu Bima ya Meli. Mhe. Naibu Spika, tume hii ya uchunguzi itatuhakikishia bima ile iliyokatwa inalingana na inavyotakiwa, yaani idadi ya watu, idadi ya mizigo pia na ile thamani yenyewe ya meli na kadhalika. Kwa hivyo, tume hii itakuja kutuhakikishia na kwa mujibu wa sheria zetu kama hukukata Bima inayostahili, basi mwenye chombo ndiye anayepaswa kulipa ile fidia ya Bima kwa wale wanaopata ajali. Kwa hivyo, kama hakukuwa na Bima inayostahiki, ina maana mwenye chombo atakuwa na dhamana ya kulipa Bima kwa wale wanaopata ajali.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mpango wa kuwa na kifaa maalum cha kusaidia kupata taarifa baharini. Ushauri huo nimeupokea ni jambo zuri na tumeanza kuulizia ulizia, kumbe wenyewe wataalamu wana nia ya kutaka kuwepo kwa kifaa hiki ambacho serikali inashughulikia, ili tuwe na hicho chombo ambacho kitaweza kusaidia kupata taarifa mbali mbali za baharini ili inapotekezea tatizo tuweze kulishughulikia kwa vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuingia melini na watu kuvaa *life jacket*. Suala hili itabidi tupate ushauri wa kitaalamu, kwa sababu kabla ya kutokea ajali kumwambia mtu vaa *life jacket* kidogo kuna mtihani. Kwa hivyo, itabidi tupate ushauri wa kitaalamu kama kweli utaratibu unaruhusu kufanya hivyo, au hizo *life jacket* zinaruhusiwa tu pale ambapo inatokea ajali. Lakini ushauri tunaupokea na tutawapelekea wahusika wazidi kuufanyia kazi.

Vile vile lilitokezea jambo kwamba SMZ imezuwia mkopo kwa Shirika la Meli kukopa kwa ajili ya ununuzi wa meli. SMZ hata siku moja hatuwezi kuzuwia mkono. Hivi sasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeamriwa na Baraza la Mapinduzi, kutafuta mkopo wa kununulia meli kwa hali yoyote na huku Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakishirikiana nao ili kutafutwa namna na njia ya kununua meli. Labda ikiwa kuna utaratibu uliosimamishwa, ina maana haukufuatwa utaratibu, shirika lenyewe litakuwa halikufuata taratibu. Lakini kama shirika limefuata taratibu zinazotakiwa, basi wapeleke kwa wizara husika nia ni kwamba SMZ imetoa ruhusa kabisa kwamba zitafutwe fedha za mkopo kwa ajili ya ununuzi wa meli na SMZ yenyewe inafanya jitihada zaidi sasa ili kuhakikisha kwamba ununuzi wa meli mpya unapatikana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu nahodha wa meli ya *MV. Spice Islander* mbona hajaonekana. Ni kweli kwa taarifa tulizonazo sisi mpaka leo hajaonekana na taarifa tulizonazo ni kwamba nahodha huyu amefariki, hakujaja taarifa nyengine za kuonesha kuwa nahodha huyu yuko hai.

Kuhusu nahodha wa MV. Skagit kuwa anavyo vyeti sahihi. Tume ile pia itatubainishia na ikionekana hana vyeti sahihi basi taratibu za kisheria zitachukua mkondo wake.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho lilikuwa ni kuhusu nchi ngapi zimetoa salamu za rambi rambi, ambapo suala hili limeulizwa na aliyekuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Ni nchi nyingi ambazo zimetoa salamu za rambi rambi kutokana na ajali iliyotokea na watu wengi wamehuzunishwa na jambo hili sana na wamesikitishwa sana.

Mhe. Naibu Spika, naamini na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie mambo kama haya yasitokee tena, lakini ajali na majanga hakuna mtu anayeweza kuyazuia yasitokee isipokuwa Mola mwenyewe. Kwa hivyo, kwetu sisi ni kumuomba Mwenyezi Mungu jambo kama hili atuepushie na lisitokee katika nchi yetu; na hilo ndio jambo kubwa kabisa la kulifanya.

Vile vile nataka nimpongeze sana Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa maelezo yake ya jana ya kuonesha nia yake nzuri kwa nchi hii, pia imani yake kwa watu wa nchi hii na maelezo aliyoyatoa jana tunamshukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa kutoa pole kwa wafiwa wetu pamoja na waliopatwa na ajali ile, kwa sababu ni jambo ambalo ni gumu sana na tunawatakia wale wote waliopata magonjwa ya hapa na pale waweze kupoa haraka; na wale waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, Amin.

Lakini napenda nirudie kusema kwamba jamani kazi hii ni ngumu, ambayo inahitaji moyo, uvumulivu, maana na wewe unayekwenda kuokoa unajitolea maisha yako na wala si kazi nyepesi. Kwa hiyo, hatua na juhudi zinazochukuliwa na vijana wetu hapa hatuna budi kuzipongeza, tena tuzipongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, watendaji hawa wanafanyakazi mpaka saa 8 za usiku, pale Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ukienda saa 8 mpaka 9 za usiku wapo wanafanya kazi, kama vile watu wa Idara ya Maafa pamoja na watendaji wengine wanashirikiana kufanya shughuli hizi. Kwa mfano,

Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi kubwa sana, pia Vikosi vyetu vya SMZ vinafanya kazi kubwa sana.

Kwa hivyo, lazima tufike mahala na uwezo wetu tulionao ni mdogo sana, basi ni vyema tufike pahala angalau tuwapongeze pamoja na kuwaunga mkono na wala tusiwalaumu tu kwa jambo ambalo wanafanya kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana tuwaunge mkono na tuwape moyo, ili kadri inapotokea hali kama hii waweze kutusaidia zaidi.

Kwa kweli jambo hili la majanga ni kubwa, ambalo ni la kushirikiana tena lenye kuhitaji umoja na wala si jambo la kulaumiana, maana linatokea nje ya uwezo wetu na lazima tufike mahala tujue hilo na tushirikiane pamoja, ili tulinde nchi yetu pamoja na wananchi wetu na tuweze kufanya wajibu wetu vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, ningependa sana nimalizie kwa kuwashukuru Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama, Vikosi vyetu vya SMZ, pia shukurani maalum ziende kwa vikundi binafsi ambavyo vilijitokeza kufanya kazi nzuri ya kusaidiana na vikosi vyetu na vikundi hivyo ni hivi vifuatavyo:-

1. Kikundi cha *Easy Blue Divers* cha Jambiani kilifanyakazi kubwa tena nzuri. *(Makofi)*
2. Jumuia ya Wavuvi wa Kojani, hawa wamefanya kazi kubwa sana na wametusaidia sana, Mhe. Mwakilishi hongera sana. *(Makofi)*
3. Vijana wa *Island Marine Service* ya Malindi wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*
4. *Scout* wetu wamefanya kazi kubwa sana, vijana hawa ni hodari wamefanya kazi nzuri.
5. Vijana wa *Red Cross* wamefanya kazi vizuri.
6. Pamoja na wananchi wote wa jirani wa eneo lile, kama vile wavuvi wetu na kila aliyeshiriki katika jambo lile tunawashukuru na kuwapongeza sana kwa kutusaidia; na ninaomba tuendelee kusaidiana, ili yanapotokea majanga kama haya tuweze kunusuru maisha ya watu wetu.

Lakini lazima tukumbuke kwamba sasa Zanzibar inahitaji kujijenga kiuchumi, ili tuwe na uwezo wa kuweza kuhudumia mambo muhimu. Tatizo letu kubwa ni uwezo wa fedha, ambao unarudisha nyuma kufanya wajibu wetu vizuri.

Kwa hivyo, jambo la msingi wazanzibari wenzangu nawaomba tushirikiane, tuache tofauti zetu ndogo ndogo na tuhakikishe tunajenga umoja wetu, upendo na ushirikiano, ili tujenge uchumi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Baada ya hayo, Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri, ahsante tunakushukuru. Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu utaratibu.

## UTARATIBU

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa ajili ya kutoa maelezo machache. Kwa kweli kwanza tunamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu

yake, ambayo yameturidhisha. Lakini mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuna jambo moja ambalo nataka maelezo ya ziada.

Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi alieleza kuhusu *concern* ya zile fedha ambazo wananchi walizochangia kupitia Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuitaka Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini kutumia kasma yake, kwa ajili ya kulipa hizi shilingi milioni 25, 000, 000/=.

Mhe. Naibu Spika, ninavyojua mimi ni kwamba fedha za maafa tunazitoa katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na leo tumeshapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambapo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iko chini ya wizara yake na mimi ndiye Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, leo kutoa kasma ya shilingi milioni 25,000,000/= katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, mimi nadhani ni kuiumiza na kuirejesha nyuma Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini kutotelekeza yale malengo ambayo tuliyoyapitisha hapa Barazani. *(Makofi)*

Sasa bado ninaomba na ndio maana tukawa tunaendelea kusisitiza, kwamba serikali iharakishe kuanzisha huu Mfuko wa Maafa, ili inapotokezea zile fedha ziwepo. Vile vile tulikubali katika ile sheria tuliyopitisha kwamba iendelee kutumika kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, basi namuomba Mhe. Waziri awasiliane na Mhe. Waziri wa Fedha, kwamba fedha hizi bado zitoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama hivi sasa zinatoka kupitia maafa.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa naomba tu, kwamba wenzetu kule Mkoa wa Kaskazini *Private Sector* walijitahidi sana; na hasa ile Taasisi inayoshughulikia Masuala ya Utalii, walijitahidi kutumia wale wenye mahoteli, ambao wawekezaji kutumia boti zao. Lakini kitu ambacho wanachosikitika wanasema hata barua ya shukurani hawakupelekewa.

Kwa hivyo, hili nilikuwa naomba tu Mhe. Waziri kupitia Idara ya Maafa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wapeleke zile barua za shukurani, kwa sababu wananchi wanapojitolea wakati mwengine kwamba pale ambapo walikopwa watahitaji walipwe, lakini pale ambapo walitumia nguvu zao basi hata ile shukurani.

Kwa maana hiyo, hili la mara ya pili lilikuwa ni shauri tu, isipokuwa la mwanzo namuomba Mhe. Waziri kama ataweza kunitolea maelezo hapa au baadaye, lakini naomba bado keki ya Mkoa wa Kaskazini Unguja fedha zenyewe tulizozitenga ni kidogo hazitoshi na wala sikubaliani kwamba waendelee kumega fedha zao shilingi milioni 25,000,000/= kwa ajili ya kulipia shughuli hii ya maafa. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri, majibu ya ziada kuhusu fedha za Mkuu wa Mkoa pamoja na barua za shukurani kwa vikundi vya Kaskazini vilivyosaidia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa maelezo yake. Ni kweli utaratibu wetu wakati wa maafa, kwa sababu hatuna Mfuko wa Maafa fedha hutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na baada ya kuwaomba vielelezo, kwa sababu Mhe. Mkuu wa Mkoa aliwasilisha maombi ya fedha

hizi kwenye Kamati ya Maafa; na Kamati ilimtaka alete vielelezo, baada ya kupata vielelezo ambavyo ameviwasilisha katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

Kwa hivyo, sisi kama kawaida yetu hupeleka utaratibu huu Hazina na wao ndio ambao wametujibu kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itumie kasma yake, lakini kweli analolisema Mhe. Mjumbe. Kwa hiyo, itabidi nikae na Mhe. Waziri wa Fedha tulizungumze zaidi tupate majibu sahihi, ili tuone tatizo hili linatatuliwa. *(Makofi)*

Kwa kweli tunajua uzito au ukubwa wake, kwamba wakati wa dharura mambo yanayotokea na wala tusiwavunje moyo wale ambao wanakuwa mbele katika kujitolea kutatua matatizo haya magumu sana, wenye moyo na
nia njema. Kwa maana hiyo, tutakaa na Mhe. Waziri wa Fedha tuone utaratibu utakaotumika, ili tuhakikishe fedha hizi zinalipwa kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. *(Makofi)*

Lakini kuhusu barua za shukurani namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kutukumbisha hili na wahusika, kwa sababu hawa watu wanapaswa sana kushukuriwa na kupewa kila aina ya sifa, na hata kama kuna tunzo maalum basi watu hawa inabidi wapewe medali, kwa sababu wanafanyakazi kubwa sana. Mhe. Naibu Spika, ni kazi ya ujasiri kabisa tena naunga mkono suala hili na tutalifanyia kazi, ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri, ahsante tunakushukuru. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe Kauli ya Serikali kuhusu Tukio la Kuzama kwa Meli tarehe 18/07/2012 eneo la Chumbe imopekelewa. Ahsante sana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 – Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba tunao wachangiaji 10 na tunataka saa 6 tumuite Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho na kupitisha vifungu. Kwa hivyo, naomba mtu aende kwenye *point* na wala tusirejee mambo ambayo tayari yameshazungumzwa na wenzetu. Mchangiaji wa mwanzo tunamuita Mhe. Abdalla Moh'd Ali na baadaye afuatie Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Ali Salum Haji ajiandae.

**Mhe. Abdalla Moh'd Ali:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa leo kuwa mchangiaji wa mwanzo asubuhi hii. Mhe. Naibu Spika, jana Waheshimiwa wengi waliosimama hapa walimsifu sana Mhe. Waziri na kwa bahati alitunukiwa Medali Maalum kwa Baraza la

Afrika kwamba yeye ni Waziri Bora, mimi namtakia kila la heri katika kazi hiyo, tena nina imani katika wizara hii, basi Nishani ya Ulimwengu ataipata.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kidogo kabla ya kwenda kwenye mchango wangu niende kwenye vifungu. Kwa kweli mara nyingi tunakuwa na wasi wasi na matumizi ya fedha, kwa hiyo mimi naomba kupata maelezo tu. Kwa mfano, tukiangalia Ofisi Kuu Pemba katika gharama za umeme unakutia kifungu cha 220102 shilingi milioni 2,400,000/= na hiyo imeitwa *office electricity*.

Lakini kifungu 220408 mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 2,400,000/= na mwaka huu wameomba shilingi milioni 30 karibu na laki 4 na hii iko kwenye *Government Office Electricity Bills*. Sasa naomba maelezo hapa kwamba hizi zote mbili zinakwenda kulipiwa wapi, kwa sababu zote zimo kwenye mafungu tofauti. (*Makofi*)

Vile vile kwenye mpango wao huu nimeona kuna misaada ya wanafunzi, na misaada hii imejitokeza kwenye idara tofauti, hivyo naomba maelezo. Kwa mfano, ukiangalia Idara ya Ajira wana kama shilingi milioni 9,000,000/=, Idara ya Ushirika shilingi milioni 8 na zaidi, Idara ya Afya Kazini shilingi milioni, yaani kila idara imejitokeza kwamba kuna fungu la msaada wa wanafunzi.

Sasa hawa wanafunzi ni wanafunzi gani na misaada hii inatolewa kwa njia gain; na ninachojua hivi sasa wengi tunapewa mikopo kwa ajili ya kwenda kujisomea na hawa wanapata misaada vipi na inakuwaje hata wao wanapata misaada kama hii.

Jengine ni kuwa kuna matumizi yaliyojitokeza mwaka jana katika Idara ya Mipango kuna kama shilingi milioni 5,000,000/= walinunua vifaa vya michezo; na mwaka huu imejitokeza vile vile kwamba wanaomba tena shilingi milioni 5,000,000/= kwa ajili ya kununua vifaa vya michezo. Sasa sijui kila mwaka hii ni *trend* itaendelea kwamba wanunua vifaa vya michezo.

Mhe. Naibu Spika, ninachojua mimi ni kwamba kama ni jezi umenunua basi kwa mwaka mmoja inakuwa bado inafanya kazi, na kama ni kiatu basi pia kinafanya kazi. Sasa inakuwaje wao kila mwaka wanaomba shilingi milioni 5,000,000/= kwa ajili ya kununua vifaa vya michezo, wakati vifaa hivyo vya mwaka jana vinaweza kutumika.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, mara nyingi hivi sasa nchi zilizoendelea au hata zinazoendelea huwa wanatoa *records*, kwamba sisi mwaka huu upungufu wa ajira umekuwa katika kiwango fulani na asilimia fulani. Hali hii inakuwa inasaidia katika kuona jinsi gani vijana wanavyokosa ajira.

Sasa sijui katika nchi yetu hivi sasa tunacho kipimo kama hicho na tunaweka *records* kama hizo, kwamba labda *unemployment* kwa mwezi wa *March* ilikuwa katika kiwango Fulani, na labda kiwango hicho kinatibika kwa njia fulani, kabla ya kufikia kuna kwamba ajira haipo sisi tunacho kigezo chochote kile ambacho kinatuonesha au kujua kupima kwamba ajira zimepungua au zimeongezeka.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende katika Idara ya Ajira. Kwa kweli tume-*delegate power* au tumetoa ruhusa kwa baadhi ya kampuni kuwa ni mawakala wa kutafuta ajira, nafikiri hili ni jambo zuri. Lakini mimi napenda kusema kwamba serikali nayo isingeliachia moja kwa moja suala hili, kwa sababu hizi kampuni mara nyingi huwa zinataka faida katika shughuli zao hizo wanazoziendeleza.

Kwa hiyo, ninachokijua mimi ni kwamba miaka mitatu iliyopita nyuma tuliandaa vijana katika njia tofauti na vijana hawa wakabahatika nchini Saudi Arabia kwa ajili ya kufanya kazi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwamba wao walipitia uwakala ni kuwa walichokuwa wakikipata kule ni *just hand to mouth*, yaani ile kula yao tu, kwa sababu faida kubwa ilikwenda kwa hawa mawakala na wale vijana walipata kidogo tu kwa ajili ya kujikimu; hata wazee wao wakashindwa kuwahudumia majumbani kwao. Matokeo yake vijana hawa ikabidi warudi huku nchini kwao, kwa sababu walishindwa kuendelea na kazi ile.

Mhe. Naibu Spika, ni suala zuri kwamba tunawapatia uwakala baadhi ya kampuni kwa ajili ya kuwatafutia ajira wananchi, vile vile serikali nayo isiondoe mkono wake moja kwa moja, kwa sababu hizi kampuni mara nyingi zinababaisha.

Katika hili naomba kuuliza tokea walipopewa uwakala huu hizi kampuni, je zimeshaanza kupeleka hao waajiriwa huko nchi za nje au wameshaanza kuwapatia wananchi wetu ajira. Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi hivi sasa wanalalamika kwamba wametoa fedha zao na kuzipeleka kwa mawakala, lakini mawakala mpaka hivi sasa wameshindwa kuwarejeshea fedha zao na wakenda kuna masharti fulani uchukue fungu fulani na jengine uliache.

Sasa katika hili ningependa serikali ikajiweka karibu sana na kampuni hizi, ili hilo lengo linalokusudiwa lipatikane, kwa sababu lengo sio kupata ajira tu, lakini je ajira ile itakusaidia nini na wala haiwezekani kijana atakuwa yupo nchi za nje na wazazi pamoja na familia yake wapo Unguja ikawa haifaidiki chochote zaidi ya yeye mwenyewe. Kwa hivyo, ninaiomba serikali hili ikaliona kwa jicho jengine na sio tuwaachie mawakala peke yao.

Mhe. Naibu Spika, pia katika hilo mwaka jana Mhe. Waziri alituambia hapa kwamba alifanya mbio nyingi sana na kufikia nchini Qatar; na kule alizungumza na wahusika wa nchi ile na kama sijasahau alisema huenda wakaja hapa Zanzibar kwa ajili ya kutiliana saini mkataba wa kuwapatia vijana wetu ajira.

Sasa je, zoezi au mbio zile zimemalizikia wapi sijui ni pale Qatar na haziendelei tena mbele au serikali imeondoa mkono wake katika suala hili basi tena, kwa sababu imewaachia mawakala. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri angetupa maelezo kwamba ile safari yake ya Qatar imezaa matunda kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu ajira za watoto. Kwa kweli mara nyingi sisi huwa tunapokea tu Maazimio kutoka Ulimwenguni, kwamba Azimio linasema Hakuna Ajira za Watoto. Sasa sijui tunaposema ajira za watoto Mhe. Waziri hapa kwetu Zanzibar tunakusudia ni ajira gani, ambazo hizi tunaziweka kwamba mtoto haruhusiki kufanya, kwa sababu sisi

mazingira yetu mtoto wa miaka 18 anakwambia nichukue na unamchukua kwa ajili ya kukusaidia kukokota nyavu pwani, ili kupata kitoweo hasa katika mwezi huu wa Ramadhani.

Lakini huyo huyo unaweza kumwambia hebu kanisaidie katika shughuli yangu fulani ndogo mtoto wako mwenyewe na Azimio la Kimataifa linasema sawa chini ya miaka 18 bado ni mtoto, sasa je katika mazingira tuliyonayo sisi, hivi serikali imeshaweka vipimo au vigezo maalum kwamba ajira hii haruhusiki kufanya mtoto na ile anaruhusika kufanya. Kwa hivyo, naomba angetupa maelezo, ili tutakapokwenda huko nje tukapata kujua ajira hii haruhusiki na nyengine anaruhusika kufanya.

Mhe. Naibu Spika, pia katika Sekta hii ya Ajira hivi sasa kuna malalamiko mengi hasa yanayotokana na ajira binafsi, kwamba wafanyakazi wengi walioko katika Sekta za Binafsi bado hawajapatiwa au hawapatiwi mikataba.

Kwa kweli ninavyojua ni kwamba waajiri wanakuwa wanafanya masuala haya kwa makusudi, kwa sababu anajua mimi nikimpa mkataba wa ajira mfanyakazi, basi itabidi yeye nimhudumie mambo mengi, lakini anamuweka katika *probation period* pengine kwa muda wa miaka miwili, akimaliza anamwambia mimi hukunifaa na kumuondosha, ili kuepusha kumpa maslahi yake mengine. Wizara hivi sasa ina zoezi la kupitia idara zote, sijui na hawa sekta binafsi wamefikia hatua gani, kwa sababu hili ni jambo muhimu sana.

Lakini katika hili naomba niulize tena kidogo, kwamba katika suala la utawala bora linakuja mpaka kwenye ajira. Kwa mfano, waajiriwa wengi hivi sasa wanapotafuta ajira wanakuwa wanadhalilishwa kijinsia, sijui Mhe. Waziri analifahamu hilo hasa katika Sekta Binafsi, kwa sababu katika Sekta ya Serikali hivi sasa kuna utaratibu maalum wa kutangaza, kwamba ajira zote lazima zitangaziwe.

Je, katika Sekta ya Binafsi shughuli kama hiyo iko katika mfumo kama huo au mpaka hivi sasa bado wameachiwa tu moja kwa moja wanafanya wao wanavyotaka.
Mhe. Naibu Spika, nafikiri nimalizie hapo, ili niwape wenzangu nafasi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadaye afuatie Mhe. Ali Salum Haji, tujali muda.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwenye ajira. Kwa kweli ajira hivi sasa zimekuwa nyingi sana na wizara bado inapambana na ajira za watoto, lakini bado ajira za watoto zimekuwa nyingi sana, yaani watoto wanaojiajiri wamekuwa ni wengi.

Kutokana na umasikini hii inachangia kwa watoto wetu kujiajiri katika kazi ambazo haziwahusu. Kwa mfano, hivi sasa Mhe. Naibu Spika, kuna watoto ambao wanazurura ovyo na kuuza bidhaa kama vile njugu, kubanja kokoto na hizi zote ni ajira ambazo watoto wamejiajiri na hali hii yote ni kutokana na umasikini wa familia zao, kwa sababu laiti kama si hivi Mhe. Naibu Spika, basi

nadhani watoto wengi wangekuwa wanashiriki maskuli na kufuata elimu yao na kuweza kujijua wapi wanakwenda.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hili wapo vijana wetu ambao wanamaliza masomo hukaa mitaani kwenye vigenge kama vile vya kuvuta bangi, sigara, wizi. Hali hii yote ni kutokana kwamba watoto wetu hawana kazi ya kufanya, na hili ni tatizo kubwa sana kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla ipange mikakati maalum ya kuanzisha viwanda hapa. Kwa mfano, viwanda vya uchongaji, ufugaji wa kuku, ili watoto wetu waepukane na hii kadhia ya kuzurura ovyo mitaani. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije kwenye Idara ya Mikopo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hana budi kukubaliana na mimi kwamba vipo Vikundi vingi vya Ushirika hufa au hushindwa kuendelea mbele kutokana na kukosa msukumo wa mikopo au misaada ya kujiendeleza. Vile vile kukosa mikopo kwa vikundi hivyo kwa mfano, nije kwenye kiambatanisho cha 5 alichosema kwamba katika Wilaya ya Chake Chake/Mkoani, hapa namuomba Mhe. Waziri aje anifahamishe, kwa sababu sijafahamu zaidi.

Mhe. Waziri anasema katika Wilaya ya Mkoani kuna vikundi 18, ambavyo vilipata mikopo na wanawake hamna, wanawake 9 na wanaume 10 jumla ni 19. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba aje anifahamishe vizuri, ili wanawake hawakupata au hapana mwanamke aliyepata, hii ni kumuinua mwanamke au vipi, kwa sababu amesema waliopata mikopo ni 18 na jumla ni 19. Sasa wanawake hawa sijaona wajasiri amali ambao wamepata mikopo au misaada hapa.

Vile vile vikundi hufa kutokana na migogoro ndani ya vikundi, kama vile kutoaminiana na ndipo vikundi hivyo hufa pamoja na kukosa elimu ya ushirika katika vikundi. Mhe. Naibu Spika, jengine ni uwekaji wa kumbukumbu za vikao pia hili ni tatizo kwa vikundi na linalosababisha hasa migogoro kwenye vikundi; hivyo ni uwekaji wa kumbukumbu kwamba hawaelewi kumbukumbu iliyowekwa au hawajui kilichotolewa ama kilichoingia ndio hii Mhe. Waziri inasababisha migogoro katika Vikundi vya Ushirika. *(Makofi)*

Hata hivyo, Mhe. Waziri bado katika wilaya yangu vipo vikundi ambavyo vina mwelekeo mzuri tu wa kujiendeleza. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri afanye ziara kuviona vikundi hivyo, ili ajue matatizo yao na kuweza kuwasaidia, kwa ajili ya kuwawezesha katika vikundi vyao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika ukurasa wa 28 kwenye Idara ya Uendeshaji na Utaratibu wa *Programs* za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika, naipongeza idara hii kwa kufanya kazi zake vizuri na kupanga *programs* kama hizi.

Lakini pamoja na *programs* hizi Mhe. Naibu Spika, naiomba idara kuandaa mikutano katika vijiji, ambapo wajasiriamali wengi wanatoka vijijini, ili kupata nasaha za wale ambao wameacha kujiunga na wale wenye migogoro katika vikundi; kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi wale kwa lengo la kujiunga na kuweza kujikusanya pamoja na kujenga umoja wao, ili waweze kuendelea na miradi yao.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 24 naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 24 unaeleza hivi:-

> "Ili kuimarisha masuala ya afya na usalama kazini, wizara imesimamia zoezi la kupima koo, pua, masikio, sukari, uzito na sindikizo la damu kwa wafanyakazi wake"...

Mhe. Naibu Spika, hapa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, je ni wafanyakazi wangapi ambao wamebainika na matatizo hayo na baada ya zoezi hilo kufanyika.

Sasa niende kwenye suala la wakulima wa mwani. Mhe. Naibu Spika, wakulima wa mwani hivi sasa imekuwa ni ajira kubwa sana kwa wananchi wetu, yaani kuliko kitu chochote hivi sasa. Kwa mfano, wananchi wameacha kilimo cha mihogo, mpunga kwa ajili ya kujiajiri kwenye kilimo cha mwani, ili kupata fedha na kukidhi mahitaji yao. *(Makofi)*

Lakini wananchi hawa Mhe. Waziri wanahitaji kuwezeshwa kwa kuwapatia vifaa, kama vile kamba, tai tai na elimu ya upandaji wa mwani. Vile vile kuwaongezea bei ya zao la mwani, kwa sababu bei ndogo kulinganisha na bei ya kamba za mwani. Kwa mfano, kamba ya mwani donge moja Mhe. Waziri ni shilingi 2,500/= au 3,000/= mpaka 5,000/= na wala hailingani kabisa na bei ya mwani ambayo ni shilingi 400/= au 600/= Mhe. Waziri naomba na hili ulione. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba uwawezeshe wakulima wa mwani, ili waweze kujikimu kimaisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia kutokana na bei ya mwani wa mvinje ni ndogo. Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri namuomba awatafutie wananchi hawa Mwani wa *Cottonii* ambao una bei kuliko Mwani wa Mvinje. Kwa mfano, tukiangalia katika Shehia yangu ya Kangani, Chokocho, Mkanyageni pamoja na Kisiwa Panza Mhe. Waziri Mwani huu wa Cottonii hamna, ambapo wakulima wengi wa mwani wanatoka katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba hili uliangalie, ili wananchi wapate bei nzuri ya mwani, kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kuwatafutia soko wananchi hawa, ili waweze kuuza bidhaa zao kwa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ahsante kwa kutumia muda vizuri. Sasa nafasi tunampa Mhe. Ali Salum Haji na baadaye Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Bikame Yussuf Hamad ajitayarishe.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya asubuhi ya leo. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, huu msemo mmoja mkubwa sana. Kwa kweli haki yake Mhe. Haroun Ali Suleiman lazima tumpe kwamba ni Mhe. Waziri ambaye ni msikivu, mfuatiliaji tena ni muadilifu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu jana wakati alipokuwa akichangia alisema kwamba alimshikia chaki na mimi ni miongoni mwa aliowashikia chaki kutoka mwaka 1983 mpaka 1985 pale Skuli ya Haile-Selassie; na mimi ni mmoja wapo. Kwa kweli tunamfahamu vya kutosho jinsi ya usimamizi wake katika utendaji wake wa kazi. Mwenyezi Mungu *Inshaallah* amjaalie, basi zile jitihada aendelee nazo katika Wizara yake ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninayo mambo matatu. Jambo la kwanza liko katika ukurasa wa 56 kuhusu suala la ajira. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tumekuwa tunapiga kelele sana; na imekuwa ni nyimbo za kawaida kila siku kwamba vijana wetu hawana ajira na serikali inafika pahala inakiri kweli haina uwezo wa kuajiri watu wote na ndio maana kila siku tunakuwa tunaambiwa kwa mwaka huu tumeandaa ajira fulani.

Sasa mimi nahisi kwamba muda umefika hivi sasa suala hili tukalifanyia kazi vya kutosha na isiwe maneno ya kila siku, kwamba tunapiga kelele kila siku kuwa vijana hawana ajira. Mhe. Naibu Spika, tumepata bahati nzuri sana katika suala la ajira kwenye Sekta Binafsi kuhusiana na masuala ya utalii, nafasi ni nyingi sana.

Lakini nafikiri bado serikali haijaandaa mikakati ya kuweka sheria maalum kwa vijana wetu. Hivi sasa imefika wakati kwamba tuwe na sheria maalum katika masuala ya Sekta Binafsi na hususan katika maeneo ya utalii kwa wale wenzetu ambao wanawekeza.

Kwa kweli kuna maeneo ukiyatizama *totally* hayastahiki kuwapa wageni. Kwa mfano, eneo la bustani Msimamizi Mkuu anakuwa mgeni tutegemee nini, sasa unapompa msimamizi mkuu kuwa ni mgeni, basi na wale wanaofuatia wa chini hatawachukua Wazanzibari na atawachukua ndugu zake na kuja kusimamia zile nafasi. Vile vile tumegundua sehemu mbali mbali kama vile Mapokezi unamkuta Mkenya ndio Mkuu wa Mapokezi, ukienda kwenye bustani unamkuta Mkuu wa Bustani ni Mganda.

Kutokana na hali hiyo, nadhani tuwe na sheria kwa hawa wawekezaji wetu kwamba katika maeneo ambayo yanawezekana kufanywa kazi na Wazanzibari, basi masuala haya lazima yasimamiwe na Wazanzibari, vyenginevyo tutakuwa tunapiga kelele vile vile.

Mhe. Naibu Spika, hakuna eneo ambalo tumewabana hawa watu na kama lipo, basi Mhe. Waziri wakati atakapokuja atatueleza, kama kuna fursa ya kuwabana wawekezaji, ili kuajiri wazanzibari katika yale maeneo husika, ambayo tunahisi Wazanzibari wenyewe wanaweza kumudu kuzifanya, vyenginevyo itakuwa vile vile kila siku itakuwa nenda rudi, vijana wetu kazi hawana wanakaa vijiweni na kupiga soga ambayo hayaeleweki pamoja na kufanya vitendo ambavyo havistahiki.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri suala hili alisimamie na aliangalie vya kutosha, kwa sababu ni suala ambalo wenzangu wengi wameshalipigia kelele na mimi naendelea kulipigia kelele, kwa sababu na mimi ni miongoni mwa kijana mwenzao.

Mhe. Naibu Spika, eneo la pili naomba niende kwenye ukurasa 28 kuhusu suala la uwezeshaji. Kwa bahati nzuri Mawaziri wetu wamekuwa wanatembea sana. Kwa maana hiyo, mimi nataka

niiombe serikali kama kuna haja ya watu kutembezwa nje basi Mwalimu Haroun Ali Suleiman Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchimu na Ushirika tumpe *priority*, kwa sababu serikali inakiri haina uwezo na tutampa mzigo mkubwa, ili uwezo uongezeke lazima uende ukaombe misaada nje ya nchi.

Sasa ni vyema na yeye akatembelea zaidi, kwa sababu kuna baadhi ya nchi za wenzetu katika kuondosha ajira kwa Sekta Binafsi kuna mikakati maalum ambayo wameiweka, na bila ya mikakati hii na sisi hatutafika pahala tukapiga hatua kabla ya hii mikakati haikuweza kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuweza kuondosha matatizo haya, basi ni lazima tuanzishe Benki za Kisekta, mimi naamini tukiwa na Benki za Kisekta serikali yetu itapiga hatua. Kwa mfano, tuwe na Benki za Vijana, Benki za Wanawake pamoja na Benki za Viwanda, hali hii itawapa wepesi watu wetu kuweza kwenda kukopa fedha katika yale maeneo, ili kuweza kujikwamua na ile hali ya umasikini iliyowakumba.

Jambo la kumalizia Mhe. Naibu Spika, katika kitabu cha Mhe. Waziri naomba nichangie ukurasa wa 35 katika eneo la mikopo. Ni kweli serikali inajitahidi mikopo, lakini kinachoonekana kwamba pamoja na jitihada na uwezo mdogo wa serikali, lakini suala la urejeshaji umekuwa ni mdogo, Mhe. Naibu Spika, hapa kuna mapungufu.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri waandae utaratibu kabla ya kutoa mikopo basi kuwe na haja au fursa maalum ya kutoa taaluma kwa wale watu ambao wanakopeshwa, kwa sababu hili tumelikuta katika baadhi ya maeneo mbali mbali wakati Kamati yetu ilipotembelea Mhe. Naibu Spika. Kwa mfano, mtu anakopeshwa fedha na kuanzisha mradi wa kuku, lakini hana taaluma ya ufugaji na matokeo yake anapopata zile fedha na kuanzisha ule mradi, basi unakuta mradi ule hauwi endelevu na kuku wanafariki.

Wakati huo na yeye huyu mtu tayari ameshachukua fedha za serikali na inamtaka arejeshe zile fedha na wala hana nia mbaya ya kukataa kurejesha zile fedha. Kwa kweli anashindwa kurejesha zile fedha, kwa sababu ule mradi aliouanzisha hakuwa na taaluma kabla ya kuanzisha ule mradi.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aangalie suala zima la kutoa taaluma kwa wale watu ambao tayari wameshakubaliwa kupewa ile mikopo kabla ya kukabidhiwa ile mikopo, ili kuweza kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu, vyenginevyo tutafika pahala tutakuja kuwafunga wananchi wetu bure, baada ya kuchukua mikopo na kushindwa kurejesha mikopo hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuchangia kitabu hichi cha Mhe. Waziri naomba nirudi kwenye kitabu kikubwa cha bajeti naomba nipate ufafanuzi kidogo kuna vifungu ambavyo vimenipa utata. Kwa mfano, kifungu 0701 Idara ya Usalama wa Afya Kazini kifungu kidogo 21116 Vikao vya Kamati. Kwa kweli fungu hili limepanda kwa nguvu sana Mhe. Naibu Spika, mwaka jana waliomba shilingi milioni 2,130,000/= lakini mwaka huu wameomba shilingi milioni 11,710,000/=.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nende katika fungu 0601 Idara ya Ajira, fungu dogo 220200 Viburudishaji mwaka jana *Nil* mwaka huu milioni kumi na moja, laki tano tisini na tano elfu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika fungu 0901 Idara ya Uendeshaji na Uratibu, fungu dogo 21116 Posho Vikao vya Kamati, mwaka jana waliomba milioni sita laki tatu, mwaka huu wameomba milioni ishirini na sita laki tatu na rubaini.

Mheshimiwa maongezeko yamekuwa ni makubwa kama tulivyosema mwanzo, kwamba kuna haja ya Kamati zinazohusika mafungu haya yakishakupitishwa basi kuangalia yanafanya kazi kwa vile yalivyoombwa. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, niseme tu kama wengi waliotangulia kwamba Maalim Haroun hatuna tatizo nae sio kwa rangi yake hatuna tatizo nae kwa uwadilifu na usimamizi na katika kufanya kazi zake kwa ushupavu kabisa.

Niunge mkono hoja hii na nina imani wenzangu wote wataunga mkono hoja na kwa Wizara hii sitegemei kama litatokezea buti. Mheshimiwa baada ya hayo nakushukuru sana.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia machache kwa sababu wenzangu wengi waliotangulia wameshachangia basi na mimi niseme tu kidogo ili niweze kuunga mkono hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, napenda nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa juhudi kubwa ambayo wanaichukua pia na kwa hotuba yao nzuri ambayo wameileta katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kuchangia katika Idara hii ya Mikopo. Kabla sijaanza mchango wangu ningeomba nitoe wito kwa wananchi wetu ambao ndio wanaopelekewa mikopo hii. Kwanza niwaombe sana akina mama wenzangu ambao wanaofanikiwa kupata hii mikopo basi waweze kuitumia mikopo hii katika yale maombi yao ambayo wameyakusudia kuyatekeleza. Wasiitumie mikopo labda kwa kukata sare au kwa kupika chai za maharusi baadaye watakosa yale malengo ambayo wameyakusudia ya kujikwamua na umasikini.

Lakini pia nikiendelea na mchango huu naomba sana Idara hii ya mikopo nilikuwa naomba mfuko ule wa AK na JK basi uweze kuidhinishwa katika Wizara hii ipewe mamlaka ili mfuko huo uweze kusaidia kwa kuwawezesha kupata ile mikopo iwe mikubwa mikubwa kidogo. Kwa sababu nimeona, hapa hiyo Idara ambayo inatoa mikopo lakini yenyewe inajiendesha kwa ruzuku. Kwa hiyo utakapoongezewa huu mfuko ukazidi kuwa mkubwa kidogo angalau ule mkopo unaotolewa utakuwa ni wa manufaa zaidi.

Pia nikiendelea naomba niseme kwamba vikundi hivi kwa kweli vipo kwa muda mrefu au SACCOS hizi, zipo kwa muda mrefu zimeanzishwa lakini utakuta bado wimbi la umasikini linatukwaza. Mimi niseme kwanza labda kwa hatua hiyo ya mikopo kuwa midogo inakuwa haiwezi ikafanyisha mradi ambao unaweza ukaleta tija kwa wananchi.

Nimuombe Mhe. Waziri kufikiria kujipanga kuwa na miradi mikubwa ambayo itaweza kweli kutukwamua kiuchumi. Mimi niseme labda kwa kuwa kina mama wapo wenye ujuzi wengi ningefikiria Mhe. Waziri ungeanzisha viwanda vya ushoni ambapo akina mama wale wangeweza

kujikusanya pamoja wakashona nguo nzuri basi wangeweza kupata ajira kwa njia hiyo. Lakini pia wangeweza kupata soko kubwa na pengine lingeweza kuzuia zile nguo ambazo tunaagiza tungeweza pengine sisi wenyewe kuzishona hapa na tukaweza kujipatia soko sisi wenyewe.

Pia nimuombe Mhe. Waziri kuangalia katika Wizara hii ya Uvuvi pia kuna vikundi kule vinajishughilisha na ufugaji wa samaki, kaa na mambo mengine. Mhe. Waziri ungeweza kuvipatia vikundi hivi navyo vikaweza kujisaidia kwa sababu wanakuwa wana mahitaji mengi wanataka lakini uwezo wao unakuwa mdogo. Hivyo wanakuwa wanashindwa njiani.

Mhe. Waziri pia wenzangu wamesema hapa njia pekee ya kuwakomboa wananchi basi ni huku kuwashirikisha katika hivi vikundi wakaweza kupatiwa fedha. Lakini katika hili mimi nilitaka niseme kweli vikundi vipo na watu wanashiriki katika kazi mbali mbali, lakini elimu na nyinyi mnajitahidi kutoa elimu sio kama haitolewi kabisa kabisa inatolewa lakini mimi ningependa iwe endelevu ili izidi kutusaidia. Kwa sababu sisi wenyewe hapa kama viongozi tunaona kila siku tunaendelea kupewa elimu ili tuweze kukabiliana na yale majukumu yetu. Basi na wao kupatiwa elimu kila wakati hawa ingeweza kuwawezesha kuviendesha vikundi vyao.

Lakini si elimu tu mheshimiwa pamoja na ufuatiliaji, hapa ndipo vikundi vinapokwama, tukishakuwapa ile elimu inakuwa sasa kuwafuatilia huwa hatuwafuatilii tunawaacha wanaweza kujiendesha wenyewe tunahisi tumeshawapa ile elimu bila ya sisi kuwa nao karibu kuwapitia mara kwa mara ili tukaweza kuona wanaendaje katika shughuli zao.

Mimi nikuombe Mhe. Waziri kupitia Mkoa wangu unapovitembelea basi vikundi nikuombe mimi unishirikishe katika ziara zako ili niweze kuviona vile vikundi ambavyo tayari umeshavisaidia na umeshavipa mikopo ili niweze na mimi kuwa karibu nao na niwe nakupa maendeleo ambayo yanapatikana pale na wapi tunakwama. Hilo nilikuwa nataka nikuombe.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ajira. Serikali ilileta mradi huu wa utalii makusudi ili kuweza kupatia wananchi ajira. Lakini mpaka sasa kwa inavyoonekana bado ajira hizi zinachukuliwa sana na wageni na kwa kuonekana sisi labda tumekosa sifa ya kukabiliana na ajira hizo. Mimi nimuombe Mhe. Waziri kukiangalia hichi Chuo chetu cha Utalii, kweli elimu ile ambayo tunaipata pale inaweza kutosheleza wananchi wetu kukabiliana na soko hili la ajira. Isiwe pengine pale vinatolewa ngazi za vyeti wenzetu wanakuja na digrii au diploma siye tukawa tumeganda kwenye ngazi ya cheti tu, ukishakupewa cheti ndio basi ukenda kule unakuta yupo mwenye sifa zaidi. Naomba sana kukiangalia Chuo hichi ili tuweze kukabiliana na soko hili.
Mhe. Naibu Spika, niendelee Mwenzangu hapa Mhe. Mwajuma aligusia ajira hizi za watoto. Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi nimwambie Mhe. Waziri afanye ziara ya makusudi hasa katika Wilaya hizi ambazo zimekithiri kwa umasikini. Kuna Wilaya Kakasini “A” Mkoa wa Kaskazini na kuna Wilaya ya Micheweni. Hizi zinaonekana kuwa zina wimbi kubwa la umasikini na ajira za watoto ndio zinaongoza. Mheshimiwa naomba hawa uwape kipaumbele kuwaangalia ili na wao waweze kujikwamua katika masuala haya ya ajira.

Mhe. Naibu Spika, kuna siku hapa Mhe. Waziri aliwahi kutuhamasisha juu ya ajira za nje huko tuwahamasishe vijana wetu waweze kuingia katika ajira hizo. Alitwambia kuna ajira Qatar na sehemu nyenginezo. Akatuhamasisha tuwatake vijana wetu wajiorodheshe, hili mimi nataka

kumuuliza kwamba limefikia wapi na wapo vijana wanatuuliza uliza kama hizo nafasi bado zipo ili na wao tuweze kuwaorodhesha tukuletee na wao waweze kufaidika na ajira hizo.
Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nasema nashukuru sana naitakia kila la kheria bajeti hii. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na akaweza kutupa uzima tukaweza kukutana hapa tukiwa tumo ndani ya kujadili mustakabal wan chi yetu kwa ujumla.

Pia Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru na wewe kwa kunigaiya na miye nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi, Kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa jukumu kubwa walilonalo la Wizara yao kwa mpango mzima wa kuwawezesha wananchi kiuchumi. Jambo ambalo ni jukumu kubwa hasa ukizingatia katika nchi yetu ya Zanzibar na mambo yanayotukabili katika hali ya uchumi.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kupitia Wizara yake kama anavyoeleza katika kitabu chake kuwa pamoja na Wizara nyengine katika kulitekeleza hili la kuwawezesha wananchi kiuchumi na mambo mengine.

Nikianza kwanza nataka nianze kwenye utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mipango Sera na Utafiti katika *program* ya kazi nje nje. Miye hapa kwanza nawashukuru sana Shirika la Kazi Duniani kwa kutaka kuisaidia Zanzibar kwa moyo wao thabit kabisa. Hii si mara ya kwanza nadhani shirika hili limefanya kazi kubwa sana ikiwa miye ni mmoja wa miongoni mwa niliyefaidika na matunda ya Shirika hili katika kutuwezesha wanawake, watoto, katika makundi mbali mbali. Kwa hivyo napenda kulipongeza Shirika, hili kwa juhudi zao wanazozichukua katika kutuwezesha hasa katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini tatizo liliopo badala ya kuja hizi *program* au kuletewa hizi *program* au miradi ambayo kuwa pengine inaletwa na shirika kama hili, hatima yake shirika hili linapomaliza muda wake basi na ile miradi yote inasambaratika. Hakuna mradi tena unaojiendeleza wala hakuna mradi unaokuwa unajiwezesha tena. Hili pia linapelekea Serikali na wao kuchangia kwa kutofuatilia tena masuala yale. Baada ya kumaliza huu mradi muda wao basi na wao Serikali huachia mkono kwa vikundi vile au kwa makundi yale ikabidi tena wao hawafuatilii kikamilifu na kuwaachia majukumu yale peke yao.

Ningemuomba miye Mhe. Waziri baada ya *program* hizi kumalizika basi Serikali na wao wasibaki nyuma baada ya kusaidiwa na wao wajikaze ili kuendeleza makundi haya katika lile lengo ambalo limekusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika huu mradi wa kupambana na ajira za watoto. Hili ni tatizo kubwa hasa katika maeneo yetu ya vijijini na kuna Wilaya hasa zinazoongoza matatizo haya ya ajira mbaya za watoto. Lakini ajira hizi zina mambo tele ambayo yanasababisha ajira za watoto.

Wengine hawasababishi tu ajira za watoto kutokana na hali za maisha za wale wazee wao. Lakini kunatokea kusababisha pengine ajira mbaya za watoto pengine kupitia mwanamke kaachwa na mumewe, badala yake kaachiwa familiwa ya watoto ambayo inamshinda yeye kutekeleza majukumu yake na kuwashughulikia watoto wale. Hiyo inawafanya watoto wale kusambaratika na kuweza kujiingiza katika ajira mbaya za watoto.

Pia husababishwa na watu wengine pengine mtu katoka mjini huko anakwenda kutafuta mtoto kulea anakenda vijijini, anakwenda kumchukua mtoto wa mwenziwe, wake yeye anasomesha lakini yule anamuweka ndani kwa ajili ya kumtumikisha mtoto yule na anakosa haki zake za elimu. Mhe. Waziri mambo haya yapo na kuwepo kwa mambo haya yanataka kufanyiwa utafiti wa kina katika ajira hizi mbaya za watoto.

Je, watoto hawa wanasababishwa tu na familia zao kuwa masikini au wanasababisha watoto hawa kupata ajira mbaya kwa kutelekezwa pengine na wazee wao wakaachiwa watoto, pengine wanawake wanapewa talaka na kuachiwa watoto inabidi wanakuwa hawawezi kuwamudu kimaisha na husababisha ajira hizi mbaya za watoto.
Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 16. Kwanza nataka niipongeze sana Wizara katika kifungu hiki cha 20 kwa utafiti wao wanaoufanya katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuzingatia kupitia rasilimali na fursa walizonazo katika maeneo yao.

Mhe. Spika, Wizara katika utafiti huu miye nawapongeza sana na wanashukuru kwa kuliona hili. Kwa sababu matatizo mengi yanayotokezea katika vikundi vingi vinavyoanzishwa husambaratika moja ni kupewa mtu kazi ambayo kuwa hana uwezo kuifanya.

Mhe. Spika, kwa mfano wananchi wa Wilaya ya Micheweni wengi sasa hivi wanajishughulisha na zao la kupanda mwani. Hapa kama unataka umuwezeshe mwananchi huyu ili akuwe kiuchumi basi uende katika ile kazi ule uzalishaji anaoufanya. Lakini huwezi kuwa mtu huyu anapanda mwani ukenda akamwambia umpe mkopo afanye biashara, atakuwa haendelei. Mimi nashukuru Mhe. Waziri kuliona hili na ndilo litakalofanya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia zile kazi zao au ule uzalishaji wao walionao, ndio njia pekee ambayo kuwa itamfanya mwananchi aweze kukua kiuchumi wake, kama ni mkulima awezeshwe, kama ni mfanyabiashara awezeshwe, kama ni mvuvi awezeshwe, lakini kwa kwenda tu ukawataka watu waende wakaunde vikundi ambavyo kuwa hawana mpango navyo, mtu keshazowea kufanya shughuli nyengine aende akafanye nyengine. Hivyo tutakuwa hatwendi na wala tutakuwa hatufiki hatma.

Mhe. Waziri, mimi ningemuomba aende katika mpango huu, akenda Wilaya ya Micheweni kama anahitaji kuwawezesha wananchi kiuchumi basi azingatie ni kazi gani katika Wilaya hii inawezekana ikafanyika na watu wakajikwamua kwa umasikini. Lakini kwa kwenda tu kuanzisha vikundi ikabidi vikundi vile kwenda watu kuchukua mikopo wakiwapa watu wengine basi tutakuwa hatufikii lengo tunalokusudia.

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye ukurasa wa 44 hapa Mhe. Waziri kifungu cha 4 kasema kuna vyama 52 vikiwemo *SACCOS* 38 na Vyama 14 vya ushirika Unguja na Pemba vimefanyiwa ukaguzi wa mahesabu yao kwa kushirikiana na Afisi. Miye hili Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi anieleze, na sitaki niende katika hivi vyama nataka nende katika

hizi *SACCOS* ni *SACCOS* gani ambazo zimefanyiwa ukaguzi ili nijue na miye, hasa katika kisiwa cha Pemba kwa sababu na miye ni mshirika mmoja au ni mdau mmoja wa hizo SACCOS basi naomba katika hili alitolee ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kasema Mhe. Waziri hapa katika ukurasa wa 46, kuna wanawake 32 na wanaume 20 kutoka *SACCOS* 19, *SACCOS* 9 za Unguja na *SACCOS* 7 za Pemba walipatiwa mafunzo juu ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za *SACCOS* kifedha kwenye *SACCOS* zao. Mheshimiwa miye mwaka jana nilichangia bajeti hii na nikamtaka Mhe. Waziri kuna *SACCOS* moja kule Pemba nikamwambia Mhe. Waziri ina matatizo na ni miongoni mwa *SACCOS* moja ambayo ilianzishwa na hili Shirika la Kazi Duniani, katika mradi wao waliokuja kuimarisha ajira za akina mama na kupunguza ajira za watoto. Mradi huu uliletwa na Shirika la Kazi Duniani na kwa kweli ulikwenda vizuri tu. Hatima yake *SACCOS* ile imesambaratika mpaka leo hawajui wendako wala warudiko. Nikamuomba Mhe. Waziri hii *SACCOS* aifuatilie ili tujue wamefikia wapi.

Mhe. Naibu Spika, ukiwauliza hao wenye *SACCOS* wanasema hakuna kinachoendelea na hawana pa kushika na ni *SACCOS* ambayo iko chini ya Afisi ya Ustawi wa Jamii, wanawake na watoto, wanafanya shughuli zao lakini mpaka leo hii waliahidiwa wataunganishwa na Benki nyengine sijui kupatiwa mikopo. Mpaka leo hii inashindikana na karibuni wanachama wa *SACCOS* ile wasiopungua 300. Hakiba zao zimekwenda ovyo, hawapati mikopo, hawana chochote wanachopata. Kwa hiyo Mhe. Waziri aje anambie katika hizi *SACCOS* ambazo wanakwenda wakizipa mafuzo katika hizi *SACCOS* ambazo zinakwenda zikikaguliwa miongoni mwa hii Pemba *SACCOS* imo? Mhe. Waziri akija na miye anieleze ili nipate ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, naona kwa misingi hiyo itakuwa sirahisi tena mwanamke aliyetoka kwenye *SACCOS* ile na madhila aliyoyapata na kupoteza pesa zao nyingi za kimasikini hawajui wakazipatie wapi. Basi si rahisi tena kwa mwanamke yule akenda kumwambia ajiunge na *SACCOS* akakubali. Hii yote ni kukosekana kwa ufuatiliaji wa wale waliokuwa wasimamizi walikuwa wakitoka kwenye Wizara hiyo lakini wengine pia katika Vyama vya Ushirika waliokuwa wakisimamia. Baada ya kufikwa na misukosuko hiyo hapana aliyeuliza tena na imekuwa hawajui la kushika wala kuwacha. Wanachama hawa na hatimaye kutaka kugombana wao pamoja na viongozi wao. Wizara yako inajukumu pia la kufuatilia masuala kama haya na matatizo kama haya usende ukatatua migogoro ya ardhi tu lakini na hii muishughulikie.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, kuna hii Idara ya Ajira, Mheshimiwa vijana wetu saa nyengine wakiwa hawana kazi basi anaweza akenda pahali akataka ajira bila ya kukubaliana pengine mikataba, yeye akaona ende tu akapate ajira pengine mkataba utafuatia baadaye. Sasa Mheshimiwa kuna hawa vijana wetu waliokuwepo Pemba walioajiriwa na Kampuni ya *ZANTEL*, vijana hawa kwa masikitiko yao makubwa Mhe. Waziri bado hawajapata mikataba ambayo itakuwa ni mikataba ya kiuhakika.

Mhe. Naibu Spika, hivi juzi wamesema kuwa walipatiwa mkataba wa miezi sita lakini mkataba huo haujulikani miguu wala mkono. Kwa hivyo Mhe. Waziri tunakuomba kuhusu vijana hawa waliokuwepo Pemba wanaoajiriwa kama ni walinzi basi tuwafuatilie ili ujue mikataba yao inakwendaje au mikataka yao inaandikwaje.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa dhati kabisa na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Awali ya yote na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma aliyetujaalia hapa leo tukiwa wazima na kuja kutekeleza yale ambayo tumetumwa na wananchi katika Baraza hili.
Mimi moja kwa moja naanza vile vile kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake ambayo ni nzuri na kwa kweli mimi nafahamu kwamba Mhe. Waziri hotuba hii pamoja na utendaji wake wote wa kazi kwa mwaka uliopita ilikuwa kwa mashirikiano mazuri na watendaji wake. Kwa sababu watendaji wake ni watu mahiri na makini kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, mimi vile vile nachukua fursa hii kumpongeza Waziri kwa kweli naangalia hotuba yake na naiona kwamba inanitosheleza. Kwa sababu kwa bajeti nyengine ambazo zimepita, hotuba nyengine ambazo zimepita mimi zilikuwa haziniridhishi kutokana na uchambuzi wa data. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutupa data kamili, nyingi ambazo amezichambua na kutuonesha kwamba katika shughuli zake basi anajua kwamba anawafanyia makundi yote, wanawake na wanaume. Kwa kweli nampongeza sana waziri.

Vile vile nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri. Mimi mwenyewe nimeshawahi kusikia vipindi vyake vingi sana, pamoja na kuona harakati nyingi katika magazeti yetu ambayo yameeleza shughuli zake pamoja na kuwaelimisha wananchi. Kwa kweli Mhe. Waziri nakupongeza sana kwa hilo.
Mhe. Naibu Spika, mimi naanza moja kwa moja katika ukurasa wa 18 ambao unatueleza kwamba Mheshimiwa Wizara yako imejipanga kwa kuanziasha *program* maalum ya kukuza ajira kwa vijana. Mimi nafikiria kwamba hili ni wazo zuri na naamini kwamba ni wazo ambalo limepangwa lakini linaweza kutekelezeka. Na haya ambayo yemepangwa vile vile mimi nafikiria Mhe. Waziri kutokana na uwezo wako pamoja na watendaji wako yanaweza kutekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mimi nilikuwa nakuomba uwakamate vijana sana, kwa kuwatafuta kwa kila njia ili uhakikishe vijana unawasaidia. Vijana wetu wengi sana wamepotea, hawajui wapi wanakwenda. Hii ni changamoto kubwa sana ya taifa letu. Hivyo nakuomba mikakati hii na mipango hii ambayo umeiandaa mwakani naomba uje utwambie hapa ni vijana wangapi ambao tayari wamefaidika na *program* hii.

Mhe. Waziri nasema hivyo kwa sababu mara nyingi tunakuwa tunajipanga, tunatengeneza *program* nzuri lakini yale mazao tunakuwa hatuyaoni. Sasa nakuomba Mhe. Waziri huu mwaka unajitayarisha lakini katika bajeti yako ya mwakani utwambie *proragram* hii imewasaidia wangapi. Tukiendelea Mhe. Waziri katika ukurasa wa 24 mimi niseme kwamba nimefarijika sana kuna ukurasa wa 26 ambao unasema kwamba Wizara yako imeweza kusaidia vikundi mbali mbali na umetaja kikundi kimoja ambacho kinaitwa *Zanzibar Drug Free*, Mhe. Waziri mimi nakupongeza sana na nakuomba sana kwamba hawa usije ukawaacha mikono. Vijana wetu ambao wameamua kuacha kutumia dawa za kulevya, wanaacha kutumia lakini wakitoka katika maeneo yale basi vijana wale wanarudi tena kwa sababu hawana cha kufanya.

Mhe. Waziri hii uchukue kama ni kazi yako muhimu, ikusaidie utengeneze *program* maalum ya kuwasaidia vijana hawa, kwa sababu wengi wao wanasema wanarudi katika tabia ile kutokana na kuwa hawana cha kufanya.
Katika kukurasa wa 30 nimeona hapa umetaja shughuli mbali mbali ambazo mnazifanya na kutembelea katika mahoteli mbali mbali ya kitalii. Mhe. Waziri mimi nataka kukupongeza sana kwa hilo. Vile vile naamini kwamba ikiwa kama itatekelezwa vizuri naamini kwamba vijana wetu watapata kazi na hata hawa wajasiri amali basi bidhaa zao zitauzika.

Mhe. Waziri lakini kuna tatizo moja, tatizo ni kwamba hawa wawekezaji wetu wengi huwa mara nyingi hawazitaki bidhaa zetu. Hilo limejitokeza sana mara nyingi sana wanakuwa wanaagizia bidhaa kutoka nje ambazo hapa bidhaa hizo zinaweza kupatikana. Hatujui kwa nini wanafanya hivyo. Mhe. Waziri sijui na wewe utasaidia vipi kwa hawa wajasiri amali ambao unawatumia katika kuhakikisha masoko haya yatavutika na kazi zao. Masoko haya ni lazima yavutike na kazi za wajasiri amali. Bila ya hivyo tutaona kwamba bado tutakuwa tunakwenda tunazungumza lakini hakuna kinachopatikana.

Vile vile Mhe. Waziri kuna hivi vikundi vya wanawake ambao wao wanashuhulika na kutumia kuchora katika *Canvas* wengi wapo katika maeneo ya Mjimkongwe. Kina mama hawa wamekuwa wanafanya kazi nzuri sana. Mara nyingi sana kazi zao wanaziuza katika mahoteli mbali mbali hata Tanzania Bara. Lakini bado hoteli zetu zinashindwa kuwachukua akina mama hawa kuwaweka katika mahoteli yao hasa wakati wa *high season* ili kuhakikisha akina mama hawa na wao angalau basi wanapata chochote katika utalii.

Nakuomba Mhe. Waziri hakikisha kwamba katika makubaliano yako na hawa wenye hoteli hizi basi angalau katika kila *high season* hawa akina mama basi wanapata nafasi ya kuweza kuonesha maonesho yao ya shughuli zao za sanaa.
Mhe. Naibu Spika, naendelea katika ukurasa wa 33 ambao unazungumzia mpango wa kushindanisha, mipango ya biashara. Katika ukurasa huu Mheshimiwa ametwambia kwamba kuna mipango ya biashara lakini haijajieleza vizuri kwamba kuna Wazanzibari wowote ambao wameshiriki. Kwa sababu hapa tumeona kuna donge nono lakini haijajieleza kwamba kuna Wazanzibari wowote ambao wameshiriki na kati ya hawa 14 ambao wameshinda Je, kuna Mzanzibari yoyote na yeye amefanikiwa kupata donge hili nono na kama kuna mipango maalum basi Mheshimiwa atatuelezea.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ukurasa wa 41 ambao unazungumzia Idara ya Ushirika. Mheshimiwa Waziri Idara ya Ushirika, ni Idara ambayo imefanya kazi kwa kipindi kirefu sana. Naweza kusema kwamba Idara ya Ushirika wamekuwa wana kazi nyingi. Lakini vile vile wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu.

Mhe. Waziri nakuomba Wizara hii kwanza sijui mpaka leo wako katika lile lile jengo ambalo ni bovu. Lakini vile vile wana tatizo la kufuatilia kazi zao kutokana nakwamba hawana usafiri au hawana mafuta. Mara nyingi sana huwa wanataka kwenda katika maeneo mbali mbali lakini wanakosa nyenzo za kufanyia kazi.

Mhe. Waziri idara hii itizame kwa sababu idara hii ni idara ambayo inasaidia sana wajasiri amali. Kwa kweli mara nyingi ukiwaita kusaidia katika kutoa elimu ya ushirika hawa kila siku wako mstari wa mbele. Hawa uwatizame kwa jicho la huruma, uhakikishe mazingira wanayofanyia kazi yawe ni mazuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kujazia hapo kitu kimoja ambacho kinahusu hizi taasisi za binafsi. Mheshimiwa najua hizi taasisi binafsi nyingi ziko chini ya Wizara yako. Lakini taasisi hizi zimejitokeza kuwa mara nyingi sana wanakuwa wafanyakazi wao hawalipwi kile kiwango cha chini ambacho kinatakiwa na Serikali. Mhe. Naibu Spika, tuna taasisi moja ambayo inaitwa *Africa Muslim Agency* kwa upande wa Pemba hawa *all most* wanawalipa nusu tu ya kile kiwango ambacho wanatakiwa wawalipe.

Mhe. Waziri nakuomba uiangalie taasisi hii, uangalie kama kweli wao kwa sababu nadhani kwamba hawa wanamakubaliano na Wizara yako. Kwa hiyo nakuomba utizame ni kiasi gani wanawalipa wafanyakazi wao. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naingia katika kasma.

Mhe. Waziri nimekiangalia sana hiki kitabu ambacho kinaelezea kasma za Idara zako mbali mbali. Mhe. Waziri nimeangalia katika ukurasa 444 ya Afisi Kuu Pemba, ambayo ina Kasma kwenye kifungu 220408 ya Gharama ya Umeme. Mhe. Waziri gharama ya umeme hapa naiona imepanda mara 100 labda uje  utuelezee kwa nini au mlikuwa mna madeni, imepanda vibaya sana.
Mhe. Naibu Spika, tunaingia katika ukurasa huo huo Kasma ya 220508 tunaona hapa vile vile kuna kasma ambayo imetoka kwenye 500, mwaka jana matumizi yenu yalikuwa laki tano na arubaini lakini sasa hivi ni milioni moja na laki mbili. Ambayo ni ununuzi wa magazeti na majarida.

Mhe. Waziri nimeona katika kila Idara yako kuna ununuzi wa magazeti na majarida, lakini kasma yake ni kubwa. Sasa uje utuelezee hapa katika kila Idara mnanunua magazeti mangapi na jarida ngapi. Kweli haya magazeti na majarida yanasomwa au ni magazeti yananunuliwa yanakaa tu, tuangalie kama yanasomwa sawa lakini kama hayana shughuli maalum yanawekwa pale hayasomwi yanazidisha makaratasi ndani ya ofisi. Mheshimiwa kasma hii ipunguzwe na muendelee na ile ile ya laki tano na arubaini.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba kasma nyingi katika Wizara yako zimeongezeka sana. Kwanza kuna fungu ambalo limeandikwa linatolewa kwa wanafunzi, katika idara, kuna michango ya wanafunzi, Mhe. Waziri michango hiyo ni wanafunzi wepi na kuna *criteria* gani ambazo unatumia katika kuwapata wanafunzi hawa ambao watapewa michango.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nimeona katika Idara ya Mipango kuna *siting allowance* ambazo ni nyingi sana wakati mwaka jana hazikuwa hivyo, vimezidi mara nne au mara tano. Mheshimiwa naomba uje uteelezee hapa, kwa nini vifungu hivi vimezidi pengine mara mbili au mara tatu au zaidi ya hapo.

Baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mgeni Hassan kwa mchango wako. Sasa nafasi tunampa Mhe. Asha Bakari Makame, afuatie Mhe. Fatma Mbaouk Said na Mhe. Kazija Khamis Kona ajitayarishe.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote na mimi nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha, kutufikisha hapa katika hali ya usalama na afya. Pia Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, jinsi walivyokipanga vizuri kitabu hiki ambacho ni roho ya serikali. Kwa sababu hotuba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika inabeba sehemu kubwa sana ya ubinadamu ili kumwendeshea mwananchi maisha yake.

Pia nichukuwe nafasi hii Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana kwa aina yake Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman, kwa sababu Mhe. Waziri huyu ni mmoja wapo ambaye kwa kweli unapotoa maelekezo. Kwa sababu niseme kuwa hii ni wizara yangu katika kamati. Basi unapompa maelekezo basi anakaa na kama hajafahamu basi anakuita, mnakaa mnaita kamati mnashirikiana. Huo ndio upendo mkubwa ambao nampendea Mhe. Haroun Ali Suleiman. Sio waziri ambaye anapuuza maagizo au maelekezo kwa wizara yake. Ndio maana unamuona Mhe. Haroun Ali Suleiman anafanikiwa sana katika kila wizara ambayo anaigusa.

Kwa hivyo, niombe Mhe. Naibu Spika, na nitowe wito kwa wale wote ambao wamekopa au wamekopeshwa fedha katika wizara hii. Kwa kweli hawatotenda haki kama hawakulipa, kwa sababu wanawanyima haki zao wengine. Kwa hivyo, nitowe wito, kwa sababu nimeona humu katika marejesho, kwa kweli sio ya kuridhisha, ingawa wizara hii inafanya majukumu makubwa sana kufuatilia ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarejeshwa.

Pia niombe kwa serikali na hii sio mara ya kwanza Mhe. Naibu Spika, kuzungumza. Kwa sababu wizara hii ni tegemeo kubwa sana kwa wananchi na ni wizara ambayo tumeipa majukumu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kiushirika. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali na pia wizara mbali mbali ambazo zinahusika kushirikiana na wizara hii, kwa baadhi ya mikopo ambayo wizara zao inatoa mikopo. Kama Wizara ya Ufugaji na Uvuvi, niipongeze sana kwamba imeshirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumi na Ushirika ili kuhakikisha fedha zile zinapelekwa kule.

Kwa hivyo, naiomba serikali na nawaomba mawaziri wanaohusika na wanaokubaliana kwa mambo haya, wamshauri Rais kwa nia njema kabisa na tunayazungumza haya kwa nia njema kabisa. Tunajua kwamba Rais anashaurika, ukimshauri kwa kitu ambacho kina maslahi ya umma, kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto. Waachiwe Wizara ya Wanawake na Watoto, lakini mambo ya vijana ambayo yanahusu ajira, basi ipelekwe katika wizara hii. Hiyo ni kwa nia safi, kwa sababu tutamuezesha waziri wa wizara hii kufanya kazi zake ipasavyo na kumpa nguvu zote Mhe. Naibu Spika.
Kwa hivyo, naiomba sana serikali ikae itafakari ili ihakikishe kwamba wizara hii iwe ni wizara moja tu ambayo inapitia mikopo kwa wananchi. Ni kwa sababu zipi. Ni kwa sababu baadhi ya wakopaji wanaokopa wizara nyengine, wanakopa mara tatu au mara nne wanapitia wizara zote zile ili kupata mikopo na kutoweza kulipa mikopo ile.

Mhe. Naibu Spika, ukenda Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kama inakopesha basi utakwenda kukuta Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, mtu yule yule amekwenda kukopa. Ukenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi utakwenda kukuta mtu yule yule amekwenda kukopa wizara zote hizo anazitataga ili kumkosesha haki mwenzake ambaye ana haki ya kuweza kuchangia. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri akae na mawaziri wenzake ambao wanahusika, kama wanavyoshirikiana basi washirikiane ili wamshauri Rais vizuri kuhusu habari ya uwezeshaji, hasa hali halisi hasa.

Mhe. Naibu Spika, nizungumze tu kuhusu habari ya ajira mahotelini. Ningemuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na kwamba amefanyakazi kubwa. Lakini ningemuomba akatataga tena, mitatago ya kuhakikisha hotelini humo ajira zinafanyiwa mavarange, ni kwa sababu watu wanaajiriwa, lakini ikifika kupunguzwa wanapunguzwa kisha mtu mmoja anapewa kazi ambazo nyengine sio zake, ni kazi mara tatu mpaka nne anafanya mtu mmoja, hilo tumeligundua tunakuomba utilie mkazo zaidi. Lakini kuna wafanyakazi wa Bwawani Mhe. Naibu Spika, safari ile nilizungumza. Naishukuru sana wizara yako ilinisaidia sana, naomba bado wizara yako irudi tena Bwawani ikawasikilize wafanyakazi wa Bwawani, naiomba sana, kwa sababu bado kuna malalamiko ya wafanyakazi wa Bwawani ambao wamefanyakazi kwa muda wa miaka 14, lakini kuna mambo ambayo ambayo sio ya kuridhisha. Nakuomba sana hilo Mhe. Waziri.

Jengine la mwisho Mhe. Naibu Spika, naomba sana ofisi ya Pemba. Naiombea sana ofisi ya Pemba kwa kweli bado haijaridhisha. Nina imani kwamba una malengo ambayo umeyaweka, lakini malengo hayo bado ofisi ya Pemba kwa kweli haileti hadhi na wanabanana hata vifaa vya kukalia hakuna. Kubwa zaidi katika kitabu hiki na kwenye tabu kubwa, kwa sababu anayekupenda anakuambia ukweli. Kwa hivyo, naomba sana safari hii mmewanyima fedha kidogo, fedha mmewapa kidogo kwa mujibu wa matumizi. Sasa sijui Mhe. Waziri utafanyaje. Mimi nimepitia pitia kidogo, sijui mtafanyaje kwa sababu nyinyi ndio makao makuu huku Unguja mtajua nini cha kufanya, lakini kuna baadhi ya vifungu kwa kweli hamkuitendea haki kwa upande wa Pemba.
Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Nitawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wamuunge mkono Mhe. Waziri Maalim Haroun Ali Suleiman katika wizara yake, ahsante sana.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, katika kuwasilisha kwake Mhe. Waziri katika Baraza letu hili tukufu. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake. Pia niishukuru Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa maoni yake.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa nambari 13 katika hotuba hii ya Mhe. Waziri ambayo aliwasilisha kwetu kwa muda mdogo, kulingana na ukubwa wa kitabu hiki, nimshukuru sana. Kwa hivyo, niende moja kwa moja kwenye ukurasa nambari 13 unaozungumzia mradi wa kupambana na ajira za watoto.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema hapa kwamba wizara imeanza kutekeleza mradi wa kupambana na ajira mbaya kwa watoto. Lengo ni kuwanusuru watoto 5,000 katika wilaya 9 za

Unguja na Pemba dhidi ya ajira za watoto na kuzijengea uwezo wa kiuchumi familia za watu hawa.

Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie ni aina gani za uwezeshaji na kila wilaya kati ya hao watoto 5,000 basi aniambie ni watoto wangapi. Mhe. Naibu Spika, nikitoka ukurasa nambari 13, niende mpaka ukurasa wa 16 kwenye fungu 20, ambalo wizara imefanya tafiti katika maeneo muhimu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema katika hotuba yake ni maeneo mangapi aliyoyafanyia utafiti huo na ni rasilimali zipi zilizopo kwenye maeneo hayo. Mhe. Waziri ameelezea vizuri sana. Kwa hivyo, nilikuwa nataka hapo na ili nisipoteze muda wa kuzungumza sana niende katika vifungu hivyo hapo kwenye maeneo madogo madogo tu nitake hesabu zake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa namabari 24 fungu 26, Mhe. Waziri amesema kuna ofisi ya waziri. Kwanza nilitaka kujua Mhe. Waziri aniambie hii ofisi ya waziri iko inajitegemea na kama inajitegemea mbona hatuoni makisio yake. Pia amesema amebadilishana mawazo na wageni mbali mbali waliohudhuria pale. Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri je, ni mafanikio gani yaliyopatikana kwa wageni wale mbali mbali waliokuja.

Mhe. Naibu Spika, niende katika fungu 29 kwenye ukurasa nambari 27. Mhe. Waziri amesema katika ofisi yake mwaka 2011/2012 alipata bahati ya kushiriki mikutano na kutembelea nchi mbali mbali. Je, nchi hizo alitumia kiasi gani na faida iliyopatikana ni kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika ukurasa nambari 28 kuhusu Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji, kuanzia fungu 34 ambalo linasema kwamba suala la uwezeshaji wananchi linagusa kila sekta, katika mnasaba huu jumuiya ya wafanyabiashara na wakulima nayo imekuwa ikichangia juhudi za serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika ukurasa 33 ambao unazungumzia kupitia mpango wa uhakiki wa uwezo wa kibiashara, jumuiya ya wafanyabiashara imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali waliowasilisha mawazo mazuri ya biashara katika mwaka 2011/12. Kati ya vikundi 220 kati ya hivyo 199 ndio vilivyofaulu katika hatua hiyo. Je, hivi vikundi 21 vilivyokuwa havijaweza kufanya vizuri, niseme basi tu vikundi hivi vimeishia kunawa. Ni juhudi gani ambazo mnachukua Mhe. Waziri kwa sababu na wao wanataka kujiondoa katika umaskini, wizara yako haioni kwamba ikiishia hapo itakuwa bado hawajafikia lile lengo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa nambari 37 utekelezaji wa malengo ya idara ya mikopo. Utekelezaji wa malengo ya idara ya ushirika katika ukurasa wa 45, Mhe. Waziri katika hotuba fungu 42(6) linahusu kutoa mafunzo kwa wanachama na viongozi 3,000. Hili ni jambo la kupigiwa mfano sana na niseme kwamba waziri kwa sababu malengo yake ni mazuri na ni kutaka kuwaokoa wananchi wa visiwa hivi, kwa kweli nimshukuru sana waziri na nimpe pongezi kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nirudi nyuma katika ukurasa 37 unaohusu utekelezaji wa malengo ya idara ya mikopo. Kwa maelezo ya Mhe. Waziri yanasema kwamba ameendelea kuratibu mfuko wa JK. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri anieleze mkopo huu ni kwa vikundi, kwa sababu hapa amesema kuratibu shughuli za mfuko kwa JK ambapo unasimamiwa na Benki ya Watu wa

Zanzibar. Kupitia mfuko huu jumla ya shilingi bilioni 1,529,888,000 zimetumika. Sasa namuuliza ni kwa vikundi au ni kwa mtu mmoja mmoja.

Vile vile ningependa nimuombe Mhe. Waziri kwamba fedha hizi zinapotoka basi watujulishe na sisi viongozi wa majimbo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine niende kwenye ukurasa wa 42(6). Samahani Mhe. Naibu Spika, nimekwisha kukisoma kuhusu kumpa pongezi Mhe. Waziri kwa kutoa mafunzo kwa wanachama hao.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa nambari 42(8) niishukuru sana idara hii ya ushirika kwa kupitia Mhe. Waziri, kwa kutupa elimu na kufungua *SACCOS* benki katika jimbo langu la Amani, nimshukuru sana na elimu hiyo tumeipata na kwa sababu nia yetu ni njema pamoja na wao, maana wametushauri vizuri. Kwa hivyo, nimshukuru waziri kwa kutuwezesha wananchi wa Jimbo la Amani kielimu na kwa sababu elimu ni jambo muhimu sana, bila ya kuwa na elimu basi hata ufanye nini mafanikio yanakuwa ni madogo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa nambari 51. Mhe. Waziri amesema hapa jumla ya taasisi 327, taasisi 268 Unguja na 59 Pemba, zimefanyiwa ukaguzi kazi na miongozo imetolewa juu ya mapungufu yaliyobainika na kuagizwa kurekebishwa kasoro hizo. Pia ningependa kumuuliza Mhe. Waziri ni mapungufu gani hayo, kwa sababu inawezekana kumetokea mapungufu pengine ya kifedha au mengine yoyote. Kwa hivyo, ningependa akija Mhe. Waziri anieleze.

Mhe. Naibu Spika, hitimisho niseme kwamba namshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba. Pia nitowe pongezi kwa Mhe. Rashid Seif Suleiman, kwa kwenda mstari wa mbele. Vile vile nimpongeze Mhe. Hamadi Masoud kwa hiyari yake kuja mstari wa nyuma. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangi hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kabla ya yote kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia hali ya uzima na kuweza kukutana hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika jinsi anavyofuatilia kazi zake na maelekezo tunayompa kwenye kamati yetu anayafuatilia ipasavyo. Nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Kwanza Mhe Waziri hana kawaida ya kuwa wazo hili la mdogo asilichukuwe na kulifanyia kazi, hilo hana. Kwa hapo nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nimuombe basi Mhe. Waziri katika vikundi vya ushirika mikopo inayotolewa ni kidogo, yaani fedha ni kidogo sana ambayo haimuwezeshi mwananchi mahitaji yake. Kwa mfano, kama kuna wanaushirika wafugaji wa kuku, fedha wanazopewa ndogo na pia taaluma wanayopewa ni ndogo. Kwa sababu ikiwa hawana taaluma ya kutosheleza basi wanashindwa kufanya shughuli zao, hawajui kuku akiugua wamsaidie vipi

na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika, nimuombe waziri aliangalie suala hili.
Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba soko bado halijawa zuri kwa wajasiriamali hasa kwa wafugaji wa kuku. Hili ni tatizo ambalo limekuwa sugu na hasa kwa kuingia huu mradi wa hawa kuku kutoka nje, basi wanapata shida sana kuhusu soko hawa wananchi wetu wafugaji wa kuku, kwa maana hiyo nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja najitihada wanazozichukua basi na hili walifuatilie kwa ukaribu mno ili kuwakomboa wananchi wetu na ile sera tunayosema ya kuondoa hali umasikini basi tuwaondolee kwanza matatizo haya kuwatatutia masoko ili wajikwamuwe.

Halafu Mhe. Naibu Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri kuna vikundi ambavyo vimekufa kabisa. Kwa hivyo, nimuombe avifuatilie vikundi hivi, ili ajuwe matatizo yao ni nini halafu awasaidie kwa namna gani, atajua yeye Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika sekta binafsi yaani mahoteli. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri katika sekta hizi hasa za mahoteli bado tatizo lipo la kuwafungisha mikataba wanaowaajiri hasa kwa miezi mitatu. Sasa hapa Mhe. Waziri aje anieleze huu mkataba wa miezi mitatu wizara yake inaliona vipi au amewapangia vipi hawa anaowaajiri. Halafu kuna mikataba ya miezi mitatu na mikataba ya miezi sita. Kama mikataba hii ya miezi sita tayari imefika *low season* mahoteli yanafungwa, hawawaiti tena hawa waliowaajiri kwa maana hiyo tayari wameshawafukuza kazi na haki zao hawazipati tena. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri awafuatilie hawa wawekezaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna mpango huu wa kazi nje nje ulioshirikishwa na Shirika la Kazi Duniani ILO. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi Mhe. Waziri bado sijamuelewa vizuri, kwa sababu mimi nilidhani hapa ajira nje nje au kazi nje nje, mimi nilidhani zinapatikana tu kirahisi. Kwa hivyo, hapa aje atuelezee kwa sababu vijana wengi hawana kazi. Ukisema kazi nje nje basi vijana watajitokeza kumbe hakuna kazi ya aina yoyote Mhe. Spika. Kwa hivyo, aje atufafanulie vizuri wizara yake imepanga programu za aina gani, ili kuhakikisha kazi hizi zipo nje nje, kijana yeyote anafanikiwa na kazi hizi kwa mwenye fani hizo.

Halafu Mhe. Naibu Spika, niende katika mradi wa kupambana na ajira za watoto. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa katika nchi yetu na ni tatizo hasa kwa maeneo ya vijijini. Hili limezidi mno Mhe. Naibu Spika. Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwanza alifuatilie suala hili, na suala hili linatokana na kuwa watoto hawa wazee wao hawajiwezi, yaani kutokana na umasikini waliokuwa nao. Sasa nimuombe Mhe. Waziri kuna baadhi ya watoto wanajihusisha na biashara ndogo ndogo, kwa hivyo namuomba awafuatilie hawa hata skuli wanatoroka kutokana na kujihusisha na ajira hizi kupata mahitaji ya kujiwezesha wenyewe.

Halafu Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alitangaza huku kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi hasa mahotelini. Mhe. Naibu Spika, hapa kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweka kima cha chini cha mshahara. Lakini pia Mhe. Waziri suala hili baada ya kutangaza tu limezua tatizo kwa vijana wetu ambao wameajiriwa katika mahoteli, vijana wengi wamefukuzwa na wengine wamefukuzwa wala hawakupewa haki zao. Sasa nimuombe Mhe. Waziri alifuatilie suala hili kwa kina na pia awaelimishe hawa wanaoajiriwa namna gani ya kuzitambua haki zao kama hizi.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 31 nimpongeze tu hapa Mhe. Waziri katika kifungu nambari nne anasema, katika kunyanyua hamasa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi wizara yake imebuni mpango wa kuanzisha vijiji vya mfano. Katika kuanzia vijiji vilivyoteuliwa ni Mbuyutende. Mhe. Waziri hapa mimi nampongeza sana, kwa sababu kukiweka kijiji cha mfano Mbuyutende mimi nitafarajika sana, kwa sababu kule ni maeneo yangu. Lakini nimuombe tu kuwa kijiji hiki kimewekwa kuwa ni cha mfano basi huu mpango alioupanga auharakishe wakati tayari ameshachukua maoni na kila kitu, auharakishe ili uendelee na uonekane ni kweli kijiji cha Mbuyutende ni cha mfano hasa kutokana na hali zao walizokuwanazo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo ahsante sana naunga mkono hoja.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi niweze kusema machache sana juu ya wizara hii. Mhe. Naibu Spika, hii ni wizara yangu, mimi Mjumbe wa kamati kwanza nichukue nafasi kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na namna wanavyomsaidia Mhe. Waziri katika utekelezaji wake wa majukumu aliyopewa na Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, tuna jukumu zito na jukumu hili kaidhinishiwa Mhe. Waziri, na vipi tutamsaidia wizara hii inaitwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kazi inafanana na ile ajira, lakini yeye kapewa kwamba afanye namna ya kuwapatia watu kazi kupitia wizara hii. Wizara hii mwaka jana ndio imebuniwa, mwaka jana tukasema imepewa fedha kidogo sana kwa vile ilikuwa ni mpya, majukumu aliyopewa ni makubwa mno lakini uwezo anaopewa awezeshe haupo. Mimi nasema haupo shilingi bilioni mbili ni za kuwezesha ofisi tu Unguja na Pemba, atakopesha nani amuache nani. Lakini pia kuna vikundi na vyenyewe vinategemea mikopo kutoka hapa hapa.

Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri sasa anabebeshwa lawama sana na vikundi mbali mbali, lakini hana pa kutoa pesa kama hajaingiziwa, nasema kitabu hiki kwenye eneo la mikopo ni pale ambapo mtiririko wa mikopo utakapokuwa mzuri, ukiwa mbaya makusanyo huko hazina maana yake na yeye pia ni mabaya kwenye kukopesha.

Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali ikubali kwamba mwenzetu imempa mzigo mzito, ni vyema kumpa kila msaada lakini kwenye kasma ya fedha anayoihitaji iongezwe kwa sababu yeye maendeleo yake ni kuwakopesha hao wananchi, kuwawezesha hao wananchi, na wananchi kwenye suala la ajira Mhe. Naibu Spika, tusilitizame kwa vikundi tu na hata wasiokuwa na vikundi wanahitaji ajira. Naomba mimi nitumie nafasi hii kuishauri serikali kwamba tuna bomu zito limetukabili nalo ni la vijana, na vijana hawa hawakopesheki kwa sababu masharti yaliyoko kwenye mabenki hawawezi kukopeshwa hawana *security* wao watabaki kukaa vijiweni, na wakikaa vijiweni ndio hilo bomu ninalolisema. Lakini hawa pia huwezi kusema kwamba uwashushe shambani ajira ni kilimo, ni sahihi lakini kilimo ni kusindika mazao ya kilimo si kwenda kulima vijana humshushi shamba akakubali.

Jengine ni kusindika mazao ya bahari. Kwa masikitiko makubwa Mhe. Naibu Spika, maeneo haya bado tuko mbali nayo. Mimi kwa maoni yangu nadhani kwamba, kwa mtindo huu wa shilingi bilioni mbili kutiliwa wizara nzima ambayo inatarajiwa iwawezeshe wananchi safari

bado ni ngumu. Na wepesi wetu Mhe. Naibu Spika, ni lazima turudi kwenye viwanda, hatuna namna kwa sababu wizara iliyotengwa kusaidia ndio hii shilingi bilioni mbili, tena tukimaliza hapa kumpitishia si kwamba zitakuweko itategemea namna zitakavyopatikana. Tatizo hili.

Lakini jengine hivi vyama vya ushirika malengo ni mazuri, sera nzuri, zinasaidia sana Mhe. Naibu Spika, hivi vyama vya ushirika lakini bado tunarudi kwamba tatizo ni fedha, fedha hapana.

Mhe. Naibu Spika, hebu serikali iamue katika hili, vijana hawa kama hatukupata kuwapa sehemu itakuwa tatizo kubwa, leo hali na matukio yanayoendelea kutokea katika nchi hii miaka mia iliyopita hayajatokea na haya ni kwa sababu ya watu hawana ajira.

Mhe. Naibu Spika, nilisema viwanda ndio mkombozi wetu, Mhe. Waziri atakapowakopesha watu wamejiunga kikundi vikundi hivi Mhe. Naibu Spika, viliumbwaumbwa tu huko nyuma tunakotoka kwa sababu mbali mbali, *seriousness* ya vikundi vyenyewe kwamba kweli vinahitaji kujiajiri haikuwepo kila mtu anajua humu ndani tulimo, ni vichache mno.

Leo Mhe. Naibu Spika, tunashuhudia kinamama wengi wao wameamka kweli kujitafutia hatma ya maisha yao kiuchumi, lakini mikopo hii haipo na haipo kwa sababu Mhe. Waziri pesa hana. Mhe. Naibu Spika, serikali ikubali kwamba tutumie rasilimali bahari, tutumie rasilimali ya ardhi, tuvijenge viwanda tuwaite wawekezaji tuingie nao mikataba, watusaidie katika janga hili vijana hawana ajira ni tatizo kubwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, na viwanda vyenyewe navyo tuna mitihani, maana lazima tuwabembeleze na wenzetu wa upande wa pili wakubali kutoa leseni na kadiri wanavyohisi kwamba hapa tutatoka huwa ni wagumu sijui ni *formula* gani Mhe. Waziri atatumia katika hilo, ni mzuri kwa kwenda ku-*bargain* na anakubaliwa mengi anafanikiwa, lakini kwa hapa kwenye suala la viwanda lazima apate msaada wa ziada.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka sana ajira za watoto lakini ajira za Wazanzibari mahotelini. Mhe. Naibu Spika, kuna ajira nadhani haijawa rasmi, kuna Wazanzibari wanatoka nje ya nchi sasa hivi sana Ghuba hatimaye kesi ambayo nimeishuhudia mwenyewe binti kapelekwa huko kufanya kazi za ndani, yaliyomkuta bahati mbaya ni mabaya mno, magumu, wazazi wake wakataka angalau apate fedha za kumpelekea aweze kurudi hapa. Wazee wameweka rehani nyumba wanayoishi, vishamba, yule binti kapatikana karudi. Mhe. Waziri hili lipo na linaendelea hapa Unguja kuna sehemu nazijua kuna watoto wameshapelekwa na wanapelekwa mabinti, usalama wa watoto hawa na dhamira hiyo ya ajira ya majumbani hatimaye huwa inabadilika. Mhe. Waziri nakuomba sana hebu tutafute namna ya kuokoa hili.

Lakini jengine mahotelini, bado Mhe. Waziri ndugu zetu wanafikwa na makubwa wanadhalilishwa mno na haki zao zile za kimsingi pia hawazipati kama inavyostahiki. Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia muda huu mfupi na mimi kutia baraka yangu ndani ya wizara hii, namtakia kila la kheri Mhe. Waziri, lakini namuomba kwenye Mikutano ya Baraza la Mawaziri kwa makusudi amtake Mhe. Rais kwamba hali hii ya mgao wa fedha anaoupata hataweza kufika lengo alilomchagulia yeye kumpa dhamana hii. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu na sasa tunamuita Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu tokea jana bajeti hii imekuwa ikichangiwa na Alhamdulillah tumefika saa sita na kwa umri wa jana wa miaka 59 basi leo umri wangu ni siku moja, kwa sababu saa sita kama hizi ndio nilipozaliwa. Kwa hivyo, nawashukuru sana Waheshimiwa walikuwa wanamchangia mtoto mchanga na wamechangia kwa utaratibu huo huo wa upole na kutupa miongozo mizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana ukiwemo kwanza wewe Mhe. Naibu Spika, na jana Spika mwenyewe namna tulivyokwenda na michango hiyo. Awali ilionekana ni wachache lakini kadiri wakati ulipokwenda na mambo yameongezeka. Mimi nakiri nimekuwepo Barazani nadhani miaka 12 sasa inakaribia na kwa mawaziri nadhani mimi nitakuwa ndio *longest serving minister* katika *cabinet* sasa hivi kwa mfululizo ingawa nimeshindwa na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati lakini yeye anaingia kwa vipindi vipindi. Lakini namna ninavyoiona michango ya Waheshimiwa inavyokwenda inanikumbusha hadithi Mhe. Naibu Spika, naomba ruhusa yako niitoe.

Hii maana yake nini, ni kwamba siku moja Mhe. Saleh alizungumza pale muasisi, alisema wale waliokuwa mbele kule wasione kwamba wanajua sana kuliko sisi tuliokuwa huku nyuma, lakini alikuwa na nia nzuri sio kudharau hapana, alikuwa anakusudia kusema kwamba, hata michango inayotolewa na *back bencher* ni mizuri na mengine hata Mawaziri watakuwa hawayaelewi wanaeleweshwa na hao Waheshimiwa. Sasa ni suala la kuheshimu michango yao ndio naendelea na hiyo hadithi yangu sasa.

Kuna mtu mmoja kiongozi fulani wa dini alipata nafasi katika eneo fulani kwenda kufanya kazi, kenda wakati wa jioni pale na alipofika akawa hana chakula nyumbani, ilibidi akitafute chakula akaanza kuingia mitaani akawakuta watoto wanachezacheza njiani, akawauliza nyinyi watoto mahali gani hapa naweza nikapata chakula, matunda na mambo mengine yanayohusiana na hayo? Wakamwambia pita njia hiyo halafu elekea Kusini nenda mashariki utafika. Bahati nzuri akenda akaelekea kule mbele akaenda mpaka akafika hapo mahali akanunua chakula chake na matunda akaja nayo, aliporudi kwa sababu yeye ni kiongozi wa kidini akamwambia kijana njoo, umenisaidia sana nilikuwa sina mahali pa kwenda kuchukua chakula kwa hivyo njoo kule kwenye eneo langu ambalo natoa mafunzo ya dini ili uje nikufahamishe na nikueleweshe njia ya kuingia peponi. Yeye aliona anamwambia jambo zuri lakini yule kijana akamjibu, babu ikiwa njia ya sokoni huijui utaijua njia ya peponi? Sasa hii maana yake kwamba ni lazima tunapoelekezwa sisi kama Mawaziri tufuate, tusione kwamba labda tunabebeshwa mambo au mizigo ambayo ni *un necessary*.

Kwa hivyo, nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na naomba niwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia kwa siku ya leo ambapo kwa jumla waliochangia moja kwa moja ni 22, na waliochangia kwa maandishi ni watatu, kwa ruhusa yako naomba niwataje.

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

4. Mhe. Abdi Mossi Kombo (Kepteni)
5. Mhe. Nassor Salim Ali
6. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
7. Mhe. Ali Abdalla Ali
8. Mhe. Hamza Hassan Juma
9. Mhe. Mussa Ali Hassan
10. Mhe. Ashura Sharif Ali
11. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
12. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
13. Mhe. Ali Salum Haji
14. Mhe. Panya Ali Abdalla
15. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Asha Bakari Makame
18. Mhe. Fatma Mbarouk Said
19. Mhe. Kazija Khamis Kona
20. Mhe. Asaa Othman Hamad

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Shadya Mohamed
2. Mhe. Asha Abdu Haji na
3. Mhe. Marina Joel Thomas

Nawashukuru sana Mhe. Naibu Spika, nitajitahidi kutoa ufafanuzi wa hapa na pale, na pale ambapo nitashindwa sitokuwa na maana labda nimedharau, lakini na muda nao utaweza kunisaidia zaidi Mhe. Spika, unapokaribia kumalizika. Lakini nitajitahidi kutoa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ya msingi yametokea hapa na yote ni mazuri na wengi wamesema kwamba Mhe. Waziri ni msikivu na kweli sina tabia ya ukaidi. Hata nilipokuwa nasomesha darasani basi wanafunzi wangu wakati mwengine walikuwa wananielekeza na kuniuliza maswali, na sikumbuki kuwa nilikasirika, sijui kama Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mahmoud Mohammed, Mhe. Marina na wengineo kama mtakumbuka niliwahi kukutoleeni ukali mkiniuliza maswali. Ukiona mwalimu anaulizwa swali anakasirika ana tatizo kwenye *profession* yake huyo.

Kwa hivyo, mimi leo napata faraja kubwa kwamba wanafunzi wangu wanamuuliza mwalimu sasa, na lazima niwe na fakhari kwao wao kwa sababu na humu ndani wanafika kama 10 wanafunzi na wengine kina Mhe. Machano Othman Said wangesoma zile skuli ambazo nimesomesha nao ningewasomesha vile vile, lakini walipitia skuli nyengine yeye na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Mansoor Yussuf Himid, lakini wote tungewapata. Kwa hivyo, nashukuru sana kwamba bado Mwenyezi Mungu amenipa nguvu na *Inshaallah* azidi kunipa nguvu.

Sasa hapa pametolewa mapendekezo mengi ya kuyapeleka serikalini, masuala ya wizara hizi Mhe. Ismail Jussa kazungumza, Mhe. Asha Bakari kazungumza wizara hizi kuwa kuna

muingiliano wa majukumu. Lakini kuna mwaka mmoja wakati nikiwa Waziri wa Elimu nilisema jambo moja na hapa naomba nilirejee leo. Yanatolewa mapendekezo mengi sana ya Waheshimiwa hapa kuyapeleka serikalini, lakini nina wasi wasi kama yanafika serikalini.

Kwa sababu inavyotakiwa kama hapa yametoka mapendekezo mkuu wa shughuli za serikali anakusanya yale halafu anayapeleka mbele. Sasa ni vizuri suala hili au utamaduni huu yamependekezwa mambo mengi, na mimi siwezi kuyaingilia kwa sababu ni masuala ambayo yako kwenye mamlaka ya Rais, lakini kupeleka mapendekezo nadhani hayatakuwa na madhara mambo kama hayo. Kwa hivyo, nashauri baadhi ya mapendekezo kwa mfano Mhe. Asha Bakari kapendekeza Mifuko yote hii ya utoaji mikopo ielekezwe kwenye Wizara inayohusika na mikopo.

Mhe. Asaa Othman kazungumza kwa vizuri sana hapa anasema kadiri itavyokuwa tunamuuliza maswali tunamwambia Mhe. Waziri awezeshe wananchi, kama hana nyenzo basi hawezi kufanya kazi hizo. Lakini likaja suala la mambo ya vijana haya nayo yakaonekana pengine ingefaa yakawekwa pahali maalum ili kuweza kupata nguvu zaidi. Sasa ni masuala ambayo ni muhimu, nadhani ipo haja ya kuyaangalia na sisi serikali tutayajadili kwa upande wetu tutashauriana na Mkuu wa Shughuli za humu ndani nitamuelekeza yale mambo yaliyotakiwa na Waheshimiwa ili baadae nimkabidhi halafu tujue namna tutakavyoyafanya. Lakini kuna mambo ambayo serikali imejiandaa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo kubwa ambalo limejitokeza hapa wengi wetu na Mhe. Naibu Spika pale ambapo hapana budi nitataja lakini nitajaribu kujibu kwa jumla jumla ili kupunguza muda vile vile. Masuala ya mikataba ya *ZANTEL*, mikataba ya Mahotelini na mambo ya aina hiyo. Nakiri Mhe. Naibu Spika, mbele ya Wajumbe wako kwamba tatizo ni kubwa, mimi nimekwenda wizarani tumeyaona mambo yaliyokuwepo pale, mambo yalikuwa mengi Mheshimiwa tumejitahidi lakini hatuyamalizi yote kwa siku moja. Wizara hii ilikuwa ni mpya wengi wamehoji mbona vifungu vimetononoka, mbona vifungu vimekuwa vikubwa.
Mwaka jana Mhe. Asaa kazungumza nimepewa shilingi bilioni moja kama sikosei nadhani na milioni mia tano wizara nzima, nitawawezesha wapi wananchi, vikundi vya ushirika vitapata wapi fedha, uwezo ulikuwa ni mdogo na hii ni wizara mpya ndio kwanza serikali ilikuwa inaingia madarakani isingekuwa rahisi. Kwa hivyo, keki iliyokuwepo serikalini tuligawana kidogo kidogo mimi nikapewa changu, nilisema sana niongezwe lakini hakipo. Mwaka huu kidogo mambo yameongezwa nashukuru, zile bajeti ambazo zilikuwepo mwaka jana katika *item* mbali mbali sio kama ndio zilikuwa zinakidhi mahitaji kwa wakati ule na ndio maana zikaonekana ndogo sana kwa sababu kiwango nilichopata kilikuwa kidogo, ilibidi sasa nikitumie hicho hicho. Sasa mwaka huu nashukuru kidogo zimeongezwa lakini katika kuongezwa na sisi tumeongeza, kwa hivyo ile tofauti inaonekana kubwa sio kwa sababu tulikuwa na milioni ngapi sijui.

Kwa mfano, katika magazeti tulikuwa na shilingi milioni mbili laki tano safari hii tumesema shilingi milioni moja laki mbili. Kwa sababu kwanza hizo idara zenyewe zilikuwa hazijakaa mahali maalum sasa hivi *Alhamdulillah* idara zote zimekaa vizuri, magazeti yale ambayo yamedaiwa na baadhi ya Waheshimiwa ni kweli, magazeti katika kila idara pale wanapata na magazeti yote kwa upande wa wizara yamekaa pale katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi, na

huku kwengine kwa upande wa Pemba wamewekewa yao maalum. Sasa tunapozungumza magazeti kutoka shilingi laki tano tumekwenda shilingi milioni moja laki mbili.

Lakini katika magazeti yale yale wizara hii ina utaratibu, mwaka jana tulishindwa kwa sababu ya pesa, katika makala, majarida, lakini pia huwa tunachapisha na kalenda ambazo huwa tunazisambaza katika maeneo mbali mbali kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Kwa sababu huwa tunapiga picha za vikundi vya ushirika mbali mbali na shughuli mbali mbali ambazo zinafanywa na wizara na ndio zinaonekana zimepanda kwa sababu ya jambo hilo. Lakini pia sio kwamba kile tulichopewa mwaka jana ndio kilikuwa kinatosheleza mahitaji kutokana na kile ambacho tulikipata ndio kikaonekana kidogo.

Suala la mikataba Mhe. Naibu Spika, ni tatizo kubwa kweli. Mimi nawashukuru Waheshimiwa wote, Mhe. Ismail alizungumza, Mhe. Hamza Hassan, juhudi tumefanya Mheshimiwa na mengine Mawaziri tunakuwa hatuyajui mpaka tuarifiwe. Sasa kama kuna mambo yanatendeka kwa watendaji tu hayafiki huku juu na wananchi, wafanyakazi huko wanapata matatizo hawaji wizarani, wakishafika kwa Mkurugenzi, kwa Kamishna wanaona ndio yamekwisha. Mimi nilisema siku moja wizara yangu bahati nzuri nimeacha milango wazi na madirisha, tena bahati nzuri hata paa halijajengwa kule juu kama wana uwezo wa kupitia kule juu wapite wafike ofisini kwangu, lakini *Inshaallah* baada ya miaka miwili tutakuwa na paa letu zuri tutapandisha ghorofa tukijaaliwa *Inshaallah*.

Sasa nakubali matatizo na naomba sana Waheshimiwa nahitaji wanipe muda zaidi. Jana Mhe. Ismail Jussa kaeleza matatizo ya suala la mikataba hawatendewi haki Wazanzibari. Nikachukua juhudi jana usiku na leo na nishampelekea *memo* au *e-mail* ambayo kaniletea kiongozi wa *ZANTEL* anayehusika na mambo ya *human resource*. Sasa kanijibu sijaridhika, alichonijibu ndicho kile ambacho kimo kwenye mikataba ni yale yale, kinachodaiwa ni nini? Kwa nini mfanyakazi wa *level* ile ile wa Zanzibar analipwa kima cha chini sawa nashukuru hilo wamelikubali, lakini kuna mambo ya *benefit* nyengine hawalipwi na wengine wanafanya kazi zile zile lakini wanalipwa.

Hili haliwezi kukubalika Mhe. Naibu Spika, na mimi madhali nimepewa jukumu hili na mimi nina uchungu sana na nchi hii tena sana, nimezaliwa katika nchi hii, baba yangu kazaliwa nchi hii na mama bila shaka, babu yangu na bibi zangu pia wamezaliwa katika nchi hii. Nimekuwemo kwenye serikali si haba *Alhamdulillah* kwenye ualimu karibu miaka 20 imekaribia, Naibu Mkurugenzi miaka mitatu, Naibu Katibu Mkuu miaka mitano, Waziri wa Elimu miaka kumi na sasa Wizara ya Kazi; nimesomesha sasa naambiwa niwape kazi, ndio kazi yangu nitaifanya hiyo tukijaaliwa.

Kwa hivyo nina uchungu sana na nimefanya mambo mimi ninapokuwa nje ya nchi kwa maslahi ya Zanzibar mengi Mheshimiwa. Ninatoa mfano jambo moja zito sana lilifanyika. Tulipokwenda Afrika Kusini, mimi nilialikwa mkutano na bosi wa *Microsoft*, ninadhani tunamuelewa sote ni Bill Gates kwa sababu tulikuwa tunataka kuingia kwenye mitandao sasa hivi na kutuunganisha katika mitandao mbali mbali, akatualika na bahati nzuri akamualika na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Karume wakati ule.

Akamualika na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na watendaji wake. Zanzibar ilialikwa kama Zanzibar na Tanzania upande wa Bara amealika Rais kenda kule. Tulipofika kule watendaji wakanijia wakaniambia sasa mheshimiwa tupo hapa Zanzibar na Tanzania basi tuwe na makubaliano ya aina moja.

Nikawaambia kwani wewe ndio uliyenialika wewe?, alikuwa mama yule. Huyo aliyenialika hajaniambia hayo Bill Gates si yule pale na Bill Clinton alikuwepo, hizo picha tu hazijapatikana mpaka leo.

Sasa ilifanyika nini. Kumbe hata Rais mwenyewe hata hana habari na ndio pale niliposema kuna mambo yanafanyika huku chini viongozi wa juu wanakuwa hawana habari. Nikamwambia sikiliza kama munasaini saini, mimi nitamwambia Rais Karume turudi kwa sababu sisi ndio hatuhusiki na suala hili.

Baadae nikamuarifu Dr. Karume, nikamwambia mheshimiwa kuna jambo hili, akaniambia hapana lisimamie utizame linavyokwenda. Basi ikahojiwa Zanzibar ika *sign*, aka-*sign* Rais Karume pale wakati ule. Anatoka saa tano, tano na robo anaingia Rais Kikwete, Rais Kikwete anamuuliza Rais Karume vipi rafiki yangu umeshaanguka huko, akamwambia tayari, hata hana habari nayo yale yote yaliyokuwa yamezungumzwa.(*Makofi*).

Ninaliongezea na lile la mkataba wa Qatar na Oman wengi wamelizungumzia hapa. Mimi kweli nilikwenda Oman si mara moja wala mara mbili, na hili ninamjibu Mhe. Fatma kwamba kuna matunda gani au faida gani inapatikana.

Mhe. Ismail *he was very right* kwamba nimelianzisha mimi kwamba sasa likataka kuingiliwa upande mwengine. Hapana tumeshamaliza Zanzibar na Oman tumeshamaliza, hivi sasa imepelekwa kwenye *cabinet* yao inangoja *approval*, lakini kila kitu tayari na hii itakuwa moja kwa moja kati ya Zanzibar na Oman.(*Makofi*).

La Qatar mimi nilipata bahati nilikwambieni. Mfalme alikuja kupumzika baada ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kama huu alikuja hapa, Khalifa yule. Rais Karume wakati ule akaniambia kampokee, nikenda alhamdullah madam ninaweza kusema, "*please and thank you*" basi nikenda. Nikamkaribisha akenda kulala kwenye meli yake, ikatokea kikao cha dharura cha nchi za Gulf na yeye akaitwa akarudi, nikamsindikiza akaja tena baada ya siku mbili nikampokea tena mimi. Siku ya kuondoka akamwambia mke wake ambaye ni Mwenyekiti wa Qatar Foundation anayeitwa Shekha Mozzay; ni mama mmoja ambaye *very intelligent*, *bright* hodari, akasema tumualike Waziri aje Qatar katika mwezi wa Disemba. Kwa hivyo Disemba 6 mpaka 10 nikaletewa mwaliko kutoka huko huko kwa bwana mkubwa.

Nikapokewa mheshimiwa kwa heshima zote Waziri kutoka Zanzibar. Nikenda pale nikaekwa katika hoteli ambayo alhamdullah sijakaa siku nyingi. Wale wasaidizi wanawahimiza watu wa hoteli mshughulikieni na mumuangalie sana, anayeambiwa ndiye mimi Mmakunduchi, mshambamshamba, *I feel proud* hata kuambiwa mshamba hata si tatizo.

Lakini siku ya pili nikapangiwa ratiba nikamuone mfalme jamani. Mtu mkubwa wa nchi na mimi ni Waziri tu. Nikenda niliyoyaona kule ndio nimeyaona. Tukazungumza na akaniuliza unataka

nini. Nikamwambia hapa pana Qatar Foundation, ninataka tuwe na Zanzibar Foundation vile vile utusaidie, hayo hayo maeneo. Akawaachia kazi wasaidizi wake. Baada ya mwezi mmoja Mhe. Naibu Spika, wakaja wasaidizi wakafanya utafiti wao wakapitia mote humo.

Mwaka jana nilipokwenda kwenye mkutano wa Geneva, faida nyengine Mhe. Fatma hiyo nikakutana na Waziri wa Qatar nikamwambia sasa wakati umefika, wakati huu kuna Qatar Foundation mambo ya *health*, Mhe. Juma Duni ni shahidi, alikuja pale tumezungumza mambo mengi na ile *program* ukiiona Mwenyezi Mungu akitujaalia inshaallah tunatarajia tukianza ku-*implement* matatizo ya hospitali yatakuwa ni historia tu.

Kwenye elimu hivyo hivyo na maeneo mengine ya *empowerment* tumeyaingiza. Basi wakaja wakafanya utafiti wao wakapeleka. Lakini nilipokutana na Waziri nikamwambia sasa tuwe na MOU yetu, haya haya. Juzi nipo wizarani Katibu Mkuu akaniletea, mambo ya nje wanamletea Katibu Mkuu wangu wanamwambia tunaomba mutoe maoni yenu juu ya mkataba huu uliotoka Qatar, mapendekezo yetu tunayotaka kuyapaleka Qatar kwa ajili ya mkataba wa pamoja kati ya Tanzania na Qatar. Mmh! nikasema haya si makubaliano. Ninasikitika ile barua sikuileta niliyomwambia Katibu Mkuu ajibu.

Nilimwambia ajibu hivi. Qatar na Zanzibar inahitajia kuwa na mkataba wake mbali na sio sawa na ule ambao ulioletwa na Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo hatukupeleka pendekezo lolote la kupendekeza la kurekebisha MOU kwa sababu sio makubaliano yetu.

Lakini juzi tu nimezungumza na Makamo Mwenyekiti wa Qatar Foundation, ninafikiri ni jana na akaniambia Waziri *is simple way* fanya hivi, chukua *address* hii muandikie mwenyewe moja kwa moja kwa sababu umeshafika huko wewe muhimize habari ya Qatar Foundation na hiyo habari ya *contract* ya Zanzibar muandikie Waziri mwenzako mwambie kwamba haya ndio makubaliano, na mimi nililetee hizo barua nitazipeleka. Kwa hivyo tumefika hatua hiyo mheshimiwa. Kwa hivyo uchungu wa nchi tunao na tutaendelea kuitumikia nchi yetu tukijaaliwa inshaallah. Wala musifikirie sisi tunafurahia haya mengine yanayotokezea, kama ajira hizo ambazo Wazanzibari wanakosa, hapana. Lakini ni vizuri tutumie diplomasia ya hali ya juu na tuzungumze vizuri ili tufahamiane. (Makofi).

Hata pale mwanzo Mhe. Naibu Spika, tulipoanzisha Vyuo Vikuu ambapo wengi wamezungumza hapa. Lilikuwa ni suala la muungano na mpaka leo limekuwa ni la muungano na halikuwa rahisi.Lakini kwa mashirikiano makubwa na mawaziri waliokuwepo wakati ule na sisi tuliokuwepo wakati ule, tukashirikiana leo Chuo Kikuu kimeshatimiza miaka 10 tunashukuru Mungu. (*Makofi*).

Tulipojiunga na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Afrika (*CAF*) mwaka 2003/2004 Mhe. Said Ali Mbarouk haikuwa rahisi. Kuna mtu alinipigia simu mbona Zanzibar imekuja na bendera Kenya, kulikuwa na mashindano ya Africa Cup haya. Lakini tumekwenda na bendera na wimbo wa taifa unapigwa. Nikajibu masuala haya tumekubaliana na waziri anayehusika na michezo Prof. Kapuya wakati ule rafiki yangu, tukashirikiana tukapeleka ujumbe Cairo, wakenda na wakaja na jibu kwamba Zanzibar imekubaliwa hata katika ile *status* ya kwamba ni *observer*, lakini tunashiriki kama timu nyengine yoyote.(*Makofi*).

Bado tunahangaika kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo si ya muungano na hata viongozi wakuu wameshasema, yale mambo ambayo si ya muungano basi tujitahidi Zanzibar ipate nafasi ya kufanya shughuli zake mbali mbali na hayo Mhe. Naibu Spika, ndio tunayoyafanyia kazi.

Mambo ya kazi si ya muungano, na mule kwenye kitabu changu nimeandika kwamba tumeshirikiana na wenzetu, kushirikianza hakuna matatizo. Lakini tujue tu kwamba masuala haya si ya muungano na ndio maana hata mkataba wa Qatar ulipokuja sisi kutoka mambo ya nje, tukasema sisi tunahitajia kuwa na mkataba wetu kwa sababu ndio makubaliano ya awali ambayo tuliyoyafanya. Kwa hivyo tunajitahidi Mhe. Naibu Spika, tumefanya hivyo.

Suala lile la taasisi ambalo Mhe. Jussa aliliulizia mambo ya utafiti. Tukalitolea ufafanuzi wa *assessment*. Nayo vile vile Zanzibar imeshiriki kama Zanzibar tokea mwanzo mpaka mwisho. Kwa hivyo hayo wanayozungumza kwamba mikataba, ajira wapatiwe Wazanzibari. Hayo ndivyo yalivyo. Sasa kulikuwa kuna sheria ya utalii ilipitishwa hapa juzi na Mhe. Jussa akasema tuliahidiwa kwamba angalau kwenye kanuni itawekwa pale badala ya Mtanzania itawekwa Mzanzibari. Lakini sasa bahati mbaya ile ni ya Wizara ya Utalii. Waziri anayehusika na mambo ya utalii anawajibika yeye kuangalia kanuni ile kwa sababu ilikuwa ni ahadi ndani ya Baraza.

Lakini sisi upande wetu wa wizara kwenye mawakala hawa binafsi, tumeweka mawakala binafsi tunawapa Wazanzibari tu ndio ambao wanaweza kusimamia suala lile. Mhe. Naibu Spika, wanne wameshajitokeza wanafanya kazi vizuri na hawa hatujawazuia na tutawaita tena wizarani kama alivyonishauri Mhe. Makame Mshimba, hebu tuwaite tuzungumze nao, wasitafute kazi za nje wakati kazi za ndani zipo tele ambazo tunaweza tukazitafuta vile vile.

Wizara yangu mimi haina jukumu la kulazimisha watu wakafanye kazi. Mimi kazi yangu ni kuratibu shughuli au kuwezesha wananchi ili kuwapeleka maeneo kwamba jamani kuna kazi hizi, na wale ambao walisema kuwa tungekuwa na kituo maalum cha kuripoti.

Mhe. Naibu Spika, karibu mwaka mmoja na nusu pale wizarani kwangu, Waheshimiwa Wajumbe njooni pale kuna mambo makubwa sana mutayaona. Kile kituo cha kutoa taarifa za ajira kipo pale na kinafanya kazi vizuri na vijana wanakitumia sana pale wanakuja. Lakini tatizo ni kwamba vijana hawa ni wengi, wanakukupurukeni huko hamna wanakuja moja kwa moja kwetu sisi.

Mimi naomba kwa suala hili la ajira na masuala ya uwezeshaji yote Mhe. Naibu Spika, Baraza letu la Wawakilishi lina jukumu kubwa sana kuhusiana na jambo hili. Kuna malalamiko mengi kwamba *SACCOS* imepewa mikopo, vyama vya ushirika vinapata mikopo, mmoja mmoja anapata mikopo wakati sisi viongozi hatuna habari.

Mimi nimeahidi hapa kuanzia bajeti ya mwaka huu, tuliulizwa katika swali na nikasema kuanzia sasa hivi mkopo wowote utakaotolewa au ziara nitazozifanya kwenye maeneo mbali mbali, Waheshimiwa Wawakilishi kwenye maeneo yale wataalikwa ili waje na waonekane na wao wanafanya kazi na ndio jukumu lao ni hilo. (*Makofi*).

Lakini masikitiko yangu Mhe. Naibu Spika, hata pale ambapo baadhi ninawapelekea taarifa kwamba ninakuja hawaji, kazi zinakuwa ni nyingi. Sasa suala linakuja Barazani kwamba

hamtushirikishi. Sasa safari hii Mhe. Naibu Spika, nitafanya hivi, nitawaalika na nakala nitakuletea Mhe. Naibu Spika, ili wakija wakilalamika kama hatuwashirikishi basi nakala iwepo ya kusema hivyo.

Matatizo ya Mji Mkongwe tunayajua kweli vijana wale, amesema Mhe. Jussa kwamba vinyago vingi. Lakini sasa nao wanatafuta riziki zao kwa njia moja au nyengine, sawa lakini hatuwezi kuendelea kwa hatua ile tunayokwenda hivi sasa, ni lazima tushirikiane na sekta inayohusika Baraza la Manispaa, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, tushirikiane nao, Wizara ya Utalii tushirikiane kwa sababu hatutaki kuharibu *business* yetu vile vile, kwa sababu na watalii nao wanataka kuona mambo ambayo ni tofauti na kule kwao ambayo wanayaona.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, tunajitahidi. Mikataba ya Zantel ninarudi pale pale. Naomba kwa Mhe. Jussa na Waheshimiwa wengine wote walioomba kuwa watazuia vifungu mpaka hapo watakapopata jawabu. Jamani kwa hili ninakuombeni muniachie, Jumatatu nimewaita uongozi wa Zantel wote watakuja watanieleza na mimi nitawaeleza yangu.

Kila haki ambayo walistahiki kuipata kama mwenzake ninakuhakikishieni, nilisema sina asili ya ukaidi lakini mimi nina msimamo. Ninaloamini kwamba ninaliamini nitaliamini kweli kweli ndani ya moyo wangu na wala hakuna mtu wa kunibadilisha. Nikishaliamini kwamba hili lina mwelekeo na hasa kwa yale yanayowasaidia wananchi wa Zanzibar hilo sina tatizo nalo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Zanzibar (*SUZA*) na *ZANTEL* wamekubaliana wao, Wizara yangu haikuhusishwa kabisa. Kwa hivyo wanapewa kazi ya kuwatafuta vijana wa kuwapeleka kwenye ile *consent* pale kati ya *Zanzibar University* na *ZANTEL*. Lakini Mhe. Naibu Spika, wanasheria wamo ndani humu. Mimi kazi yangu nikishapata lalamiko tunamu-*advice* sasa, tuna kitengo kinaitwa *DHU*. *DHU* maana yake nini? Ni kitengo ambacho kinaitwa *Dispute Handling Unit*. Ni kitengo cha migogoro ya kazi kipo pale, kimeanzishwa na Mwenyekiti na bodi yake tayari, nimeanzisha hivi karibuni.

Watu wote au wananchi wote waliokuwa na matatizo na mikataba yao basi wote bila hata ya kupitia wizarani kwangu wakitaka sisi tutawapa miongozo ili wafike, kwa sababu kipo kwenye mamlaka ya wizara yetu. Mahakama ya Kazi ipo vile vile pale Mwanakwerekwe.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina hakika wakenda pale haki zao zote wanazostahiki kisheria watapatiwa. Mimi kama Waziri siwezi kumlazimisha Meneja wa Zantel au sio wa Zantel walipe mshahara huu kwa sababu ule mkataba ni kati ya yule muajiriwa na muajiri. Isipokuwa sasa ana haki na mimi kama ninayesimamia suala la ajira, aje anilalamikie, na akija kwangu mimi ninachofanya ninamwabia nenda kwenye kitengo kile cha kutatua migogoro ya kazi. Pale akishindwa jambo ambalo tunataka lisifike mwisho anakwenda Mahakama ya Kazi.

Mhe. Naibu Spika, tumefanya hivyo, mara moja, mbili, tatu. Vijana wengi waliokuja na malalamiko wamepitia eneo hilo, wamekwenda mpaka kwenye Mahakama ya Kazi. Zaidi ya kesi 18 ninadhani tayari wananchi wameshakwenda pale wamepatiwa haki zao. Naomba sana hao wenye matatizo ya aina hii, Waheshimiwa Wajumbe wakija kwenu ninakuombeni ama muje

nao au waelekezeni waje kwenye ofisi zetu, na usione shida nipigie simu kwamba kuna mtu anakuja mimi nitamsikiliza.

Mimi nimesema kwenye kitabu changu nimepokea karibu wageni 2900. Jamani nina kazi nyingi za kufanya lakini ninafika hatua mpaka wageni 2900 ziara wilayani nimefanya nyingi tu, nimekwenda kutembelea *SACCOS* mbali mbali, sidharau popote ambapo ninaitwa ninakwenda kwa sababu ndio kazi zenyewe. Wananchi wametupa ridhaa yao tuwatumikie na kuwatumikia ndio huko.

Kwa hivyo naomba sana suala la mikataba ni tatizo tunaelewa na mimi ninaelewa. Mimi ninalikubali lakini bado tunaomba sana bado kwamba ninahitajia muda kulifanyia kazi. Ninashukuru sana mimi kama kuna kasoro zimejitokeza na moja ambayo Mhe. Jussa alilizungumza ilinigusa sana mimi.

Imenigusa kwa sababu katia neno kidogo pale ambalo kwangu mimi ni sumu. Alisema kwamba baadhi ya wafanyakazi wanaofanya kazi mahotelini wanaopata migogoro ya kazi wakija pale na katumia neno ajiangalie Waziri na watendaji wake. Jee, hakuna kidalili cha rushwa rushwa hapa?

Mimi nimefanya kazi miaka mingi alhamdullah. Siku moja kuna mtu mmoja aliniambia wewe utakufa maskini. Miradi yote ya Wizara ya Elimu hapo mpaka leo upo hivyo tu hata nyumba umekaa miaka kumi hujaimaliza. Mimi ninakwenda kuzikwa kwenye shubiri moja na leo nina swaumu Mhe. Naibu Spika, maisha yangu sijawahi kuomba kitu kama hicho katika maisha na wala sikiombi.

Lakini kama watendaji wangu wamehusika Mhe. Naibu Spika, ninamwambia Mhe. Jussa aje aniambie. Kama ni mteuliwa wa Rais nitamuandikia Rais kwamba huyu hanifai, kama ni afisa wangu tu yupo chini ya mamlaka yangu, kesho atakuwa keshapumzika kazi huyo. Kwa sababu suala la rushwa hatutaki na pale kwenye Wizara yangu nimebandika pale, wanaita rushwa *free zone* ile hakuna. Lakini kama ipo binadamu hajakamilika.

Nilipokuwa Waziri wa Michezo niliulizwa kuna ishara ya rushwa kwenye michezo, nikasema mimi sijawahi kuisikia. Marifarii kama wanapewa wao wenyewe wanajuana ndani, mimi nikasema sijui lakini mimi sitokaribisha masuala kama hayo. *I want to remain clean*, nimalize muda wangu wa uongozi nikiwa safi na hata wakati ule nilipogombania uongozi wa Rais Mhe. Naibu Spika, kama ningekuwa na madoa haya ya rushwa magazeti yangeniandika. Mbona hayakuniandika na mpaka leo nipo hapa *alhamdulillah*.

Hata Imamu Msikitini anasema, *"ninakuusieni na kuiusia nafsi yangu"*. Kwa hivyo ninajiusia kwanza mimi mwenyewe kuwa nijiangalie mimi mwenyewe, kama kuna kasoro za kibinadamu zipo lakini suala kama hili tupo *very careful*. Kama kuna mfanyakazi kapata tatizo kama hilo kaja pale, halafu ofisa wangu anamwambia meneja wa hoteli, huyo kaja mchukulie hatua fulani, *that's very bad* na halikubaliki.

Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, hata waje waninong'oneze tu kama huyo ofisa wako au kijana aliyekwenda huko akaletwa, halafu zikapelekwa taarifa huko, niletee. Mimi ninacheka sana na kufurahi sana, nina mashirikiano mazuri katika suala la haki za mtu hakuna matatizo. Kwa hivyo

Mhe. Jussa hili ninakuomba sana, kwanza ninakuhakikishia kwamba wizara yangu siwezi kusema ni *hundred percent* lakini *ninety nine percent*, ninaiacha *one percent*, ninasema sijui nitie kwenye *benefit of doubt* kidogo au vipi.

Lakini kwamba inawezekana kibinadamu mimi sikatai, lakini kwa pale mimi ninavyowajua wanajituma sana. Mhe. Makame Mshimba anakuja pale anamchukua Kamishna anamwambia twende hotelini, iwe saa nane au saa kumi, na yule bwana humwambia njoo kwangu mimi kwanza. Yeye anakata *short cut* anakwenda huko anamchukua Kamishna anakwenda naye. Anampiga vigongo vyake kule vizuri vya kumuelekeza lakini si vya kumpiga.

Kamishna anakuja ananijibu mimi. Tumekwenda kulikuwa na tatizo na wala sio tatizo hili, tayari hoteli ishachukua uamuzi huu na ule. Lakini mambo mengine yanahitajia subra. *Low season* kwenye mahoteli mambo mengi yanapunguzwa punguzwa kule na kipindi hiki kilichopita ilikuwa ndio *low season.* Sasa hivi hiyo *season* imeshaanza, mimi Mhe. Mshimba ninakuhakikishia kwamba mtu wake kuwa bado mambo yake hayajawa mazuri, ninakuhakikishia mambo yake yatakuwa mazuri wala usiwe na wasi wasi.

Kwa hivyo ninakuombeni sana tusafishe nyoyo zetu sote tuaminiane. Tumepewa majukumu, mimi nimekamata msahafu nikasema na hauna mchezo ule. Mwalimu wangu aliniambia siku moja mtu atakayeapa akasema wallahi au kwa kumtaja Mwenyezi Mungu halafu jambo lile kama kalifanya au kama kaja akalifanya wanasema basi akisafiri baharini atakuja kuzama. Sasa sijui mimi niliambiwa hivyo. Ni jambo baya kuja kula kiapo halafu usikiteketeze kile ambacho umekifanya.

Nakuombeni sana mutuamini. Serikali hii ya awamu ya saba yenye mfumo wa serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni serikali makini. Nyote ninasema jamani ninasema sisi ni wamoja. Tushirikiane, Mhe. Rashid Seif huyo katiririka huko kakaa huku mbele sasa.

Heshi kuniuliza maswali wakati fulani ilipokuwa elimu kila siku mpaka juzi anaagaaga tena na fanicha za skuli. Lakini sio kwamba alikuwa anatuonea, ametusaidia. Mbona leo tumefika mahali Wizara ya Elimu imeshawekwa bajeti maalum kwa ajili ya mambo ya madeski na mambo mengine.

Vifaa vya maabara tumekwenda tumehangaika, vimepatikana vifaa vya maabara, keshokutwa skuli Mhe. Waziri atazifungua na vifaa vya maabara viko ndani. Mimi sina mashaka na hilo yatafanyika. Kwa hivyo tuaminini, serikali hii ni makini, Dr. Shein ni makini, Makamo wa Kwanza ni makini, Makamo wa Pili ni makini na Mawaziri wote ni makini na mimi nimo humo (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninadhani nimezungumza vya kutosha kuhusu suala la mikataba, ni matarajio yangu kwamba inshaallah wamenifahamu vizuri na tuendelee kushirikiana zaidi, pale ambapo watahitajia maelezo zaidi sitokuwa na matatizo ya kuwajibu.

Lakini pia suala zima la mikataba ya muda mfupi ya miaka miwili miwili au miezi sita sita, nayo inakera. Anatoka hoteli moja miaka miwili anakwenda hoteli nyengine miaka miwili, ile miaka

miwili aliyofanya kazi haina maana yoyote pale halipwi chochote. Hili nalo halikubaliki vile vile.

Tayari tutatengeneza kanuni zetu kwa utaratibu wetu kwa suala kama hili ili tuingize na vipengele hivyo kwamba mfanyakazi yeyote anapofanya kazi hata kama siku tatu, nne imetokea dharura basi zile siku zake zihesabiwe ili ziingizwe apate *benefit* zake, hatuwezi kumnyima kwa sababu yule ni binadamu na yeye anataka haki zake vile vile. Anahangaika huku kwenda hoteli nyengine sio kwa sababu anapenda, anaona kule kuna maslahi mazuri zaidi.

Sasa huku alikotumika miaka miwili basi unashindwa kumpatia haki yake, haiwezekani na hilo tutaliangalia vizuri inshaaallah kama nilivyosema hatutokuwa tayari kusema kuona vijana wetu wanapata matatizo.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamezungumzia ajira za wazalendo kidogo mahotelini. Mimi nilifanya utafiti jana wala hatukumtuma mtoto mdogo dukani. Tumefanya *direct contact* na mameneja wenyewe. Naomba nitoe takwimu hizi *samples* za hoteli tatu au nne tumefanya.

Tumekwenda kwenye hoteli moja mutanisamehe itabidi niitaje ni Tembo Hotel. Wazanzibari wanaofanya kazi katika hoteli ile ni 72, na bahati nzuri huyu ni mwekezaji wa kizalendo, yeye mwenyewe na 5 ndio wageni. Serena ndio mutaona ile *difference*. Hii hoteli *owner* ni Aga Khan tunamjua ndio *network* yao, 81 ni Wazanzibari 82 ni wageni. Kwa hivyo hapa *almost* ni *fifty fifty*.

Lakini *nature* ya hoteli ile wameifanya vile, sasa hivi jana nikawaambia mikataba inayomalizika kwa hizi kazi ambazo zinazoweza kufanywa na Wazanzibari, mikataba hiyo basi na tutawatia Wazanzibari watakwenda kufanya kazi hizo.

Grand Palace mwekezaji ni mzalendo, 38 ni Wazanzibari na 7 wageni. Kiwengwa ni hoteli ya mgeni kule, 125 Wazanzibari na 35 ni wageni. Kiwengwa Beach Hotel 96 ni Wazanzibari na 42 ni wageni. Kwa hivyo juhudi zimefanywa jamani, hali haikuwa hivi na hizi *figures* zipo zifuatiliwe na kama munataka *aunthentic* ile barua yenyewe hasa ambayo tumeletewa nitakuonesheni nitakupeni kuhakikisha jambo hilo.

Lakini tukubali bado kuna maeneo ambayo yanahitajia tupeleke vijana wetu. Lakini na moja tulikubali. Mimi alikuja mwekezaji wa mpira (*rubber*) kule Pemba, anasema mimi wafanyakazi ninawalipa kwa siku, nikiwalipa kwa mwezi nitakula hasara kwa sababu kila siku na orodha kaniletea na kweli ipo orodha, anakwenda siku mbili, siku ya tatu anapeleka habari kwamba amefiliwa na babu yake, anakwenda mpaka amefiliwa na jirani wa babu au jirani wa rafiki yangu. Katika mwezi siku nne, tano, sita au saba hendi, nani atakuajiri mtu kama huyo au kumpa pesa kama hizo. Tuwe *fair* kama hili.

Anasema mimi nipo tayari kwanza mimi ninawalipa zaidi ya kiwango ambacho umetangaza Waziri, lakini tatizo vijana hawa *excuse* zimekuwa nyingi. Sasa mtu yeyote anayeanzisha mradi anataka apate watu vijana wa kumsaidia na yeye apate faida. Kaniambia mimi kwa mfano yule wa Residence, ananiambia mimi ninawalipa zaidi ya *one forty five thousand*s, mimi ninawalipa zaidi ya laki tatu wafanyakazi wangu pale. Lakini *discipline* nimeeka mbele, hakuna mtu

ninamkata mshahara wake na anapofanya uzembe sisi hatuna muhali. Kasema Mhe. Mshimba yule aliyemdhalilisha mtoto tumemfukuzia mbali kaondoka. Mtoto kapewa chochote pale ninadhani milioni tatu au sijui shilingi ngapi kapewa si haba yamekwisha.

Kule *La gemma* hoteli jeuri imefanyika kule. Kuna wafanyakazi fulani wamekwenda yule jamaa ana mbwa wake akamuachia na munakumbuka nyinyi waheshimiwa muliokwenda. Mama yule keshaondoka nchini hayupo. Neptune kuna meneja wa sehemu ya jikoni alipewa dhamana, alianza kuwafanyia mambo yasiyo ya kawaida wale wafanyakazi, ikaripotiwa. Hayupo hapa nchini ameshaondoka.

Sasa yale ambayo yanafika kwetu sisi tutayachukulia hatua. Mengine ninawaomba wananchi popote pale walipo wakiwa na matatizo, munayo haki ya kutuleteeni nyinyi Waheshimiwa, na nyinyi mukiyapata tuleteeni na kama wao wanaweza kuja, ninatoa wito waje moja kwa moja sisi hayo tutayapokea.

Ni kweli nimezungumza suala zima la wafanyakazi wazalendo, jamani tunajitahidi. Lakini na sisi lazima tu-*change attitude* yetu ya kazi vile vile. Baadhi ya vijana ukiwaambia nendeni kafanyeni kazi ya kutandika vitanda mahoteli, ndio nafasi iliyokuwepo vyumbani kule Mheshimiwa kazi hii anaifahamu alikuwepo kule hoteli, anakwambia mimi changu kinanishinda kutandika nikatandike huko, utamfanyaje mtu kama huyo.

Kafanye kazi ya bustani, unatakiwa ufike kazini saa moja anakwenda saa mbili au tatu, kazi zitakwenda? Lakini pamoja na hayo yote bado tutalisimamia suala hili. Mimi ninataka nikimaliza kipindi changu cha Waziri wa Kazi basi kwa asilimia zaidi ya 60, 70 au 80 katika maeneo yote ya vijana wa Kizanzibari wanafanya kazi. Kwa sababu na utaalamu tunauhitajia. Hatuwezi kuwa sisi kila kitu tunacho na utaalamu tunahitajia na ujumbe ndio huo. Ninazungumza hapa nina hakika wananisikiliza huko mahotelini na maeneo mengine, kwamba ninasema kwamba Wazanzibari kadri itakavyowezekana wajitokeze waje kujiripoti kwenye kituo chetu cha mambo ya ajira na inshaallah tutafanya kila liwezekanalo tutawasaidia wapate ajira hizo. Lakini inapotokezea tatizo wasichelewe kuja kwetu sisi tutawasaidia.

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa suala jengine la mikopo. Wengi sana wamezungumza kuhusu suala hili la mikopo ya AK, JK na mfuko wa kujitegemea. Mhe. Asaa kasema na mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa kasema, alisema pesa anazopewa Maalim Haroun ni kidogo.

Hebu tujikumbushe kwa msanii maarufu wa Makunduchi tena nimeshatoa mara nyingi, anaitwa Mzee Mudu. Kwenye uzazi wa mpangilio analalamika mama watoto, ana watoto wengi hawahudumii, yeye hana uzazi wa mpangilio, uzazi wake wa mpangilio alipoulizwa akasema wa kwanza huyu, wa pili, wa tatu, wa nne huyu wanaendelea mpaka kumi.

Akaambiwa wewe hata sabuni unashindwa kuleta hapa nyumbani, anaambiwa na mama watoto, sisemi mimi, kwenye televisheni hiyo, unashindwa kuleta hata sabuni, akamwambia sabuni ninaleta lakini sema ni kidogo tu, sio kama hapeleki lakini anapeleka kwa mujibu wa uwezo wake, na alisema kwa Kimakunduchi akamwambia hivi, Mhe. Naibu Spika, uniruhusu nizungumze Kimakunduchi kidogo, “Sabuni ninakuletea mama heya sema haba”, na sisi pesa tunapata lakini hazitoshi, tunapewa kweli tunashukuru.

Lakini hebu tutizame mwaka jana *capital* ya wizara yangu nzima ilikuwa ni *only ninety millions* kwenye vyama vya ushirika. Mwaka huu kwa makusudi kabisa Dk. Shein kwa kujua umuhimu wa suala hili kwenye sekta hasa ya kusaidia mikopo kwa vijana *one point one billion* kazitoa.

Zitawaendelea wale wanaotaka kufuga watasaidiwa, wanaotaka kuja kwenye uvuvi tutawapa na boti tutawanunulia tukijaaliwa. Kwenye mambo ya ufugaji tutawapelekea kwa kushirikiana na wizara inayohusika. Kama hayo hayatoshi Dk. Shein ameanzisha mfuko wa uwezeshaji, mimi ndiye mwenyewe.

Hivi sasa ninavyozungumza na kwenye *budget speech* hatukuficha tumezitia. Tayari karibu milioni sita tushazikusanya, lengo letu angalau tukusanye bilioni tatu tuongeze na mfuko wetu tukae na mkao wa kuondokana na umaskini, mimi ninakwambieni. Umaskini Zanzibar siku si nyingi itakuwa ni historia lakini lazima sote tushikamane tushirikiane, kwa pamoja nina hakika mambo haya tunaweza tukayafanya, mukimuachia tu maalum Haroun peke yake na watendaji wake au tukimuachia Dk. Shein peke yake mambo hayawezi kwenda hivyo, sote tuna jukumu la kufanya hivyo.

Mimi ninashukuru sana Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge na wengineo wanasaidia sana vikundi mbali mbali vya ushirika. Lakini tujitahidi kuwasaidia mfululizo, tusingojee pale mambo yanakaribia karibia ndio tunaanza kusaidia. Kwa sababu mimi juzi nilikwenda Mkwajuni kuna *SACCOS* pale benki imeanzishwa, ninashukuru ninampongeza Mhe. Mwakilishi na watendaji wake waliokuwepo, uongozi wa Sheha ulikuwepo pale, Diwani alikuwepo na ninashukuru Mhe. Panya alikuja baadae alikuwa na dharura.

Mimi ninapenda nikikuoneni nyinyi japo sinenepi ndio mwili wangu na bora nisinenepe nisije kuambiwa mengine tena. Lakini tumezindua *SACCOS* benki pale *CRDB* wametusaidia. Sasa benki zipo tayari, PBZ wapo tayari, *CRDB* wapo tayari na wengine wapo tayari. Lakini na mfuko wa AK na JK tukubali ulikosewa utaratibu. Ilikuwa upitie kwa Sheha na upitie wapi, sasa kuna taarifa na wasi wasi uliokuwepo kwamba baadhi ya Masheha waliwapa watu wao wa karibu zaidi.

Tukasema kuanzia sasa na bajeti hii mutaona maombi yote yanakuja wizarani moja kwa moja na sisi tunayapeleka moja kwa moja katika idara inayohusika na mikopo ndio itakayokuwa dhamana wa kutoa mikopo. Hata *PBZ* tumeshakubaliana kwa kiutaratibu na kimsingi kwamba zile pesa za AK na JK ambazo wanazisimamia wao, sasa zitasimamiwa na wizara yetu moja kwa moja katika suala zima la utoaji mikopo.

Lakini pia kilichowavunja moyo watu wetu kwa sababu mkopo wa JK na AK ulikwenda zaidi kwa watu binafsi au kwa vikundi binafsi au kwa watu wachache. Riba ilikuwa kubwa na hii inawaumiza na hali ya Zanzibar na suala la riba tunalijua tatizo lake. Tunajaribu karibu itawezekana kutumia *system* za Islamic Bank hizi, lakini pia tutumie utaratibu ambao tutajaribu kuziondosha zile riba, lakini tutoe mikopo lakini tupate pesa kwa njia nyengine ambayo haitokuwa riba. Sitaki kuyasema hapa kwa sababu ni nyeti kidogo, bado hayajaiva hayo, yakiiva nitakuja kukwambieni.

Lakini tunafanya utaratibu kwamba mikopo tuitoe, iwe kama itakuwepo basi iwe ni ndogo sana na pengine tunataka hasa kuiondosha kwa sababu huwezi kumkopesha mtu shilingi laki moja unamwambie baada ya miezi kumi aje akulipe kila mwezi elfu kumi kwa kufanya mradi wa maandazi. Akitoka kule Mkwajuni au Makunduchi, Chokocho akija afisi kuu pale anakuja kulipa shilingi elfu kumi wakati nauli yake ni elfu nne, kaja mjini asinunue mikate, atanunua hata kama kule inapatikana shamba, mkate wa mjini ni mtamu ati.

Anaondoka anatumia shilingi kumi na tano, miezi kumi huyu atatumia laki moja na hamsini na pengine huyu alikuwa alipe laki moja na ishirini. Hapa pana tatizo. Kwa hivyo tunajaribu hivi sasa ku-*central* mambo. Kwa hivyo mfuko huu wa uwezeshaji uliokuwa na milioni mia sita, mfuko wa kujitegemea unaendelea na mfuko wa AK na JK. Lakini ninakuhakikishieni bado tunatafuta pesa sehemu mbali mbali nje na ndani ya nchi mpaka tuhakikishe kile kiwango ambacho tulichokusudia cha bilioni tatu kinafika, kama si mwaka huu, mwakani, kama si mwakani lakini tutafika kwa kuwasaidia vijana wetu.

Vijana nao ninawatoa wasi wasi. Serikali hii ipo makini, tunakujalini sana na ndio maana Dr. Shein akaweka kifungu maalum akakiweka kwenye wizara hii, akihakikisha kwamba vijana tunawapa fursa mbali mbali za kuweza kujiwezesha.

Mhe. Naibu Spika, tunajaribu karibu iwezekanavyo na sisi upande wetu tunaomba mashirikiano yenu katika kila hali ili tuweze kufikia kiwango ambacho tumekusudia.

Vyama vya ushirika vimekufa. Nilisema hapa mwaka jana vyama vya ushirika vingi vipo *ICU*, taaban, vyengine vimeshazikwa, katika vile elfu tano vya wilaya mbili, elfu moja mia sita musifikirie vyote vizima vile, vinachechemea. Ni vichache vinavyofanya kazi na Waheshimiwa munavijua.

Tumeanzisha programu maalum za mafunzo, na safari hii Idara ya Ushirika tumewapa *thirty millions* kwa ajili ya mambo ya mafunzo tu hayo. Mkurugenzi wangu wa ushirika anafanya kazi uzuri, anajulikana kote huko, akifika tu bwana ushirika. Sasa tushirikiane kwa pamoja, wanapokuja kufanya ziara ya mafunzo huko. Mimi namshukuru sana Mhe. Ali Juma Shamuhuna, namshukuru sana Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Fatma Mbarouk Said na waheshimiwa wengine, mmeshiriki kikamilifu katika mafunzo ambayo tumeyaandaa kwa ajili ya vijana wetu, nawashukuruni sana.

Pia Donge nimeshatia kwenye bajeti *speech* yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Tunakufungulia *SACCOS* benki kule, tukimaliza Ramadhani yale mambo tuyamalize kuyakamilisha ili tuanze kutayari *SACCOS* benki moja Donge, tumesema Matemwe na maeneo mengine tutazifungua. Hivi sasa tunazo 14, tunataka zifike 25 tukijaaliwa mpaka mwaka huu ukimalizika na tutafika hatua hiyo.

Mikopo binafsi inanufaisha Unguja na Pemba, kuna watu wanalalamika mbona mimi watu wangu hawajapata mikopo. Hawajakuambia tu, lakini wamepata. Akikuambia wewe hutomsaidia tena. Kwa hivyo, takwimu ninazo lakini muda hauruhusu Mhe. Naibu Spika, nadhani nimeshatumia karibu dakika 50 kwa ajili ya masuala haya, naomba niendelee na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema, kuna mjumbe mmoja aliuliza. Je, waziri umetumia kiasi gani kwenda safari zako za nje. Hesabu itanishinda maana yake kila siku mimi ninasafiri kwenda nje. Akauliza tena, je, faida gani umetuletea. Ndio yale mambo ya mikataba ambayo ninahangaikia vijana wetu Wazanzibari, sio haya tu na misaada tunaipata. Hao *ILO* tukikutana huko Geneva, ndio ile misaada ambayo tunaipata, watatoa karibu milioni 300 au dola kama laki tatu, 300,000 katika kusaidia miradi yetu mbali mbali. Ninachotumia kinakuwa kidogo kuliko tunachokipata.

Mhe. Saidi Ali Mbarouk wakati nikiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ali-*comment* wakati alipokuwa *backbencher*. Alisema ingekuwa mtu mwengine ningehoji, lakini bahati nzuri anasafiri sana Maalim Haroun, lakini kila anaposafiri akija anachokileta kinaonekana. na mimi nakuhakikishieni kwamba tunapata faida nyingi. Lakini sio lazima kwamba ukenda kule upate pesa, ukenda kujifunza tu peke yake si dogo.

Mhe. Hamza Hassan Juma kenda Rwanda leo huna vya kumwambia kwa mambo ya Rwanda huyo. Kwa hivyo, tumetumia pesa kweli na ndio maana yake bajeti safari hii, ile bajeti iliyotoka milioni 24 imekwenda mpaka milioni 84 kwenye posho maalum. Tumekwenda kwenye kifungu kile cha idara ya uendeshaji pale 84. Tiketi ambayo anasafiri waziri ya daraja la kwanza karibu dola 5,000 anakaa Geneva pengine siku 10 au 15 anakwenda yeye, anakwenda Katibu Mkuu na wale *ZATU* na *ZANEMA* wote tuwalipie sisi kwa mujibu wa utaratibu wa Shirika la Kazi Duniani. Tunashindwa, mwaka jana hatukuwachukua na mwaka huu tumewachukua. Imebidi tuhaulishe pesa kwa ajili ya ku *accommodate* ndio utatu wenyewe. Jamani usafiri unatugharimu pesa nyingi, hali tunaijua ya fedha zetu zilivyo, lakini tunamshukuru Mhe. Rais wetu anaturuhusu tunakwenda na Dk. Shein hawezi kuruhusu tu kama huna pesa ambazo umetenga kwa ajili ya bajeti ile na mawaziri pamoja na mamlaka tulizokuwa nayo ya kuhaulisha vifungu, lazima tuwatake ushauri wenzetu wa wizara ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, kama kungekuwa kuna uwezekano Mhe. Ismail Jussa alipokuwa anasema, kuwa zile pesa za wizara nyengine basi kama kuna uwezekano watakapo punguziwa kama hawana pakuzipeleka basi waniletee kwenye mfuko wangu wa uwezeshaji nitashukuru sana, kwa sababu nitapata njia ya kuwakopesha wananchi wengi zaidi. Lakini kama wanazo njia za kuzipeleka huko huko bora waziache tusije tukatafuta ugomvi mwengine.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, waliokuwa nje waingie ndani tunataka kupitisha vifungu. Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Naibu Spika, kuna wajumbe waliuliza wizara hii na misaada ya wanafunzi inakuwaje. Mhe. Naibu Spika, wanafunzi hawa katika kila idara wapo ni wale ambao wako masomoni wanasoma, inabidi tuwalipie usafiri wao, tuwalipi *per diem* zao, wanakwenda kule na *Alhamdulillah* kwenye kitabu chetu utaona wanafunzi ambao wamekwenda masomoni sio kidogo na wengine wanaendelea. Kwa hivyo, msaada wa wanafunzi sio kama tunawapa msaada tu hivi hivi, lakini wale wafanyakazi wa serikali ambao wako masomoni na wanaendelea masomoni. Kwa hivyo, nadhani jibu lake sahihi itakuwa ni hilo.

Mhe. Naibu Spika, labda kwa haraka niingie kwenye vifungu nitowe ufafanuzi wa hapa na pale. Lakini kabla ya hilo kuna *Sunday market.* Mhe. Marina nakushukuru sana mchango wako ni mzuri, tunahitaji kuitangaza zaidi *Sunday market*. Kuna watu wanabeza beza bado aah!, lakini tunajitahidi. Lakini kweli tutajitahidi kuitangazia ili iweze kufanyakazi vizuri. *Sunday market* ni mahali ambapo wanaweza kwenda watu wetu wakafanya biashara nzuri tu. Natoa wito kwa wajasiriamali wote wajitokeze kwenda kufanyabiashara zao pale *Inshaallah*.

Kuhusu *private office* kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliuliza hapa kwamba hii *private office* mbona haina bajeti. Ofisi hii iko chini ya Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi, lakini ime *centralize* pale kuna mambo ya muhimu ya kimsingi ya huduma kila wakati, sina haja ya kumwita Mkurugenzi, anakuwepo msaidizi wangu pale na kitengo changu cha mawasiliano kiko pale, kwa hivyo inakuwa rahisi. Lakini hakuna bajeti ambayo waziri kawekewa pale. Bajeti ya waziri iko kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi, safari zake, maposho mengine, mishahara yake yote inatoka pale pale.

Mhe. Naibu Spika, kazi njenje. Mhe. Kazija Khamis Kona hayupo. Sasa sijui namjibu nani, nisije nikajibu hapa yeye hayupo halafu nikajakupata mtihani mwengine wa kugongewa miguu. Kwa hivyo, kazi njenje kwa faida ya wengine tu. Tumeandaa vijana 32 mheshimiwa, hawa ni vijana ambao ni *graduate*, wamemaliza *University* na wachache wana *diploma* katika hawa tumewa-*train* namna ya kujifundisha kupenda kazi, wasichaguwe kazi. Lakini pia njia gani ambayo unaweza ukam-*convince* mwenzako na ukamshauri akaweza kujua mradi gani afanye na mradi gani asifanye ambao utakuwa na tija.

Mhe. Naibu Spika, tumeandaa vijana 32 ambao tayari tumeshawasambaza katika kila wilaya. Katika hizo wilaya kila kijana mmoja tumempa jukumu la kuwaandaa vijana 200. 200 mara 32 utakuta ni sawa na 6,400. Katika kipindi cha mwaka mmoja vijana 6,400 watakuwa na taaluma ya kujiajiri au kuajiri wenzao. na hao vijana 6,400 na wao watapewa jukumu kama hilo la kuwa *train* vijana 100 au 200 vile vile, haja yetu kila Mzanzibari mwenye uwezo wa kufanyakazi awe na taaluma ya kufanyakazi kabla hajapata mradi wowote au hajapewa pesa za kufanyakazi. Ukishapata mafunzo yale sasa ndio pale ambapo tunakuwezesha. Wewe una *interest* gani. Watu wa uvuvi pwani kule uvuvi, sawa. Watu wa maweni kilimo, sawa. Watu wa mijini kule biashara, watu wa shamba kule kuna wafugaji wa kuku, ng'ombe na mbuzi. Sasa ndio zile pesa ambazo zimewekwa 1.1 bilioni, pamoja na hizi milioni 600. Sasa tunavi-*establish* vikundi vya ushirika huko kwenye majimbo yenu na nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu, kama tutakuwa na bilioni moja, basi nitazigawa kwa majimbo 50 sawa sawa ili kila eneo wapate sawa sawa pesa zile ziwahudumie wananchi wao.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nataka nijibu na lile suala la Mhe. Ashura Sharif Ali. Kuna kiharufu cha mambo ya upendeleo wa kisiasa. Hee! Sasa hivi tena. Mimi tokea niko elimu pale mpaka nimemaliza. Sikuwahi kumfukuza mwalimu hata mmoja kwa sababu ya kujiingiza katika mambo ya kisiasa. Zaidi ya hivyo, wale ambao walifukuzwa huko nyuma, nilitoa agizo nikafuta wote wale na nikawaambia warejeshwe wote kazini. Waheshimiwa wengine walikuwemo humu mwaka jana hawakurudi wakaingia kwenye uwakilishi mpaka leo wengine wamo, haya sina haja ya kuwataja. Lakini hatuwezi kuingiza siasa katika mambo haya. Sote kila mmoja ana imani yake na itikadi yake, kama na dini hivyo hivyo. Nikianza kubagua watu na mimi sinitakuja kubaguliwa, ni dhambi kubwa kumbagua mtu. Quran inasema sote tuko sawa sawa, yameumbwa

makabila na watu mbali mbali na rangi mbali mbali, sio kwa sababu ya ubora. Mbora ni yule anayemcha Mwenyezi Mungu na ndio tunafunga sasa tumo katika kumcha Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, nawahakikishieni kwamba chembechembe za kisiasa haina nafasi katika Serikali ya Awamu ya Saba, haikuwa na nafasi huko nyuma na haitokuwa na nafasi kwa sababu sio jambo zuri. Mimi sisemi kitu. Siku moja jimboni kwangu nilimwambia kiongozi mmoja mkubwa wa Chama cha CUF, nilimwambia kweli. Nikamwambia mheshimiwa kule Makunduchi usimuweke mgombea, mimi nina wahudumia sawa sawa hawa. Akaniambia hapana, kwa demokrasia ni lazima nimuweke, kama sikumuweka tutakuja kufahamika vibaya. Nilikusudia kwamba hakuna suala la ubaguzi katika suala hili. Unapopeleka huduma ya maji au elimu huwezi kubagua kitu kama hiki ukasema hawa watumie na hawa wasitumie. Sina historia ya kitu hiki cha ubaguzi na sitofanya tukijaaliwa na mpaka nitakufa sitombagua mtu. Mimi nawaheshimu wote, wakubwa na wadogo *Alhamdulillah*. Mimi nawashukuru sana mmenipa nguvu kweli humu ndani jana na leo. Kila mmoja kasifia alivyosifia, sisemi kama, aaah! Basi, bora tuendelee.

Mhe. Naibu Spika, kazi njenje ndio hizo nimeshazieleza jamani vijana hao wanaandaliwa. Kuku hao wanaokuja Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa sababu mambo mengine mnanibebesha mimi sio yangu. Lakini nawaombeni *Inshaallah* tushirikianeni kwa pamoja sote twende vizuri katika suala hili.

Nakubali suala la viwanda ni *solution* kubwa, viwanda vidogo vidogo vitakuwa na ukombozi mkubwa sana hapa na vitasaidia kuhusu masuala ya ajira. Vijiji vya Mbuyu Tende na Ungi kule Msuka, hali ya umaskini katika maeneo haya tunayaelewa. Katika msaada mmoja tuliouanzisha katika eneo la Mbuyu Tende pale skuli, tunachimbisha kisima cha kuwasaidia wananchi wa pale wana tatizo la maji na tunaendelea tumefika hatua nzuri, karibu watapata maji yao *Inshaallah* na tumewaahidi tutawapelekea na jenereta mapaka hapo umeme utakapokuwa tayari.

Kuhusu kudhalilishwa wa wafanyakazi Mhe. Assa Othman Hamad, kweli. Ndio hao niliosema wengine tumeshawavukuza kazi hatukubali. Pia na wafanyakazi mahotelini nao wawe makini, wakafanye kazi ile ambayo wamepangiwa kwenye mkataba wakaifanye, wasifanye kazi za *extra curricular activities* hazina haja. Mimi nasema mtu akijiheshimu basi na yeye ataheshimiwa, tujitahidini. Mimi naamini wafanyakazi wetu Wazanzibari ni watu makini, wazuri na hata pale nilipopata shinikizo kwamba Zanzibar tuingie kwenye mashindano ya warembo. Mnakumbuka vizuri wengine. Nikasema Wazanzibari hakuna haja ya kuingia kwenye mashindano hayo, kwa sababu wote ni wazuri. Kwa hivyo, waendelee kufanya kazi vizuri wataheshimika na Mwenyezi Mungu atawajaalia *Inshaallah* watapata maslahi mazuri zaidi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye vifungu kwa haraka. Nadhani ufafanuzi huu utasaidia hata kwenye mambo ya vifungu. Pemba kulikuwa na kosa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeyakubali. Safari hii buku lile lina makosa mengi, hata zile *line item* zilizoandikwa, mfano mahali pameandikwa umeme kumbe pamekusudiwa mambo ya kompyuta kihamishwe kule kipelekwe kule pamefanyika makosa, lakini kwa bahati pesa ni zile zile.

Kwa mfano, hapa fungu la Pemba kutoka milioni 2,400,000 zimekwenda milioni 30,000,000. Ukweli umeme pale ni milioni 2,400,000 sawa sawa, lakini pesa hizi zitatumika katika maeneo mbali mbali. Kuna gharama za petroli ambazo ziko kwenye kifungu 220401 pana 20,000,000

pale ambazo zitatoka kwenye ile 30,000,000 milioni. Halafu kuna 220801 matengenezo ya zana, kuna 4,400,014. Halafu na ununuzi wa kompyuta ni milioni 6,000,000 kwenye 311207. Vifungu hivi vitatu kwa bahati mbaya havikupata pesa hizi. Kwa hivyo, pesa hizi zitaingizwa huku. Ni makosa ya kiutendaji yaliyotendeka kwenye Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Nadhani sasa umefika wakati Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, yale majina ya tabu lile wayaandike upya kwa mujibu wa hali halisi ilivyo, ambayo itatuondoshea usumbufu kwa mambo mengi sana.

Posho na kamati kwenye kifungu cha 211116 mipango. Kuna 12,000,000 milion tumefika 35,000,000 milioni. Mhe. Naibu Spika, kuna 3, 250,000 ni kwa ajili ya posho za idara ya uwezeshaji kwa wafanyakazi watakaowaleta mbali mbali kwenye vikao, hii ni wizara mpya. Tunahitaji kupata mafunzo kuwawezesha watu wetu. Huko wilayani tunashirikiana na Wakuu wa Wilaya katika suala zima la uwezeshaji, pamoja na vijana 32. Kwa hivyo, hawa wote wataingia kwenye programu na wengine ambao tutawashirikisha katika programu, hizi pesa sio nyingi hata kidogo, hizo shilingi milioni 3,000,000 nilizozitenga hapo.

Pia Mhe. Naibu Spika, kuna vikao vya kamati vya sekta mbali mbali mtambuka tunaita, kuna 3.250, yaani milioni 3200,000,000, kuna posho kwa ajili ya mikutano kwa wahusika mbali mbali katika kutathmini ufuatiliaji wa wizara, kuna milioni 2,700,000. Pesa hizi zote ukizijumlisha zinajieleza vizuri sana. Kwa wale ambao watahitajia ufafanuzi *document* inayo nitawapa *Inshaallah*. Kama kutakuwa na kasoro yoyote basi mimi nitakuwa tayari kwa ajili ya kukaa na kamati inayohusika ili tuweze kuweka sawa, lakini nakuhakikishia kuwa hakuna matatizo yoyote, tuko makini sana. Ukitizama wizara hii maeneo mengi sana pesa zake zimeongezeka kidogo kidogo, isipokuwa yale maeneo maalum. Lakini kuna maeneo mengine imeongezeka sana.

Kwa mfano, tunataka kununua gari, tumeweka usafiri imewekwa 50,000,000. Pale pana vespa, gari na kuna vifaa vyengine ambapo maelezo yake yako hapo. Mhe. Naibu Spika, kutokana na wakati labda itakapohitajika nitowe ufafanuzi zaidi, basi nitatowa ufafanuzi huo.

Mhe. Naibu Spika, kwenye idara hii ya usalama wa afya kazini tulikuwa na 2,000,000, tumeweka 12,000,000 milioni. Posho za wajumbe kwa vikao vinne, kamati ya usalama wa afya kazini milioni 1,400,000, posho kwa wajumbe kwa ajili kikao kutayarisha miongozi ya usalama wa afya shilingi 1,000,000 na hayo yanaendelea yote mpaka mwisho tunafika milioni 11,000,000 zinatumika Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Kazi tumetoka 7,000,000 milioni mpaka 11,000,000 milioni. Tulipata 7,000,000 milioni hizi sio kwa sababu ndio ambazo tulizitaka. Mimi niliomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanipatie 8 bilioni, lakini nilichokipata ni 1.5 bilioni. Sasa imebidi tukate kate. Mwaka huu kidogo tumeongezewa na sisi tumeongeza kidogo, kutoka 7,000,000 milioni kwenda 11,000,000 milioni nadhani hakuna tofauti kubwa kiasi hicho. Lakini pia hapa kuna suala zima la kupambana na suala la ajira za watoto na wamelizungumza wengi hapa, ninanikera Mhe. Makame Mshimba ameniambaia angalau basi ukemee.

Mhe. Naibu Spika, Mwalimu Nyerere tulipovamia na Iddi Amini, aliziambia nchi za Afrika kwamba angalau jamani mimi nimevamiwa, Tanzania tumevamiwa na Iddi Amini, akawaambia

angalau basi mkemeeni tu msitusaidie kwa vifaa vyovyote. Akasema hakuona kilichofanyika pale, matokeo yake akatangaza nia tunayo, sababu tunayo na uwezo tunao. Akatolewa Iddi Amini kule, watu wakaingia mpaka Kampala kule.

Kwa hivyo, nasema na sisi kwa ajira za watoto hizi Mhe. Naibu Spika, tutapambana nalo mpaka dakika za mwisho. Kwanza huwezi kumnyima elimu yake mtoto yule. Lakini tufahamiane ajira za watoto, kapewa mandazi na mama yake, dada yake anakwenda kuuza sokoni, zile sio ajira ambazo za kumtumikisha mtoto, zile ni za kusaidia familia tu. Ajira mbaya ni zipi, unawachukua watoto, kwa mfano pale Micheweni wanakwenda kuvunja kokoto. Unawachukua watoto wa darasa la tano au sita wanakwenda kuchukua mchanga ajira zile hazifai. Kwa hivyo, naomba tushirikiane, tawala za mikoa, manispaa, wakuu wa wilaya na sisi wawakilishi wote, ajira za watoto hizi hazikubaliki hasa zile ambazo hazina heshima ambazo zinamdhalilisha mtoto.
Kwa hivyo, kamisheni ya kazi hapa tumetoka kwenye 7,000,000 tumekwenda kwenye 11,000,000 milioni. Kuna bodi ile ya mishahara wana vikao vyao vya kawaida, kuna kamati ya utatu *tripartism* wanakwenda nayo na mambo mengine yanayohusiana na kama hayo. Mipango pale ilikuwa hakuna bajeti yoyote lakini tumeweka milioni 20,000,000 kwenye kifungu 220201 chakula na vinywaji. Maelezo yapo hapo yatakapohitajika nitayatoa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nadhani Waheshimiwa Wajumbe watakapotaka ufafanuzi wa moja kwa moja wa kila kifungu, nitakuwa tayari, kwa sababu nisipoteze muda hapa, halafu baadae yakahitajika tena. Mimi naomba nichukuwe nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kwa dhaati kabisa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. Nimejitahidi kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu amenijaalia kujieleza na nina mengi ya kuyaeleza mheshimiwa. Nilikuwa nina *documentary* yangu nilitaka niioneshe hapa, lakini kanuni haziniruhusu, ingejibu hoja nyingi za waheshimiwa ambao wameziuliza. Lakini Inshaallah ile semina ambayo wajumbe waliiomba ifanyike kule ile iliyobakia ya Mhe. Abubakar nitawaombeni japo kwa nusu saa munigaiye siku hiyo, ili niwaoneshe Waheshimiwa Wajumbe waone yale mambo ambayo tumeyapanga katika kipindi kinachokuja kwenye utekelezaji wa wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya yote hayo nawashukuru tena na kuwatakia waendelee kuichangia na kuihoji. Pia mkumbuke kwamba leo nina umri wa siku moja tu kwa hivyo, nihurumieni. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

## MUONGOZO

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Naibu Spika, kuna suala hapa limekuwa likijitokeza mara kwa mara naomba hebu leo mtusaidie tulielewe. Tuliomo ndani ya ukumbi ni chini ya nusu ya wajumbe wa Baraza hili. Kuna wakati mmoja niliwahi kulizungumza hili, nikanukuliwa katika kifungu cha katiba, lakini mpaka leo kinanipa shida hiki. Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, leo naomba unisaidie muongozo wako.

Mhe. Naibu Spika, katiba yetu kifungu cha 82(2), kinasema

Kifungu cha 82(2)

"Bila ya kuathiri masharti yaliomo katika kifungu cha 80 cha katiba hii, idadi ya wajumbe kufanya mkutano itakuwa nusu ya wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi".

Lakini halafu kifungu cha 83(1) hapo chini yake kinasema

Kifungu cha 83(1)

"Isipokuwa kama imeelezwa vyengine katika katiba hii, suala lolote au uwamuzi katika Baraza la Wawakilishi litaamuliwa kutoka na idadi kubwa ya wajumbe waliohudhuria kwenye kikao na kupiga kura".

Sasa kifungu cha juu kimetajwa mkutano na kifungu cha chini yake kimetaja kikao. Lakini kanuni zetu ukizisoma ambazo zimepata uhalali kutokana na katiba hii hii. Mfano kanuni ya 72(1) inasema

Kanuni ya 72(1)

"Kiwango cha vikao vyote vya Baraza vitakuwa ni nusu ya wajumbe wote".

Lakini fasili ya (2) inasema

Kanuni ya 72(2)

"mara kabla ya uwamuzi wowote kufanyika, ikiwa mjumbe yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali na Spika, wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote, basi kama Spika, atathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote, basi atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano na huku muhudumu kwa maelezo ya katibu akipiga kengele kwa vituo, yaani sio mfululizo".

Sasa Mhe. Naibu Spika, suala hili linatutanza kidogo, hebu naomba leo tusaidiwe na tupate muongozo wako, kwa sababu hili linahitahi muongozo wako Mhe. Naibu Spika. Kwa sababu inawezekana katiba imeandika mkutano, lakini kwa sababu ni maamuzi, inakusudiwa kwamba kila siku wakati wa kufanya maamuzi, na ndio taratibu za Mabunge mengine yote ya Mhe. Naibu Spika, kwamba wakati wa kufanya maamuzi ni lazima muwepo angalau nusu ya wajumbe.

Sasa tafsiri iliyotoka siku ile mimi inanipa mashaka kidogo kwamba tunataka kuambiwa hata tukiwepo 10 humu ndani, wakipiga kura 6 basi itakuwa maamuzi ya Baraza hili ni halali, mimi hii inanipa shida. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, sijui kama sasa hivi wanavyoingia mmoja mmoja tumetimia, lakini nilikuwa naomba hili tulisimamie sana Mhe. Naibu Spika, ili maamuzi yetu yawe halali, basi tunaweza kuhakikisha kwamba angalau nusu ya wajumbe wanakuwepo katika ukumbi. Naomba muongozo wako Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Katibu naomba uhesabu wajumbe halafu nitowe muongozo.
(*Hapa Waheshimiwa Wajumbe wanahesabiwa ili kujua idadi yao wote)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na kanuni yetu ni kwamba wajumbe wote waliomo ndani hawajatimia nusu ya idadi yetu, kwa mujibu wa kanuni tunaahirisha kikao

kwa muda wa dakika 5, ili Wanadhimu wakawatafute wajumbe waingie ndani, ili tumalize kazi iliyobakia.

*(Hapa Kikao kiliahirishwa kwa muda wa dakika 5 ili wajumbe wakamilike au wafike nusu ya wajumbe wote)*

*(Hapa baada ya dakika 5 Baraza lilirudia)*

**Mhe. Naibu Spika:** Katibu wahesabu wajumbe.

(*Hapa Wajumbe walihesabiwa ili kujua idadi yao wote)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, Baraza letu lina wajumbe 81 na sasa hivi tuko wajumbe 41. Kwa hivyo, tumefika nusu. Kwa hivyo, tunaendelea.

Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, wanyooshe mkono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA MATUMIZI

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, msitoke nje.

**FUNGU 27 – WIZARA YA KAZI UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMINA USHIRIKA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0801 | Kamisheni ya Kazi | 83,000,000 |
| Kifungu 1001 | Idara ya Ushirika | 10,000,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **93,000,000** |

**FUNGU 27 – WIZARA YA KAZI UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMINA USHIRIKA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0301 | Ofisi Kuu Pemba | 336,214,000 |
| Kifungu 0401 | | |

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina hoja za msingi nilizozichangia hapa, lakini hizo nitazishikia vifungu pahala pengine, lakini hapa naomba niseme jambo moja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa, nilikuwa mmoja wa watu ambao walikuwa wakizungumzia suala la sera kwa maana ya muundo wa serikali kwamba wizara mbili hizi, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, inafanyakazi ambazo zinazofanana sana na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu hoja zetu, alisema kwamba hayo masuala ameyasikia, lakini kimsingi yeye hana mamlaka na hayo, na yule mwenye mamlaka hasa ya kuyapokea haya Mhe. Mwenyekiti, tunasikitika sana Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi hayupo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kusema kwamba hili ni tatizo na tunakuomba tutumie fursa hii serikali ilipokee na sijui nani atamuambia. Lakini tunasikitishwa kwamba kwa muda mrefu tunapokaa hapa katika Kikao hichi Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi hatumuoni katika kikao hichi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii inatusikitisha sana Wajumbe wako, kwa sababu ili tupitishe vifungu maana yake hoja zetu zote zijibiwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni yetu katika masuala ya upitishaji vifungu Kanuni ya 98(6) (e) na (f) zinataka kwamba hoja ikiwa Mhe. Waziri amezijibu hatukutosheka, basi anyanyuke Kiongozi wa Shughuli za Serikali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tangu tumeanza vikao vyetu imekuwa kawaida, mara nyingi tukipitisha vifungu mbali ya majadiliano ya kawaida imekuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali hatumuoni.

Mhe. Mwenyekiti, hili linatupa tabu kwa sababu hata Katiba yetu, kwamba Katiba yetu kifungu cha 43(5) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

> Katiba ya Zanzibar kifungu cha 43(5) kinaeleza hivi:-
>
> > "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, nimeamua nisamehe hata vifungu vyangu katika idara hii na niliseme hili, kwamba linatusikitisha na ninakuomba Ofisi yako ichukue jukumu la kumwambia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, shughuli nyengine zote aziache kwa kawaida katika Vikao kama hivi dunia nzima katika utaratibu wa Mabaraza ya Kutunga Sheria, Mkuu wa Shughuli za Serikali hubakia ndani ya Baraza akasikiliza hoja za Wajumbe, ili yeye kama ndiye Mkuu wa Mawaziri katika Baraza hili achukue na kuyafikisha kwa Rais na wengine wanaohusika. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, kazi hiyo tutaifanya kwa niaba ya Baraza. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia sana ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu akielezea *concern* zake kuhusu kutowepo kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika Kikao hichi wakati huu.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais yuko Dar-es-Salaam kwa sababu ya kuhudhuria Siku ya Mashujaa, nyote mnajua jambo hilo na umuhimu wake, lakini wakati mwingi huwemo katika kikao chetu cha Baraza na anapoondoka huacha shughuli zake zisimamiwe na Waziri atakayemteua kwa sasa alimteua Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kusimamia shughuli za Makamo wa Pili wa Rais.

Kwa hivyo, haya yote anayoyasema yatafikishwa kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, ili yapelekwe kwa Mhe. Rais yale yanayohitaji kupelekwa kwa Mhe. Rais. Kwa maana hiyo, kila tunalolizungumza hapa tunali-*record* sawa sawa, ili kuliwasilisha kwa Mhe. Makamu wa Pili na utaratibu wa serikali uendelee katika mkondo wake na wala pasitokee matatizo katika utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba ijapokuwa Mhe. Makamu wa Pili hayupo, lakini ameacha dhamana hiyo isimamiwe na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mpaka pale atakaporudi, kwa sababu dharura ni dharura na hasa tukiangalia wakati tulionao huu wa majanga makubwa yaliyotokea na yako mambo mengi ya kushauriana. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, sikuwa na lazima ya kunyanyuka, lakini siridhiki na maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, tusitafute visingizio kwa mambo yaliyotokezea kwa dharura na ajali imetokezea juzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tangu tumeanza Baraza hili imekuwa ni kawaida kabisa na hili Wajumbe halitupendezi Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama nilivyosema imeshafika wakati hapa anatuambia majibu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba anaacha mtu.

Mhe. Mwenyekiti, imeshatokezea wakati hapa na wala hatusemi tu hapa, kwamba katika *bench* nzima ya mawaziri imeshatokezea siku tunapitisha vifungu hapa mawaziri wamebakishwa wawili na wala si utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Suala hili Mhe. Spika, ameshawahi kulikemea pale juu kuhusu mawaziri na tendo lililotokezea hapa halipendezi hata kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu tunalipwa na wananchi kwa ajili ya kufanyakazi hapa, katika kipindi hichi *priority* ya kwanza ya serikali ni shughuli za Baraza, kwa sababu hapa ndio katika mwaka mzima tunapokuja kujadili utendaji wa serikali Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akubali na achukue ujumbe huu na aufikishe kunakohusika, kwamba tabia hii irekebishwe haturidhiki Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, ahsante hoja imechukuliwa. Tunaendelea Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikapata maelezo ya ziada kwa Mhe. Waziri. Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi alioutoa hoja nyingi ambazo tulizozizungumza amezijibu kwa ufasaha na tunamshukuru sana kama alivyosema mwanzo alipofuatilia ile Mikataba ya *ZANTEL*, na ninaamini vijana wetu wamesikia kauli za Mhe. Waziri na ninaamini kwamba wataungana na kauli yake kuendelea kumfuata au kutufuata sisi kwa kuunganisha kwa Mhe. Waziri katika jitihada hizo za kuondoa matatizo hayo.

Sasa swali langu lipo hapa wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia zaidi katika kuangalia kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia bajeti anayotengewa Mhe. Waziri, kwa kweli bado haitoshelezi kuweza kuwawezesha wananchi wengi kiuchumi, pamoja na kwamba kuna mifuko hii na tunashukuru ameeleza kuwa kuna kama shilingi milioni 600 ambazo zinatoka kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na tunamshukuru kuendeleza mfuko huu.

Lakini kubwa zaidi ambazo nilipendekeza, ni vizuri tena ni busara kama tulivyopendekeza katika Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, pia wizara inayowawezesha, yaani iliyopewa jukumu la kuwawezesha wananchi, ambayo ni Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alieleza kwamba hivi sasa *SACCOS* hizi kuna taratibu ambazo tayari tumeshazungumza na Benki ya *CRDB* nafikiri na benki nyengine, kwa ajili ya kuviwezesha hivi vikundi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, ili aweze kunipatia ufafanuzi. Je, hivi sasa tumeridhika wananchi wetu wategemee wanapoleta maombi yako ya mikopo hasa kwa *SACCOS*, ambapo hata mimi *SACCOS* yangu ya Jimbo la Kwamtipura imeshapeleka maombi hayo.

Je, hivi sasa tutegemee kwamba tutaunganishwa hayo maombi kupelekwa katika Benki ya *CRDB*, na ule umuhimu wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana au Akinamama, sasa Mhe. Waziri anatuambia yeye mwenyewe anahisi umekuwa basi na tuzitegemee hizi benki ambazo ziliopo. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Mjumbe na kweli hili sikulitolea ufafanuzi. Wallahi sina mashaka na aliyoyasema na hiyo *SACCOS* yake ya Jimbo la Kwamtipura ninaijua ameshaniletea.

Kwa hivyo, nitafanya juhudi moja tukijaaliwa kwa kushirikiana na yeye Mhe. Mjumbe, kwamba tuandae siku tuje tuzungumze na Vyama vyake vyote vya Ushirika katika eneo lake na Benki ya *CRDB* tutakwenda nayo pale, kwa ajili ya kutoa maelekezo na mafunzo juu ya njia gani itumike mpaka wa-*qualify* kupata huo mkopo wenyewe. Kwa hiyo, hilo halina mashaka.

Lakini suala la Benki ya Vijana na Wanawake, sisi kwa upande wetu tumesema tutaanzisha Benki ya ushirika. Mhe. Mwenyekiti, benki zote hizi kwa kweli zinafanya kazi za aina moja na

nitashirikiana na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kuhakikisha kwamba ile Benki inayotaka kuanzishwa ya Wanawake, kwa sababu inahitaji *capital* na mpaka hivi sasa mwenzangu bado hajapata *capital*, lakini mimi tayari *capital* ninayo, yaani nimeshakuwa na zaidi ya shilingi milioni 500 na zitafika mpaka shilingi bilioni 1. *(Makofi)*

Kwa hivyo, benki hii kwa muda wa hapo tutakapokuwa tayari kuanzisha Benki ya Wanawake na wanawake wote watakaohitaji mikopo, vijana pamoja na wanaushirika wote watatumia hiyo Benki ya Ushirika, kwa lengo la kuwapatia njia rahisi ya kupata mikopo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi kwamba benki hii itaanzishwa na nimeshasema kwamba tutakwenda India, kwa ajili ya kujifunza, ambapo wenzetu wamefanikiwa sana katika kuanzisha benki kama hii katika suala zima la kuwakopesha wajasiriamali wadogo wadogo pamoja na vikundi mbali mbali vya ushirika. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri mimi huwa napenda nimsifu sana kwa jitihada zake na ninaamini wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura hivi sasa wataridhika na maneno ambayo ameyazungumza Mhe. Waziri.
Vile vile naomba Mhe. Waziri kwamba hii jitihada yake ya kuanzisha Benki ya Ushirika hiyo safari yake ya India, matatizo ya mawaziri wetu wenyeviti wenu hamuwachukui katika hizi ziara. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba Mwenyekiti wako wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ambayo iko chini ya wizara yako kwa sababu haya na wao wayaone. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe baada ya kwenda Pemba na Unguja hawana pengine wanapokwenda, sasa haya maendeleo mnapokwenda huko hamtakiwi muje muyaseme nyinyi mawaziri, isipokuwa wanatakiwa waje waseme hawa wenyeviti wenu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri hii ziara yake atakayokwenda si lazima India ni pahala popote anapofanya hizi jitihada za kutafuta hii misaada basi hawa ni mabalozi wako wenyeviti wako. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, tuendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tuendelee na ujumbe umefika.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0401 – | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 222,407,000/= |
| Kifungu 0501 – | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | |

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri ametupatia. Lakini wakati nilipokuwa nikichangia niliomba kupata ufafanuzi juu ya kitabu chetu hichi ambacho tulikuja kusomewa hapa katika malengo ya Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa *Program* ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mwaka 2011/2012.

Lakini bado sijapata ufafanuzi pamoja na maelekezo ambayo nilikuwa nimeomba kutoka kwa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anipatie.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, ufafanuzi zaidi.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, maelekezo pamoja na malengo yote tumeyaeleza kwenye kitabu chetu cha bajeti. Sasa nilisema pale kwamba muda hauniruhusu kwa kutoa ufafanuzi wa kila kitu na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ni mmoja katika wasomaji wazuri sana.

Kwa hivyo, nadhani angefungua kitabu kwenye malengo ya Idara ya Uwezeshaji, mambo yote yamewekwa bayana. Lakini kama atahitaji maelezo zaidi, basi namkaribisha ofisini kwangu na tutakaa kitako na kumuelekeza moja na jengine, ili aweze kufahamu vizuri zaidi.

Kwa kweli mimi sina mashaka akifungua ukurasa wa 28 pale nimeweka malengo ya Uendelezaji wa Utaratibu wa *Program* ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ukurasa wa 28 hadi 29 na sikuyasoma wakati nilipowasilisha bajeti na nilisema tu, kwamba angalia ukurasa wa 28 hadi 29. Kwa hivyo, ikiwa anahitaji maelezo zaidi kwa jambo lolote mimi niko tayari kumsaidia na yeye ni mwanafunzi wangu nitaendelea kumsomesha. *(Makofi)*

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, sawa tuendelee.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza niruhusu kwa sababu pale mwanzo nilizungumza suala la msingi la sera linalohusu Serikali Kuu nzima. Nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa hoja nyingi ambazo tumezitoa, tena ametoa maelezo ya kina katika vifungu vyetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo au labda niseme zaidi natoa angalizo, kwa sababu hivi sasa sitaki nimshughulishe mwalimu wangu.

Lakini nalisimamia hili katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwa sababu nilisema katika mchango wangu kwamba vifungu vingi vya matumizi Mhe. Mwenyekiti bado haviturudhishi, na Mhe. Waziri amejitahidi kutoa ufafanuzi. Kwa kweli nashukuru tokea jana ameshanipa mapema ile ambayo alikuwa akiisoma ili nijiridhishe.

Sasa nilichokigundua mimi Mhe. Mwenyekiti na hichi bado naendelea kuwaomba Mawaziri wote wakiangalie, kwamba bado inaonekana msisitizo mkubwa wa utendaji katika wizara zetu imekuwa ni semina na vikao. Kwa hivyo, kumbe hata yale mafungu ya viburudishaji tunayoyahoji ndani yake mna posho za chakula kwa ajili ya semina na vikao, kwenye posho maalum angalau tumepata maelezo imetenganisha na marupurupu ya wakubwa ya wizara.

Kwa maana hiyo, ukija katika fungu la Posho na Vikao pia ni kwa ajili ya vikao, na ndani yake umo usafiri wa ndani kwenda kwenye hivyo vikao, na kamati wakati pia kuna mafungu mengine ya usafiri ndani ya bajeti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ndipo ninaposema kwamba inatupa mashaka, kwamba inaonekana *priority* kubwa ya watendaji wetu katika shughuli zetu ni semina, vikao, makongamano, warsha. Lakini katika hili namshukuru Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kufuatia na ufafanuzi ndio umenisaidia kuyaona haya.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili hata katika Jamhuri ya Muungano kama unakumbuka limewahi kutolewa maelekezo na Mhe. Waziri Mkuu, kwamba hatuwezi kuwa na serikali ambayo shughuli zake kubwa katika bajeti ya kawaida ikawa vikao, posho, makongamano, warsha, semina.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema sitaki kupiga buti kwa ajili ya kuzuia fungu kwa sasa, lakini tumeshamwambia Mhe. Waziri wa Fedha lakini kwa bahati mbaya na yeye pia hayupo. Kwa hivyo, tunasisitiza tena kwa serikali kwamba kuna haja ya kuangalia tena, watapokaa na kuandaa huo Mpango wa Malengo ya Kati (*MTEF)*, ambao ndio unaotoa vipaumbele katika kupanga bajeti hii.

Nadhani sasa Mawaziri wasiwaachie watendaji peke yao, wanapaswa wajiridhishe na waone kama fedha hizi zinazopelekwa pale zinaleta tija katika nchi. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tunasema tatizo fedha katika bajeti ya wizara inaongezeka kwa jumla, kwa hiyo unaongeza *input*, lakini *output* kwa maana ya matarajio na matumaini ya wananchi waliokuwa nayo hayaonekani, kwa sababu fedha nyingi zinaingia katika vikao, warsha, makongamano, semina.

Sasa nilikuwa ninasema hili Waheshimiwa Mawaziri kwa jumla watizame katika wizara zao, ili tuone fedha hizi zinakwenda katika kuwahudumia wananchi zaidi. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kutoa angalizo hili kwa Mhe. Waziri na akinijibu kwamba nifuatilie na mimi sina tatizo nitamruhusu aendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri majibu na serikali imesikia.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa angalizo pamoja na indhari. Kwa kweli hii ni Wizara mpya kabisa Mhe. Mwenyekiti na imeanza mwaka jana tunatembea na wala hatujenda mbio.

Wizara hii imeanzisha idara mpya ya kwa mfano Idara ya Uwezeshaji, Idara ya Mikopo na ule utaratibu ule uliokuwa ukitumika huko nyuma sasa tumebadilisha pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, tutahitaji mikutano mingi kadri itakavyowezekana pamoja na wataalamu kutoka nje na serikali imekubali tutamuajiri mtaalamu kutoka Rwanda kwa ajili ya kusimamia mafunzo ya aina hii kumleta hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wanaomba Waheshimiwa Wajumbe kwa kipindi cha mwaka huu na pengine mwakani japo kwa nusu mwaka tutaendelea kutumia vikao vya semina, mikutano na mambo mengine kama hayo yanayohusiana na hayo.

Vile vile angalizo lake nalikubali kwamba hata mimi silipendelei kuwa mtu anakuja kwenye semina ikiwa analipwa au anapewa bahasha ama fedha kidogo. Lakini kuhusu suala la vinywaji, viburudishaji pamoja na chakula ndio utamaduni wetu wazanzibari takrima, pia nalo tutaliangalia ni kwa kiasi gani tunaweza kupunguza, ili kunusuru fedha hizi zikatumika kwa shughuli nyengine zaidi za kimaendeleo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimia Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 0501 – Idara ya Uendeshaji na Utumishi 844,681,000/=

Kifungu 0502 – Idara ya Mikopo

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niliomba na hili Mhe. Waziri nadhani atalikumbuka kwamba akija anisaidie maelezo makhsusi kuhusu hii Idara ya Mikopo. Mhe. Mwenyekiti, katika buku hili la matumizi fungu hili limeingizwa kama ni ruzuku na utaratibu wake umewekwa kama katika mashirika mengine au idara nyengine za serikali zinazojitegemea.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hii imeandikwa ni Idara ya Mikopo, na utaratibu wa idara tumezoea kwamba wote unakuwa na mchanganuo wake wa matumizi kama ilivyo idara nyengine zote, sasa hii imeitwa Idara ya Mikopo na utaratibu wake umewekwa kama vile taasisi zinazojitegemea kama vile bodi au mashirika ama mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, nilimuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo katika hili, kwamba kwa nini bajeti hii haikuwekwa mchanganuo wake kama zilivyo idara nyengine wakati hii ni idara kama zilivyo idara nyengine. Sasa hili katika majibu yake nadhani alighafilika hakuligusa na wala sikulisikia na nilikuwa nikimsikiliza kwa makini sana.

Kwa hivyo, naomba anisaidie majibu kuhusiana na suali hili, kwa nini Idara hii ya Mikopo imewekewa ruzuku badala ya kuwa na utaratibu wa kawaida wa mchanganuo wa matumizi kama zilivyo idara nyengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, majibu ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na napenda nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba ni kweli na mwaka jana aliliuliza. Lakini mwaka jana tuliweka makisio ya shilingi milioni 110 na safari hii ni shilingi milioni 288, bila ya shaka kuna mishahara ya wafanyakazi imeongezeka hapa.

Kwa hivyo, pamoja na fedha hizi kwa mwaka huu ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya ongezeko la mishahara mipya kwa wafanyakazi, ambapo jumla yake ni shilingi milioni 107,195,987,000/= na hiyo mishahara tu kwa ajili ya mishahara mipya kwa wafanyakazi. Vile vile shilingi milioni 10,719,598/= ni mchango ambao unaopelekwa *ZSSF*.

Kwa maana hiyo, katika hizo karibu shilingi milioni 117 zitakuwa zimetumika kwa ajili ya shughuli ya mishahara na *ZSSF* na zilizobakia ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa shughuli za wizara.

Mhe. Mwenyekiti, *point* yake naifahamu kwamba hii ni idara kama idara nyengine, lakini Wizara ya Fedha wametukubalia ni ombi maalum na walisema angalau watatuchukua kwa miaka miwili hivi sasa. Lakini kuanzia mwaka ujao itakuwa kama idara kamili kama zilivyo idara nyengine na tutaipangia utaratibu wa kuwa na bajeti yake, kwa sababu ina suala zima la kufuatilia ile mikopo ambayo ilitolewa na Benki ya *PBZ* kwa watu mbali mbali katika Mifuko ya AK na JK.

Kutokana na hali hiyo, ni lazima iwe inapata ruzuku kama ni idara tu shughuli kama hizi hatuwezi kuzifanyia bajeti yake peke yake. Kwa hiyo, tutajitahidi na hapa tumeweka ufafanuzi kidogo kwamba pia tunakusudia kununua gari mpya, kwa ajili ya kusaidia idara hii iweze kufuatilia hiyo mikopo huko iliko kwa sababu ni vijijini na shilingi milioni 50 nyengine zinaingia hapa.

Kwa hivyo, utaona kama zimebakia kama shilingi milioni 24 kwa ajili ya mafunzo pamoja na masuala mazima ya kuwahamasisha wananchi waweze kurejesha mikopo ile, kwa kweli tunahitaji taaluma ya kutosha Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu watu hawataki kulipa mikopo hii, hivyo tunahitaji kwenda na kurudi kila wakati na tutajitahidi kusimamia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana pamoja na hayo kuna suala zima la kununua samani, pia jengo lao ni bovu na Mwenyezi Mungu akitujaalia tukipata jengo zuri basi tutawaweka mahala pazuri. Lakini hivi sasa na mimi nimekwenda juzi kutembelea jengo lile na wala haliridhishi hata kidogo, hawana samani za kutosha pamoja na vifaa vya kutosha.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti Wizara ya Fedha wenyewe wakatuonea huruma na wakasema hapa tutatoa ruzuku kipindi cha mwaka jana na huu, na kuanzia mwakani mtaweza kujitegemea wenyewe *Inshaallah* kwa utaratibu wa kawaida.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo hayo na kwa ufafanuzi kwamba huu ni utaratibu wa muda tu na baadaye utarekebishwa, nashukuru na naomba tuendelee. Ahsante.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0502 – | Idara ya Mikopo | 288,000,000/= |
| Kifungu 0601 – | Idara ya Ajira | |

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilimuomba Mhe. Waziri pia wakati atakapokuja anitolee maelezo kuhusu ule mradi au *Project* iliyoanzishwa na Benki Kuu ya Tanzania *BOT*, ambayo ilikuwa imetaja benki maalum katika Jamhuri ya Muungano zilizotengewa fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa hawa wanaoitwa wajasiriamali. (*Small and Medium Enterprises – SME's*), ambayo ilikuwa ni kuwawezesha kufanya miradi ya ajira ya kujiajiri wao pamoja na wengine.

Katika hotuba yake Mhe. Waziri aliligusa hili katika maeneo ambayo yanatakiwa kusaidiwa kwa ajili ya kuzalisha ajira. Sasa najua kwamba tulimpa hoja nyingi Mhe. Waziri, kwa hiyo simlaumu kuwa baadhi ya mambo aliyaacha, lakini alituahidi kwamba haya tukiyasimamia kwenye vifungu atatupa maelezo.

Kwa hivyo, naomba anipe kauli yake tu Mhe. Waziri, angalau kwa sasa kuwa je, anao mpango wa kuwasiliana na Benki Kuu au zile benki ambazo ziliorodheshwa katika mpango ule, kusudi kwamba ile mikopo iliyokusudiwa kufika kwa ajili ya kusaidia kuzalisha ajira iweze kupatikana kwa hawa waliotaka kuanzisha ajira hapa Zanzibar; kupitia mpango huu wa *Small and Medium Enterprises*. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kwa Mhe. Waziri.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, maelezo ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba muda ulikuwa hauridhishi, lakini majibu yote ninayo na *Inshaallah* mikopo iliyokuwa ikitolewa na *BOT* wakati ule kwa *SME's* na hii *Credit Guarantee Scheme*, ambayo kwa kweli haisimamiwi na wizara yangu moja kwa moja ni suala ambalo linalosimamiwa na Wizara ya Fedha.

Kwa hivyo, huu ni mpango wa udhamini maalum ambapo mikopo kwa wafanyabiashara inatolewa. Lakini pamoja na hayo yote kwa sababu yana maslahi na wananchi wetu wa Zanzibar, tutashirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu, ili tukae pamoja tutazame uwezekano wa nini tufanye kwa ajili ya kuwasaidia wazanzibari nao wanufaike katika utaratibu huu.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri na nimhakikishie kwamba ule mradi niliomtajia katika mchango wangu wa kijana wa Mji Mkongwe ambaye amefanyakazi kubwa sana na akatimiza masharti yote, lakini utaratibu huu wa mkopo katika suala la ajira nitampelekea kwanza, ili aweze kunufaika katika jambo hili. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0601 – | Idara ya Ajira | 137,274,000/= |
| Kifungu 0701 – | Idara ya Usalama na Afya Kazini | 143,200,000/= |
| Kifungu 0801 – | Kamisheni ya Kazi | |

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri katika suala ambalo nilieleza kuhusu habari ya vijana wetu kule Kiwengwa wanavyofukuzwa ovyo ovyo, na kusema Mkurugenzi wake anafanya kazi kupitia *time* ambayo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuweka *hansard* yangu vizuri tu, kwa sababu nilisema sitounga mkono wakati ule. Kwa hivyo, sasa nasema naunga mkono kwa asilimia mia moja, tena naomba sana Mkurugenzi aendelee na uzi ule ule, na hao vijana waliofukuzwa kazi wa Kiwengwa, hivi nikiondoka hapa Mhe. Waziri nikisema uendelee basi naomba anipe jibu kama alivyokuwa akinipa majibu huko nyuma, kuniambia pahala fulani tayari wamesharudishwa watu kazini. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, nimeweka *hansard* yangu vizuri na sasa nimeunga mkono. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Kamisheni ya Kazi, hapa ndipo mchango wangu mkubwa katika wizara hii ulipojikita na Mhe Mwenyekiti nalo ni suala la vijana wetu wanaofanya kazi katika Kampuni ya *ZANTEL* na jinsi ambavyo mikataba yao ya kazi pamoja na masharti ya kazi yamekuwa yakikiukwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini majibu ya Mhe. Waziri na ninashukuru kabla hajenda kujibu hoja aliniletea kama alivyosema mwenyewe pale nakala ya *e-mail* ambayo aliwasiliana na uongozi kuhusiana na suala hili.

Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kufuatilia vizuri tokea jana, kwa hivyo amenitaka kwamba suala hili nimuachie atalifuatilia baada ya kukamilika kupitisha bajeti hii. Kwa hivyo, nataka kuweka *records* sahihi tu Mhe. Mwenyekiti, kwanza aniambie kitu kimoja, ili anithibitishie na halafu tuendelee. Mhe. Mwenyekiti, hawa vijana kama kwenye *e-mail* yake ambayo ameniletea alivyoambiwa, kwamba kwanza alitajiwa kuwa wako vijana 78 na kuambiwa 48 wamekubali kusaini mikataba.

Sasa nataka nimwambie kwamba hao 48 wamesaini mikataba katika hali ya vitisho, kwamba kuambiwa kuwa wasiposaini hawatopata kazi, kwa hiyo hata hawa awaangalie Mhe. Waziri kupitia Kamisheni ya Kazi. Lakini zaidi hawa vijana ambao waliokuwa wameajiriwa katika sehemu ya ulinzi ni zaidi ya 78. Mhe. Mwenyekiti, kama atakumbuka mwaka jana nilipolileta kwake nilimpa na orodha ya vijana wale wote. Kwa hivyo, naomba alifuatilie kwa makini kuhusu idara hii.

Vile vile nimuombe anipe uhakikisho kwamba katika kipindi hichi ambacho amelifanyia kazi awasiliane na uongozi wa kampuni inayohusika kupitia Kamisheni ya Kazi, kuhakikisha kwamba wanasimamisha hatua zozote za kutaka kuwanyanyasa vijana hawa wale ambao bado hawajasaini mikataba na wale ambao wamesaini mpaka suala hili limalizike, ili kuhakikisha kama nilivyosema kwamba watu hawa wanatendewa haki sawa.

Kwa kweli haiwezekani walioajiriwa ulinzi Tanganyika walipwe mara tatu ya walioajiriwa ulinzi Zanzibar wakati kampuni ni ile ile na viwango ndivyo vile vile, na nimemtolea mifano ya mikataba jana hapa na ameliona. Kwa hivyo, nataka hilo moja alifuatilie na anihakikishie kwamba atawalindia ajira zao mpaka suala hili litakapoweza kumalizika baina ya wizara yake na kampuni hii.
Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala la vijana wa *Core Centre*, ambao pia wamejibiwa katika *e-mail* aliyonionesha hapa. Lakini nilimwambia jana vile wamekuwa wakilipwa shilingi 1,200/= kwa saa badala ya shilingi 3,000/= ilipokuwa *Core Centre* iko Dar-es-Salaam. Sasa Mhe. Waziri kwenye *e-mail* yake ile aliyoletewa ameambiwa kuwa kuna 10 *percent* inalipwa *Zanzibar University* kwa ajili ya ku-*facilitate* lile suala.

Lakini mimi siamini kwamba katika shilingi 3,000/= shilingi 1,800/= ni 10 *percent*. Kwa hivyo, nasema na hili aniahidi kwamba atalifuatilia na kuhakikisha kuwa fursa zile ambazo zimetolewa kwa wenzao walioko Dar-es-Salaam na hapa zinatolewa na hasa ikizingatiwa kwamba Kampuni ya *ZANTEL* ni kampuni ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa, kwa hiyo ni sehemu ya wamiliki wa kampuni hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba anihakikishie Mhe. Waziri na atakaponihakikishia hilo, basi nitamuachia kwa sababu nitajua baadae wapi nitakwenda kumuhoji Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Mwenyekiti, tayari nilikuwa nimeshamuhakikishia pale kwenye *podium* na hivi sasa nipo karibu yake zaidi atanisikia.

Suala hili nimesema tuna uchungu nalo sana sote Wazanzibari, na wala hatuwezi kuona vijana wetu wa kizanzibari wanahenyeka na kuteswa au hawapati haki sawa na wenzao na ikiwezekana wapate nyingi zaidi kuliko hao wenzao.

Kwa hivyo, hili nitalifanyia kazi na nimemwambia siku ya Jumatatu nimeitisha kikao na Uongozi wa *ZANTEL* nitakaa nao. Lakini nitamuomba pia na nimeshamuandikia ki-*note* kwamba kabla ya Jumatatu sijakutana nao ule uongozi wa wale vijana niletee pale ofisini kwangu siku ya Ijumaa, ili na wao wanisaidie kunipa *information live* niwasikie na nitawauliza maswali yangu na baadaye nitakapokutana na huo Uongozi wa *ZANTEL* tutaweka mambo sawa. Kwa maana hiyo, wakae mkao wa kufanikiwa mambo yao tukijaaliwa.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na ninafurahi sana kila Mhe. Waziri mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman akisisitiza kwamba yeye ni miongoni mwa wenye uchungu wa Zanzibar, kumbe katika kusimamia maslahi ya Zanzibar msimamo wake hauna tofauti yoyote na Mhe. Mansoor Yussuf Himid.

Kwa hivyo, nadhani wale wanaompotoshea kwamba anawapotosha wananchi wa Makunduchi, wataamini kwamba wananchi wa Makunduchi wanapotoshwa na watu wengine sio na Mwalimu Haroun, kwa sababu msimamo wake ni kama wa Mhe. Mansoor Yussuf Himid katika kusimamia haki za Zanzibar katika Muungano huu. *(Makofi)*

Mhe Mwenyekiti, baada ya hilo nimepokea uhakikisho wake na nitamsaidia kama alivyoniomba kuhakikisha kwamba anawapata hawa vijana, ili baadhi yao wampatie maelezo ya kutosha na wale waliyoandika nimemkabidhi, lakini nitahakikisha kuwa atakutana nao, kwa ajili ya kumpa maelezo ya kutosha na atakapokaa na Uongozi wa *ZANTEL* waweze kupata ufumbuzi wa suala hili. Kwa hivyo, namshukuru kwa uhakikisho wake na Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0801 – | Kamisheni ya Kazi | 310,703,000/= |
| Kifungu 0901 – | Idara ya Uendeshaji na Utaratibu wa Mpango na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 149,042,000/= |
| Kifungu 1001 – | Idara ya Ushirika | 247,479,000/= |
| **Jumla ya Fungu** | | **2,679,000,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 27 – WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0601 – | Idara ya Ajira | 1,100,000,000/= |
| Kifungu 0801 – | Kamisheni ya Kazi | 49,273,000/= |
| Kifungu 1001 – | Idara ya Ushirika | 306,588,000/= |

**Jumla ya Fungu** **1,455,861,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na*
*Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Naibu Spika, kabla sijatamka hili ambalo nataka kulitamka naomba kutoa taarifa ndogo sana kwa ruhusa yako. Kwanza nawashukuru sana Wazee waliokuja kutoka Makunduchi jana kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi leo.

Jambo la pili kesho tukijaaliwa na wala sikutaka kulifanya mapema ikaonekana labda natumia njia za mkato, lakini *Inshaallah* kesho tukijaaliwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wote pamoja na Spika, wafanyakazi, kuna Futari Maalum ambayo imeandaliwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwa hiyo kadi zitatolewa na *Inshaallah* waje wafutari kesho wizarani kwangu tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo ilivyokuwa Kamati ya Matumizi, imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba Baraza lako Tukufu kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri, ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika; kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa tuliyoifanya. Lakini nisikitike kutokana na Waheshimiwa Wajumbe hamtulii kwenye Baraza. Sasa tunaomba na Katibu amechukua orodha ya wale wote ambao wamekuja na kuondoka bila ya ruhusa, basi Baraza litachukua hatua kwa mujibu wa utaratibu wa Baraza letu. *(Makofi)*

Jambo la pili kwa kuwa tulikuwa tuendelee na Hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo lakini muda umekuwa mdogo. Sasa namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atoe hoja, ili tuakhirishe kikao kabla ya wakati wake hadi hapo kesho.

**KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI**

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki mpaka kufikia muda wa kawaida kuakhirisha kikao ni mdogo, ambao hautotosha kumalizia shughuli iliopo mbele yetu. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu litengue Kanuni ya Muda, ili tuakhirishe kabla ya muda wake hadi kesho. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.
**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, ninayo matangazo mawili kabla ya kuakhirisha. Tangazo la kwanza wenzetu Waheshimiwa Wanawake kwamba yale mafunzo kwa mwezi huu wa Ramadhani hayapo.

Tangazo la pili Wajumbe wote wa Chama cha Mapinduzi tukishakuakhirisha kikao hichi tubakie humu ndani kwa dakika tano kuna jambo muhimu.

Baada ya hayo, niwashukuru na naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 26/07/2012 saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 8:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi*
*tarehe 26/07/2012 saa 3:00 asubuhi)*